JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora, S.L.P. 9080, Dar es Salaam.Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: +255(022)2115157/8, Tarakishi: +255(022)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. FA.27/249/01/2015/2016/42/01 27 Machi 2017

Mh. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P 9120
Barabara ya Barack Obama, Na.1
11400, DAR ES SALAAM.

YAH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na mabadiliko na kama ilivyoainishwa katika Sehemu ya 11(4) ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, nawasilisha kwako ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa mwaka wa fedha 2015/16 kwa ajili ya kuiwasilisha Bungeni kulingana na matakwa ya sheria.

Wako Mwaminifu,

Prof. Mussa Juma Assad.

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
(Kama ilivyoanzishwa chini ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)

Majukumu ya kisheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) na kufafanuliwa na Sheria ya Ukaguzi ya Umma, Na. 11 ya mwaka 2008 (kama ilivyorekebishwa) na kufafanuliwa na Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009.

Dira ya Ofisi
Kuwa kituo bora kwenye ukaguzi wa hesabu katika sekta ya ukaguzi wa umma.

Lengo la Ofisi
Kutoa huduma bora za ukaguzi zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji unaozingatia thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

Misingi Yetu

Kutopendelea:	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki bila upendeleo.
Ubora:	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya ukaguzi.
Uadilifu:	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha maadili ya kazi ya kiwango cha juu na kuheshimu sheria.
Kujali Watu:	Tunajali mahitaji ya wadau kwa kujenga utamaduni mzuri wa kujali wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na kuongeza tija.
Ubunifu:	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya taasisi.
Matumizi bora ya Rasilimali za Umma:	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi inayozingatia matumizi bora ya rasilimali zilizokabidhiwa kwake.

YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI v

TAFSIRI YA VIFUPISHO 1

SHUKRANI vi

DIBAJI viii

MUHTASARI KWA WAANDAMIZI x

SURA YA KWANZA... 1

UTANGULIZI NA TAARIFA ZA JUMLA 1

SURA YA PILI 10

AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA............................. 10

SURA YA TATU 13

MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA MIAKA ILIYOPITA... 13

SURA YA NNE 14

MASUALA YALIYOPEWA UZITO KATIKA UKAGUZI 14

SURA YA TANO 34

MAPITIO YA MIKAKATI NA UENDESHAJI WA KIUFANISI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA... 34

SURA YA SITA 95

MAPITIO YA UFANISI WA SEKTA YA MADINI NCHINI TANZANIA 95

SURA YA SABA 133

UKAGUZI MAALUM NA KAGUZI ZA UCHUNGUZI WA KISAYANSI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA... 133

SURA YA NANE 146

MASUALA MENGINEYO NA MATOKEO YA JUMLA YA UKAGUZI 146

HITIMISHO 154

VIAMBATISHO 155

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: gharama za uzalishaji za makampuni binafsi ya kuzalisha umeme 35
Jedwali Na. 2: Mikopo juu ya asilimia 50 ya mali zote za Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo 43
Jedwali Na. 3: Mikopo ya SACCOS Ambayo Haijalipwa.............. 57
Jedwali Na. 4: Hasara iliyoingiwa na PPF 60
Jedwali Na. 5: Makadirio ya Mzunguko wa Fedha.................... 65
Jedwali Na. 6: Mapato ambayo hayakuwasilishwa kwenye akaunti ya TPA 85
Jedwali Na. 7: Ufanisi katika Meli...................................... 87
Jedwali Na. 8: Repoti ya Utendaji Kazi 88
Jedwali Na. 9: Wastani wa muda unaotumiwa na meli katika Single Point Mooring (SPM) 88
Jedwali Na. 10: Meli zilizokaa kwa muda mrefu zikisubiri gati... 89
Jedwali Na. 11: Mchangauo wa jinsi makampuni makubwa ya uchimbaji madini Tanzania yanavyopata Hasara 112
Jedwali Na. 12: Faida Kulingana na PSA Iliyokubaliwa baina ya Serikali na PAET 124
Jedwali Na. 13: Madeni ya Serikali yaliyozidi muda wa kulipwa 148
Jedwali Na. 14: Ucheleweshaji na kutopelekwa kwa makato ya kodi 150
Jedwali Na. 15: Taasisi zilizofanya malipo bila kupatiwa risiti za kielektroniki:.. 151
Jedwali Na. 16: Madeni ya Muda Mrefu 153

SHUKRANI

Nina furaha kubwa sana kuwa, kwa mara nyingine, tumeweza kutimiza wajibu wa kikatiba wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) kuwasilisha ripoti kwa Rais mwishoni mwa mwezi Machi.

Kwa furaha kubwa natumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dk. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa msaada wake mkubwa na juhudi binafsi kuhakikisha ofisi yangu inatimiza jukumu lake kikatiba.

Shukrani zangu za dhati ziende kwa Mheshimiwa Spika na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wenyeviti pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa wakati wote kuiunga mkono ofisi yangu.

Kwa Wabia wetu wa Maendeleo, ningependa kutambua mchango wao mkubwa wa kuendelea kuzifanya kazi za ukaguzi katika katika ofisi yangu kuwa za kisasa kwa kudhamini mafunzo na kutoa zana muhimu za na msaada wa kiufundi.

Pia, natoa shukrani zangu za dhati, kwa Bodi za Wakurugenzi, Maafisa Masuuli, Wasimamizi Waandamizi na Watumishi wa Mashirika yote ya Umma kwa msaada mkubwa na ushirikiano walioonyesha katika kaguzi zetu.

Tukiwa tunajitahidi kudumisha viwango na ubora wa ripoti zetu, napongeza michango ya makampuni binafsi ya ukaguzi ambayo yamekuwa yakifanya kazi nasi kwa bidii na kwa weledi. Mchango

wao kuelekea maandalizi ya ripoti hii ni muhimu na wenye thamani kubwa.

Mwisho, napenda kuwapongeza wafanyakazi wangu wote ambao wamekuwa wakifanya kazi bila kuchoka; tena, hata nje ya muda wa ofisi, wakisukumwa na wito wa kiweledi - bila motisha yoyote ya fedha - kukamilisha shughuli za ukaguzi. Ni umakini, dhamira ya dhati pamoja na moyo wa kujitolea ambavyo vimesababisha utoaji kwa wakati wa ripoti hii.

Prof. Mussa Juma Assad
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI
27 Machi 2017

DIBAJI

Ninayo furaha na heshima kuwasilisha Ripoti Kuu ya Mwaka ya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa mwaka 2015/2016. Hili linatekeleza matakwa ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sura ya 34 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

Ripoti hii ni mkusanyiko wa masuala muhimu yaliyojitokeza katika kaguzi za Mashirika ya Umma kwa vipindi vilivyoishia tarehe 31 Desemba 2015 na tarehe 30 Juni 2016. Pia, ripoti hii imejumuisha mapendekezo yaliyotolewa kwa wasimamizi wa mashirika haya ili kupunguza mapungufu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi.

Kama ilivyokuwa kwa mwaka uliopita, nimekagua masuala ya kimkakati na ufanisi katika utendaji wa Mashirika kwa lengo la kujibu maswali muhimu ya kisera au changamoto muhimu na vikwazo vya kiutendaji ambavyo vinaathiri mikakati, mipango, na ufanisi kwa Mashirika 11 ya Umma katika Sura ya Tano ya Ripoti hii.

Kufuatia ugunduzi wa hivi karibuni katika sekta ya mafuta na gesi eneo la Mtwara, na nia ya Serikali ya kujenga uchumi imara wa viwanda nchini, hakuna shaka kuwa mustakabali wa uchumi wetu hapo baadae utategemea sekta ya uchimbaji mafuta na gesi na madini (extractive industry). Mafuta na gesi asilia vitasaidia kuzalisha umeme wa kutosha, kwa gharama nafuu na wenye uhakika kwa ajili ya kuendeshea viwanda. Kwa maana hiyo, katika Sura ya Sita ya ripoti hii, nimekagua na kutathmini ufanisi wa sekta ya mafuta na madini na gesi Tanzania.

Ripoti pia inajumuisha matokeo ya kaguzi maalumu na kaguzi za kiuchunguzi (forensic audit) kwa Mashirika ya Umma zilizoombwa

na wadau mbalimbali. Kaguzi hizi zilifanyika kwa mujibu wa Hadidu za Rejea za kaguzi husika.

MUHTASARI KWA WAANDAMIZI

i. Utangulizi

Muhtasari huu unaainisha kwa kifupi masuala mahususi yaliyojadiliwa kwa kina katika ripoti hii na ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti ya Taasisi husika ili kuhakikisha kuna ongezeko la ufanisi katika utendaji wa Mashirika ya Umma.

Ripoti hii inajumuisha hoja mbalimbali zilizotolewa katika ripoti za ukaguzi za Mashirika ya Umma zinazoonesha kuwapo kwa mapungufu yanayokwamisha utendaji wa mashirika hayo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi kwa haraka. Masuala yaliyoainishwa kwa kifupi ni kama ifuatavyo:

ii. Hati za Ukaguzi na Ripoti

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2015/2016 nilikagua na kukamilisha kaguzi za mashirika 150 kati mashirika 200 yaliyotakiwa kukaguliwa. Niliweza kutoa maoni ya ukaguzi 126 kwa hesabu za mashirika ikijumuisha maoni 14 ya kaguzi za miaka ya nyuma. Kati ya kaguzi za mashirika 112 zilizokamilika na kutolewa maoni (hati) ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2015/2016, mashirika manne (4) yalipata hati yenye mashaka wakati mashirika 108 yalipata hati zinazoridhisha. Hati isiyoridhisha na hati mbaya hazikutolewa kwa shirika lolote au taasisi nyingine za umma katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha.

iii. Muhtasari wa Mapendekezo ya Kaguzi Zilizopita

Katika kufuatilia utekelezaji wa kaguzi za miaka iliyopita nilibaini kwamba, kati ya mapendekezo 53 ni mapendekezo 39 (sawa na asilimia 74) ndio ambayo yametekelezwa na hivyo kubakisha mapendekezo 14 (sawa na asilimia 26) yakiwa katika

hatua za utekelezaji. Mapendekezo haya yanapatikana katika sura ya tatu (3) ya ripoti hii.

Mapendekezo hayo ni pamoja na mapitio ya mchakato wa ubinafsishaji wa ATCL; TCAA kushindwa kutekeleza mpango wa njia za ndege; Maandalizi na mpango kazi wa mwaka katika Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mapungufu katika mkataba baina ya TICTS na TPA; Umiliki wa hisa katika Kampuni ya General Tyre (EA) na mapitio ya faida na ufanisi wa uendeshaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

iv. Maswala Yaliyopewa Uzito katika Ukaguzi

Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) ilitoa Mikopo yenye jumla ya Shilingi milioni 655 bila kuthibitisha uwepo wa makampuni yaliyokopeshwa, pia imebainika kuwa hakuna dhamana iliyowekwa kwa mkopo ya Shilingi milioni 200 iliyotolewa.

Nilibaini kwamba hakuna ushahidi unaoonesha kuwa uthamini ulifanyika kwa dhamana zilizowekwa dhidi ya mikopo yenye jumla ya Shilingi milioni 330. Kiasi cha mikopo ya Shilingi milioni 355 imetolewa kwa wateja ambao muda wa matumizi wa leseni zao za biashara ulikwisha malizika. Zaidi nimebaini kwamba mtaji wa benki umepungua kulinganisha na kiwango kinachotakiwa kama kilivyoanishwa kwenye Kanuni namba 5 na 9 za Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha.

Katika kupitia uendelevu na uendeshaji wa benki ya Twiga nilibaini kwamba mpaka kufikia mwisho wa mwaka wa fedha, benki ya Twiga ilikuwa imepata hasara ya Shilingi bilioni 18.7 na pia mtaji wake ulipita kiwango cha chini cha bilioni tano ambacho kimeainishwa kwenye Kifungu cha 17 cha Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha.

Katika ukaguzi wa TANAPA nilibaini kwamba Mamlaka ilishindwa kukamilisha miradi ya maendeleo yenye gharama ya Shilingi milioni 756.89. Ilibainika kwamba utekelezaji wa miradi hiyo

ulisimamishwa kutokana na migogoro ya ardhi pamoja na mkandarasi kutotimiza wajibu wake kama ilivyooneshwa kwenye mkataba. Pia nilibaini kwamba Mamlaka haina utaratibu wa kuhakiki usahihi wa taarifa za mapato wanazopokea kutoka kwa wamiliki wa hoteli, nyumba za kupangisha na kambi za kulala watalii.

Nilibaini kwamba utekelezaji wa mradi wa awamu ya kwanza wa Mfumo wa Usimamizi wa Anga (ADS-B) wenye thamani ya Shilingi bilioni 3.4 unaofanywa na Mamlaka ya Anga Tanzania (TCAA) umekuwa wa kusuasua. Hii imesababishwa na kufilisika kwa mkandarasi wa mradi huu. Pia nimebaini kuwa Mamlaka imeweza kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi wa kina wa mfumo uliofanyika hapa Tanzania na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO) kwa asilimia 57.28 tangu mwaka 2013, hali ambayo inatishia usalama wa anga.

v. Tathmini ya Ufanisi wa Kimkakati na Uendeshaji wa Mashirika ya Umma

Ukaguzi niliofanya kutathmini ufanisi wa utendaji wa mashirika ya umma ulibainisha masuala makuu yafuatayo:

TANESCO ina malimbikizo makubwa ya madeni katika manunuzi ya umeme kutoka kwa wazalishaji huru wa nishati (IPPs) na Wazaluishajiwa dharura wa nishati (EPPs) watano. Hii imesababishwa na, TANESCO kununua umeme kwa bei ya wastani wa Shilingi 544.65 na kuuza kwa Shilingi 279.35 kwa kila uniti hivyo kusababisha hasara ya Shilingi 265.30 kwa kila uniti. Jitihada zaidi zinahitajika kuliokoa shirika katika hali liliyopo kwa kutafuta nishati mbadala yenye bei nafuu kama matumizi ya umeme unaozalishwa kwa maji na nishati ya gesi na kuachana na wazalishaji binafsi wanaotumia mafuta.

Wizara ya Nishati na Madini inadaiwa na TANESCO kodi ya pango ya Shilingi bilioni 1.12. Kushindwa kulipa deni hili kunaweza kuongeza hali mbaya ya kifedha ya Shirika.

Nilibaini hali ya kushuka kwa mapato ya uwekezaji kwa kiasi kikubwa inayoikabili mifuko ya pensheni ya NSSF, PPF, PSPF na LAPF inatokana na kutokuwepo kwa ufanisi wa menejimeti katika kusimamia mikopo iliyotolewa kwa vyama vya ushirika wa kuweka na kukopa, Usimamizi hafifu wa kuratibu na kudhibiti madeni ya muda mrefu na kuchelewa kulipwa kwa madeni ambayo mifuko inaidai serikali.

TCRA ina upungufu wa vituo vya kusimamia mfumo wa masafa vinavyotembea, kadhalika hakuna utaratibu wowote wa kuhakikisha makampuni yote binafsi yaliyopo Tanzania yanatumia mfumo wa 'dot tz' (.tz) na hakuna Mpango wa kibiashara kuweza kurahisisha utekelezaji wa mpango wa kujisajili katika mfumo wa 'dot tz'. Mamlaka inashindwa kusimamia taarifa za intaneti, matumizi ya muda wa maongezi na watumiaji ambao hawajasajiliwa na wasiokuwa na vibali halali, hii inasababisha Mamlaka kukosa makadirio sahihi ya mapato ya kodi yanayotokana na utoaji huduma wa mawasiliano.

Nilibaini mapungufu makubwa katika mkataba ulioingiwa kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na 'Mlimani City holding' yaliyosababisha muda wa miaka kumi kupita bila utekelezaji wa matakwa ya makubaliano ikiwa ni pamoja na kujenga hoteli ya kiwango cha nyota 3 na kuboresha bustani ya mimea ya Chuo. Vile vile, nimebaini kuwa Chuo inapata asilimia 10 kutoka katika kodi ya pango inayotozwa kwa wapangaji (ambayo haijumuishi gharama za huduma na uendeshaji) badala ya kutoza kwenye pato la jumla la kodi ya jengo kama ilivyoainishwa kwenye memoranda ya makubaliano.

Nilibaini kupungua kwa ufanisi katika uendeshaji katika maeneo kadhaa kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania, ambapo Mamlaka imeonesha kupungua kwa kiwango cha utekelezaji wa shughuli zake kulinganisha na malengo waliyojiwekea. Miongoni mwa viashiria hivi ni muda wa meli kukaa bandarini, ambapo kiwango

cha wastani cha sasa cha meli kukaa bandarini ni siku 6.1 mpaka 8.6 ambapo ni chini ya kiwango kinachokubalika cha siku 5. Pia meli huchukua siku 4 katika sehemu ya gati badala ya siku 3 zinazokubalika. Mapungufu haya yanaleta athari katika utoaji wa huduma.

Mamlaka ya Bandari inakabiliwa na tatizo la utoaji mdogo wa mafuta katika gati za mafuta za KOJ na SPM, kutokana na umbali wa kutoka SPM au KOJ kwenda kwenye matenki ya kupokelea mafuta.

Pia Mamlaka inaendelea kushusha mafuta kuelekea katika matenki ya kuhifadhi mafuta kupitia gati ya KOJ bila kutumia mita za kupimia mafuta hivyo kuathiri mapato ya Mamlaka.

vi. Ukaguzi wa Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Madini;

Ukaguzi niliofanya katika sekta ya Madini ili kuishauri serikali jinsi ya kuongeza mapato ulibaini mambo yafuatayo:

Mikataba ya madini ina vifungu vinavyoathiri maslahi ya umma kama vile masharti yasiyoridhisha katika kuongeza mikataba, vifungu vinavyozuia mabadiliko ya sheria kuathiri mikataba husika, sera zisizoridhisha katika miamala ya fedha za kigeni na forodha, motisha za kodi ziliozidi kwenye taratibu za kodi na kihasibu katika manunuzi ya vifaa vya uchimbaji.

Pia nilibaini kuwa, wachimbaji wadogo wengi hawalipii leseni za uchimbaji madini kwa mwaka na mrabaha kama inavyotakiwa na Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

Nimebaini kuwa, kifungu cha 21 cha Sheria ya madini ya Mwaka 2010 kimeondoa mamlaka ya kutafiti na kujihusisha na tafiti za madini kwa Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) hivyo kuathiri usiamamizi wa serikali kwenye shughuli za utafiti wa madini zinazofanywa na makampuni binafsi.

Pia nilibaini kuwa, kuna mapungufu kadhaa kwenye ubia kati ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na 'Tanzanite One Mining Limited' ikiwa ni pamoja na kutofanyika kwa vikao vya Kamati ya pamoja ya uendeshaji wa mgodi (Joint Operation Committee), kuchelewa kufunguliwa kwa Akaunti ya Pamoja na Akaunti ya ukarabati wa mazingira ya mgodi, Kutofanyika kwa Biashara ya Grafiti na Marumaru, uongezaji thamani na utafutaji masoko ya Tanzanite kufanywa na kampuni inayoendesha mgodi kinyume na makubaliano ya ubia, Changamoto ya uhalisia wa bei ya Tanzanite kutokana na ushiriki wa makampuni tanzu katika kuuza na kununua madini ya tanzanite.

Ukaguzi kwenye shughuli za mgodi wa dhahabu wa Buckreef kupitia Mkataba wa ubia kati ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Kampuni ya TANZAM 2000 ulibaini kuwa mwaka 2011 TANZAM (2000) ililipa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 3 kwa STAMICO kama gharama za kununua asilimia 55 ya thamani ya mgodi bila ya kuwa na vigezo vinavyotambulika kama uthaminishaji wa mali za mgodi kabla ya ubia. Zaidi ya hayo, tangu mwaka 2011 hadi wakati wa Ukaguzi huu, Januari, 2017 mgodi ulikuwa haujaanza kufanya kazi.

Ukaguzi wangu kwenye shughuli za uendeshaji wa mgodi wa makaa ya mawe wa Kiwira ulibaini kuwa, Mgodi haujaanza shughuli za uchimbaji tangu ulivyorudishwa kwenye umiliki wa serikali mwaka 2004 kutokana na changamoto za kifedha na maswala ya kisheria yaliyochagizwa na kushindwa kuhamisha jina la umiliki wa mgodi kutoka kwa mwekezaji wa awali ambaye ni Tan Power Resources Ltd kwenda Shirika la Madini la Taifa (STAMICO).

Mapitio yangu ya marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani na Kodi ya Makampuni yanayohusu migodi mitano ya Geita Gold Mine, Bulyanhulu Gold Mine, North Mara Gold Mine na Pangea Gold Mine kwa miaka mitano kuanzia 2012 hadi mwaka 2016 ulibaini rejesho la Kodi ya Ongezeko la Thamani ya kiasi cha

Shilingi trilioni 1.14 iliyosababishwa na Kampuni za Madini kutotozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa madini yanayosafirishwa nje ya nchi. Pia, kutokulipa kodi ya makampuni kutokana na hasara mfululizo makampuni iliyosababishwa na kuruhusiwa kutoa kwa asilimia 100 gharama za vifaa vya uchimbaji. Pia nilibaini kuwa Serikali inapoteza mapato kwa kutoza kiwango kidogo cha Kodi ya Zuio katika Gharama za Menejimenti kutoka kampuni tanzu kwa mujibu wa Mikataba ya Madini.

Mafuta na Gesi;
Mapitio yangu ya sekta ya Gesi na Mafuta yalibaini mambo yafuatayo:

Ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam ulifanywa bila kutambua wateja jambo lililopelekea TPDC hadi sasa kuwa na mnunuzi mmoja tu ambaye ni TANESCO na kusababisha mapato yatokanayo na uuzaji wa gesi kuwa ya kiwango cha chini kuliko ilivyotizamiwa.

Pia nilibaini, matumizi ya bomba ya kiwango cha chini cha ujazo kwa asilimia 94 huku TANESCO akiwa ndiye mteja pekee akitumia wastani wa futi za ujazo milioni 46.61 ambayo ni sawa na asilimia 6 tuu ya ujazo wa bomba husika licha ya kuwepo makubaliano kati ya TPDC na TANESCO ya kusambaza futi za ujazo milioni 138.8 katika vituo 6 vya kuzalisha umeme vya TANESCO.

Pia nilibaini TPDC inatoza gharama sawa ya Dola za Kimarekani 5.14/mmBTU kwa wateja wote bila kuzingatia umbali wa mteja kutoka kwenye chanzo cha gesi.

Hata hivyo, kuna deni la Dola za Kimarekani Milioni 61.35 (Shilingi bilioni 133.37) ambalo Shirika la TANESCO halijailipa TPDC bila kuwepo dhamana ya deni hilo.

Mapitio zaidi ya bei ya gesi yalibaini kuwa bei ya Dola za Kimarekani 5.14/mmBTU ambayo TPDC inaitoza TANESCO ni kubwa kulinganisha na ile ya Dola za Kimarekani 3.5/mmBTU ambayo Kampuni ya Pan African Energy Tanzania Limited (PAET) inaiuzia TANESCO. Hii inaweza kufanya wateja wengi ikiwa ni pamoja na TANESCO kununua gesi kutoka katika chanzo nafuu hivyo kuathiri utendaji wa TPDC kutokana na kukosa mapato.

Pia nilibaini kuwa, Mkataba wa Ubia wa Uzalishaji wa Gesi (PSA) baina ya TPDC na Kampuni ya Pan African Energy Tanzania Limited (PAET) umetengenezwa kwa namna ambayo gawio la Serikali kutoka kwenye mauzo ya gesi asilia litakuwa linapungua kadri uzalishaji unavyoongezeka. Pia, TPDC na PAET, wana mgogoro tangu tarehe 30 Novemba 2012, wa gharama Dola za Kimarekani milioni 34 zilizotakiwa kurejeshwa.

vii. Taarifa ya Kaguzi Maalumu na Kaguzi za Kiuchunguzi Zilizofanyika katika Mashirika ya Umma

Ifuatayo ni taarifa fupi ya kaguzi maalum na kaguzi za kiuchunguzi zilizofanyika katika mashirika ya umma kwa mwaka 2015/2016:

Ukaguzi Maalum Juu ya Usimamizi wa Ardhi na Majengo yanayomilikiwa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogovidogo (SIDO) ulilenga kuhakiki uhalali na usahihi wa thamani ya Ardhi na Majengo, umiliki wa mali hizo na kutathmini misingi ya mchakato wa uuzaji wa mali hizo. Ukaguzi ulibaini mabadiliko ya umiliki wa Viwanja 25 vya SIDO ambao haukufuata taratibu za kisheria uliofanywa na Halmashauri za Wilaya za Kinondoni, Mtwara, Mbeya na Moshi. Pia ukaguzi ulibainisha uuzaji wa viwanja vitano (5) vya SIDO vyenye Na.09 na 10 Kitalu "X" Mwakibete, Mbeya na viwanja Na.673 - 675 Kitalu 46 Kijitonjama, Dar es Salaam kwa watu binafsi na Mfuko wa Pensheni wa PPF bila kufuata utaratibu.

Pia nilifanya ukaguzi maalumu kwenye ubia kati ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na kampuni ya uchimbaji madini ya Tanzanite One (TML). Ukaguzi huu ulijikita katika kukagua iwapo TML (Mwendeshaji) alikuwa na udhibiti wa ndani katika kutekeleza uendeshaji wa Ubia huo. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Wizara ya Nishati na Madini ilitoa ridhaa ya mauzo ya hisa 50% za TML (mbia wa Serikali) zilizokuwa zikimilikiwa na M/s Richland Resources Ltd kwenda kwa M/s Sky Associates Ltd bila kufanya upembuzi yakinifu juu ya uwezo wa kifedha na kiufundi wa M/s Sky Associates katika kufanya shughuli za uchimbaji wa madini ya Tanzanite.

Vile vile nilibaini kuwa, hapakuwa na Akaunti ya pamoja ya mauzo kama inavyotakiwa na mkataba hivyo mapato yote ya mauzo ya Tanzanite yaliingia katika akaunti zinazomilikiwa na TML. Hivyo kufanya STAMICO ambaye ni mmiliki wa asilimia 50 katika ubia kutokuwa na udhibiti wa mapato na taarifa ya mauzo ya Tanzanite.

Ukaguzi Maalumu Kuhusu Malipo ya Ushuru Forodha kwenye Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) ulilenga kubaini waliohusika katika ukwepaji wa ushuru wa forodha na kubaini kiwango cha hasara iliyotokana na ukwepaji wa ushuru huo. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, ushuru wa Shilingi bilioni 15.02 haukukusanywa na Mamlaka ya Bandari kutokana na ubadhirifu wa makampuni ya kutoa mizigo bandarini, wafanyakazi wa Mamlaka ya bandari na watumishi wa mabenki.

Pia nilifanya Ukaguzi Maalum wa Ubia kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na ETC Holding Limited (ETC) wenye lengo kuu la kubaini kama makubaliano ya ubia yalitekelezwa kwa mujibu wa madhumuni yaliyokusudiwa. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa mkataba wa ubia Kati ya NDC na ETC ulitiwa saini bila Mapitio na Ridhaa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia, mabadiliko ya umiliki wa Kiwanja Na.1-66 Kitalu "R" kwenda kwa M/s ETC Cargo Ltd haukupata idhini ya Bodi ya Wakurugenzi wa

NDC wala ridhaa ya Msajili wa Hazina. Pia Kiwanja Na.101 Kitalu "Q" kilikodishwa kwa miaka 98 kwa ETC Cargo Ltd bila idhini ya Bodi ya Wakurugenzi.

viii. **Taarifa ya Masuala Mengineyo na Matokeo ya Jumla ya Ukaguzi**

Kwa mwaka huu wa ukaguzi, kulikuwa na Bodi 18 ambazo zimemaliza muda wake na hakuna Bodi mpya zilizochaguliwa mpaka ninapokamilisha ukaguzi wangu mwezi Machi 2017. Baadhi ya taasisi zimekuwa zikiendelea na utendaji wa kazi bila ya Bodi kwa zaidi ya mwaka mmoja.

Kaguzi za Mifuko ya Pensheni, zimebaini kuwa Mifuko bado haijapokea majina na taarifa za wafanyakazi hewa kutoka Hazina na hakuna uhakiki binafsi uliofanywa na menejimenti za Mifuko ili kutambua deni linalotokana na michango ya wafanyakazi hewa. Kuna uwezekano wa kuwepo deni kwa Mifuko linalotokana michango ya wafanyakazi hewa.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16 imebainika ya kwamba, serikali inadaiwa Shilingi bilioni 1.60 kwa madeni yaliyozidi muda wake wa kulipwa kutoka Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Madeni haya yanatokana na mikopo ya moja kwa moja, dhamana, na michango ambayo haikuwasilishwa kulingana na matakwa ya kisheria.

Tathmini ya makato ya kisheria ilibaini kuwa, baadhi ya mashirika hayakupeleka makato yake katika muda uliowekwa kisheria. Makato hayo yanajumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Kodi Kadri ya Kipato chako (PAYE), michango ya pensheni pamoja na Kodi ya Mafunzo na Maendeleo (SDL) yenye thamani ya Shilingi bilioni 26.26.

Pia nilibaini kuwa, taasisi mbalimbali za Serikali zilifanya malipo ya Shilingi bilioni 5.61 bila kupatiwa Ankara/risiti za kielectroniki (EFD).

Ukaguzi ulibaini jumla ya madeni Shilingi bilioni 61.28 yanayodaiwa na mashirika na taasisi mbalimbali kutoka kwa wateja wake. Madeni hayo yamepita ukomo wake kama iivyoelekezwa katika Ankara na sera za kusimamia ukusanyaji wa maduhuli za mashirika husika.

SURA YA KWANZA

TAFSIRI YA VIFUPISHO

ADS-B	Mfumo wa Usimamizi wa Anga
AFROSAI-E	Umoja wa Ofisi za Taifa za Ukaguzi za Nchi za Kiafrika Zinazozungumza Lugha ya Kiingereza
AMHS	Mfumo wa Utunzaji wa Mawasiliano ya Ndege
AOC	Cheti cha Mwendeshaji wa Huduma za Ndege
ATC	Shirika la Ndege Tanzania
ATCL	Kampuni ya Ndege Tanzania
ATM	Mfumo wa Usimamizi wa Safari za Ndege
BoT	Benki Kuu ya Tanzania
CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali
CBE	Chuo cha Elimu ya Biashara
CDA	Mamlaka ya Uendelezaji wa Makao Makuu
CHC	Shirika Hodhi ya Mali za Serikali
CMS	Mfumo wa Usimami wa Forodha
CMSA	Mamlaka ya Masoko ya Mitaji
COSTECH	Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania
DAWASCO	Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam
DIT	Chuo cha Teknolojia Cha Dar es Salaam
DUCE	Chuo Kikuu Kishiriki Cha Elimu Dar es Salaam
EADB	Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki
EFD	Kifaa cha Ukusanyaji Fedha cha Kielektroniki
EWURA	Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Nishati na Maji
GmbH	Kampuni Ambayo Dhima ya Deni ya Wamiliki Inabaki kwenye Mtaji Wanaomiliki tu
HESLB	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu
IAS	Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu

IATA	Jumuiya ya Usafirishaji wa Anga ya Kimataifa
ICAO	Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga
ICD	Bandari Kavu
IFAC	Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu
IFM	Chuo cha Usimamizi wa Fedha
IFRS	Mfumo wa Kimataifa wa Kutoa Taarifa na Uandaaji wa Hesabu
IOSA	Ukaguzi wa Usalama Viwanjani wa Kimataifa
IPSASs	Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Taasisi za Umma
ISA	Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu
ISSAIs	Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu wa Taasisi za Umma
KOJ	Gati ya Kupakulia Mafuta ya Kurasini
KPI	Kiashiria cha Utendaji
LAPF	Mfuko wa Pensheni wa LAPF
LCMS	Mfumo wa Kusimamia na Kudhibiti Mawasiliano ya Ndani
MNH	Hospitali ya Taifa ya Muhimbili
MOI	Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili
MoU	Randama za Makubaliano
MSD	Bohari Kuu ya Dawa
MUCCOBs	Chuo cha Ushirika na Biashara Moshi
MUST	Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya
MWAUWASA	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza
NACTE	Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi
NAOT	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi
NARCO	Kampuni ya Ranchi za Taifa
NBC	Benki ya Taifa ya Biashara
NCAA	Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro
NDC	Shirika la Maendeleo la Taifa
NECTA	Baraza la Mitihani la Taifa

NHC	Shirika la Nyumba la Taifa
NHIF	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya
NIMR	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu
NIT	Taasisi ya Taifa ya Usafirishaji
NSSF	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii
OUT	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
PA &oBs	Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma
PAA	Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008
PAC	Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali
PAYE	Lipa Kodi Kadri ya Pato Lako
PMG	Mlipaji Mkuu wa Serikali
PPF	Mfuko wa Pensheni wa PPF
PPP	Ushirikiano wa Taasisi za Umma na Binafsi
PPRA	Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma
PRIDE	Taasisi ya Kukuza Maendeleo Vijijini
PSPF	Mfuko wa Pensheni wa Sekta ya Umma
PSRC	Tume ya Rais ya Kurekebisha na Kubinafsisha Mashirika ya Umma
RAHCO	Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli Tanzania
SACCOS	Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo
SAI	Taasisi ya Ukaguzi ya Taifa
SPM	Kiwanda cha Karatasi Kusini
SSRA	Mamlaka ya Udhibiti ya Hifadhi za Jamii
SUMATRA	Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi kavu na Majini
TAFIRI	Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania
TANAPA	Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa
TANCIS	Mfumo wa Pamoja wa Forodha wa Tanzania
TANESCO	Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania
TBC	Shirika la Utangazaji Tanzania
TBS	Shirika la Viwango Tanzania
TCAA	Mamlaka ya anga Tanzania

TCB	Bodi ya Pamba Tanzania
TCRA	Mamlaka ya Udhibiti Mawasiliano Tanzania
TFDA	Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania
TICTS	Kituo cha Huduma za Makontena ya Kimataifa
TPA	Mamlaka ya Bandari Tanzania
TPDC	Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania
TPRI	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa
TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania
TSN	Kampuni ya Magazeti Tanzania
TTCL	Kampuni ya Simu Tanzania
TTMS	Mradi wa Mfumo wa Usimamizi wa Nyendo za Mawasiliano ya Simu
TZS	Shilingi ya Tanzania
UCSAF	Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote
UDOM	Chuo Kikuu Cha Dodoma
UTT-AMIS	Mfuko wa Uwekezaji Tanzania wa kusimamia Mali na Uwekezaji
UTT-PID	Mfuko wa Uwekezaji Tanzania wa Kusimamia Miradi na Maendeleo ya Ujenzi
VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani
WHC	Kampuni ya Nyumba za Watumishi

UTANGULIZI NA TAARIFA ZA JUMLA

1.0 Uanzishaji wa Ofisi ya Ukaguzi Kisheria

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni Ofisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara). Ibara ya 143 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008 na kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.7 ya Mwaka 2011 inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma angalau mara moja kwa mwaka wa fedha.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ana mamlaka ya kufanya ukaguzi wa hesabu na ukaguzi wa thamani ya fedha au kaguzi nyingine katika Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kama ilivyoainishwa kwenye vifungu Na. 26, 27, 28 na 29 vya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008. Kifungu cha 12 cha Sheria hiyo kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kutoa maoni kwa nia ya:

- Kuzuia au kupunguza matumizi ya fedha za umma yasiyokuwa na tija;
- Kuongeza makusanyo ya maduhuli ya umma;
- Kuzuia hasara inayoweza kutokea kwa uzembe, wizi, kukosa uaminifu, udanganyifu, au rushwa kuhusiana na fedha na rasilimali za umma;
- Kuongeza uchumi, tija na ufanisi katika matumizi ya fedha za umma.

Mashirika na Taasisi Nyingine za umma nchini zinafanya kazi kwa kutumia mifumo ya uhasibu (accrual basis of accounting) ambayo inayalazimu kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IFRSs) au Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSASs). Miongozo zaidi ya kisheria inayotumika kuandaa hesabu ni pamoja na Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002 au sheria yeyote iliyopitishwa na Bunge ya kuanzishwa kwa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008.

Sheria namba 418 ya Msajili wa Hazina na kifungu cha 6 cha Sheria ya Mashirika ya Umma namba 16 ya mwaka 1992 zinahusiana na majukumu ya Msajili wa Hazina katika Mashirika ya Umma. Sheria hizo zinaelezea kuwa Msajili wa Hazina ana kazi na jukumu la kusimamia vyema uendeshaji wa shughuli za Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa kushirikiana na Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika husika. Vyombo vyote hivyo vinafanya kazi katika kusimamia na kuongoza kwa ukaribu Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa ufanisi na kwa kutoa maelekezo ya kiusimamizi.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha ripoti za mwaka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Katika kanuni ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma, ripoti hizo zinatakiwa kuwasilishwa kwa Rais ifikapo tarehe 31 Machi ya kila mwaka. Baada ya kupokea ripoti hizo, Rais atawataka wahusika kuwasilisha ripoti hizo Bungeni ndani ya siku saba tangu kuanza kwa kikao cha kwanza cha Bunge.

Kama Rais hatachukuwa hatua zozote za kuwasilisha taarifa hizo Bungeni, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu atawasilisha nakala za ripoti hizo kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano (au Naibu Spika

ikiwa kiti cha Spika kiko wazi wakati huo au ikiwa kwa sababu yeyote Spika hawezi kutekeleza majukumu yake) ambaye atawasilisha ripoti hiyo Bungeni. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inayohusu Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma itajadiliwa kwanza na Kamati za Bunge za Hesabu (PAC) kwa niaba ya Bunge na kuandaa ripoti ambayo itawasilishwa Bungeni.

1.1 Wigo wa Ukaguzi na Viwango vya Ukaguzi Vinavyotumika

1.1.1 Wigo na Madhumuni ya Ukaguzi

Madhumuni ya kufanya ukaguzi ni kumuwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serekali kutimiza jukumu la kutoa maoni huru kuhusu hesabu za Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa mwaka 2014/2015 ili kuona iwapo zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu. Ukaguzi huu unahusiana na hesabu zilizokaguliwa kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Desemba, 2015 na tarehe 30 Juni, 2016.

Wigo wa ukaguzi wangu unajumuisha tathmini ya ufanisi wa mifumo ya kihasibu na udhibiti wa ndani katika shughuli za taasisi husika. Pia unahusisha ukaguzi na uhakiki wa hesabu, ripoti za utekelezaji, na taratibu nyingine za kikaguzi ambazo ni muhimu katika kukamilisha ukaguzi. Ukaguzi huu ulifanyika kwa kuzingatia viashiria vya hatari na kiwango cha juu cha miamala kinachokubalika “risk and materiality”. Kwa hiyo, matokeo ya ukaguzi yanatokana na kiwango ambacho kumbukumbu, nyaraka, na taarifa zilizoombwa kwa madhumuni ya ukaguzi na zikawasilishwa kwangu.

1.1.2 Viwango vya Ukaguzi Vilivyotumika

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni mwanachama katika Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi Duniani (INTOSAI), Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi za Nchi za Afrika (AFROSAI) na Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi kwa Nchi za Afrika Zinazoongea Kiingereza (AFROSAI-E). Hivyo, Ofisi inatumia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi vya Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi Duniani (ISSAI) vinavyotolewa na "INTOSAI" na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu (ISA) zilizowekwa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC).

1.2 Majukumu ya Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma

Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyingine za umma zina jukumu la kutayarisha kwa usahihi hesabu kama inavyotakiwa katika Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu (IFRSs) au Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSAS). Majukumu hayo yanajumuisha:

- Kuhakikisha taarifa za hesabu zinaandaliwa kwa kiwango cha kimataifa ikiwa ni pamoja na kubuni, kutekeleza, na kudumisha mifumo thabiti ya ndani itakayowezesha kuwandaa mahesabu yaliyo huru, yasiyo na makosa, wala mapungufu yatokanayo na udanganyifu;
- Kuchagua na kutumia sera sahihi za uandaaji wa mahesabu; na
- Kufanya makadirio ya mahesabu yanayoendana na mazingira halisi.

Viwango vya Kimataifa vya Kihasibu (IAS 1) na viwango vya Kitaifa vya Utayarishaji wa Hesabu za Taasisi za Umma (IPSAS 1) vinaainisha aina za hesabu zinazotakiwa kuwandaliwa na taasisi hizi.

1.3 Mpangilio na Uteuzi wa Makampuni Binafsi kwa Kazi ya Ukaguzi

Ili Ofisi yangu iweze kutimiza majukumu ya ukaguzi kwa ufanisi katika Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma nchini, kaguzi za baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma yamekaguliwa na makampuni binafsi ya ukaguzi kwa niaba yangu. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 33 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, ambacho kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kumruhusu mtu au kampuni yeyote iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Wakaguzi wa Hesabu na Wahasibu Na. 33 ya Mwaka 1972 iliyorekebishwa mwaka 1995 kufanya ukaguzi kwenye Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa niaba yake.

Kulingana na Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, wakaguzi watakaoteuliwa watafuata sheria kama inavyotakiwa na pia hawatatoa siri za mashirika wanayoyakagua. Wajibu wa kutoa hati ya ukaguzi unabaki kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kaguzi zitakazofanywa na Makampuni binafsi zitahakikiwa ubora wa kazi zake na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT).

SURA YA PILI

AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

2.0 Utangulizi

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi Namba 200 (ISA 200), lengo la kufanya ukaguzi wa hesabu ni kumwezesha Mkaguzi kutoa hati ya ukaguzi inayoeleza iwapo hesabu zinaonyesha hali halisi ya kifedha ya Shirika na kama zimeandaliwa kwa kufuata viwango na mfumo unaokubalika. Ukaguzi wa hesabu unafanyika ili kumuongezea imani mtumiaji wa hesabu husika kwamba zimetengenezwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika. Hivyo, kumfanya Mkaguzi kupata sababu za uhakika kwamba hesabu kwa ujumla wake hazina makosa na pia kutoa taarifa ya matokeo ya ukaguzi.

2.1 Aina za Hati za Kaguzi Zilizotolewa

2.1.1 Hati Inayoridhisha

Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu, na vile vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania au viwango vingine vya utoaji wa taarifa za fedha vinavyokubalika kimataifa.

2.1.2 Hati Yenye Shaka

Aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anapokutana na mazingira ya kutokukubaliana na Menejimenti au mazingira yenye shaka ambayo yana athari lakini si za kimsingi katika usahihi wa hesabu. Maelezo ya hati yenye shaka yanafanana sana na hati

inayoridhisha lakini aya ya ufafanuzi inaongezwa ili kuelezea sababu zinazoleta shaka.

Hivyo, hati itaonyesha kuwa hesabu kwa ujumla zinaonesha vizuri uandaaji wa hesabu isipokuwa kwa kasoro zitokanazo na masuala yaliyohojiwa.

2.1.3 Hati Isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha inatolewa pale Mkaguzi anapoona kuwa, taarifa za fedha za Shirika au Taasisi Nyingine za Umma kwa kiasi kikubwa zina makosa, na zikiangaliwa kwa ujumla wake zinakuwa hazikufuata viwango vinavyokubalika vya uandaaji wa hesabu.

2.1.4 Hati Mbaya

Aina hii ya hati ni mojawapo ya sababu zinazoweza kubadilisha hati ya ukaguzi. Hati hii hutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu hesabu zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo inaathiri hesabu kiasi cha kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kuhusiana na hesabu hizo.

2.1.4.1 Aya za Msisitizo wa Jambo Kwenye Ripoti ya Mkaguzi

Aya za msisitizo wa jambo hujumuishwa kwenye ripoti ya mkaguzi kwa lengo la kutoa maelezo ya ziada kwa watumiaji wa taarifa za hesabu ili kuvuta umakini wa watumiaji husika kwa jambo ambalo limeoneshwa au kuwainishwa kwenye taarifa ya fedha, na ambalo limeonekana kuwa ni muhimu na la msingi kwa ajili ya kuleta uelewa wa taarifa hizo kwa ajili ya kufanya maamuzi yenye tija.

Ujumuishaji wa suala lenye msisitizo kwenye ripoti ya mkaguzi hauathiri hati ya ukaguzi iliyotolewa na mkaguzi; na si mbadala wa: (a) Hati Isiyoridhisha, Hati yenye shaka na hati mbaya iliyotolewa na mkaguzi pale inapohitajika kutokana na mazingira maalumu ya ukaguzi; au (b) Masuala ambayo yanaonyeshwa

kwenye taarifa ya fedha ambayo Menejimenti ilipaswa kufanya kutokana na mahitaji au matakwa ya mfumo uliokubalika wa uaandaaji wa taarifa za hesabu.

2.2 Maoni ya Ukaguzi yaliyotolewa katika kipindi cha mwaka

Katika kipindi cha mwaka ninaoripoti, kulikuwa na jumla ya hati za ukaguzi 112, kati ya hizo; zinazoridhisha 108; Pia, kulikuwa hati nne (4) zenye mashaka zilitolewa; na hapakuwa na hati yoyote mbaya.

2.3 Muelekeo wa Hati za Ukaguzi

Uchambuzi wa muelekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Mashirika ya Umma kwa muda wa miaka mitano kuanzi 2011/2012 mpaka 2015/2016 ni kama ifuatavyo:-

Jedwali Na. 1: Muelekeo wa Hati za Ukaguzi

Aina ya Hati ya Ukaguzi	Ripoti ya Mwaka				
Mwaka wa hesabu	**2011/2012**	**2012/2013**	**2013/2014**	**2014/2015**	**2015/2016**
Zinazoridhisha	85	92	117	107	108
Zenye mashaka	9	1	3	5	4
Isiyoridhisha	1	0	1	0	0
Mbaya	0	0	0	0	0
Total	**95**	**93**	**121***	**112****	**112**

*** Inajumuisha hati za ukaguzi nne (4) ambazo hazikuwepo mwaka 2013/2014 na 2014/2015**

****Inajumuisha hati za ukaguzi kumi (10) ambazo hazikuwepo za mwaka 2014/2015**

SURA YA TATU

MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA MIAKA ILIYOPITA

3.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha muhtasari wa mapendekezo ya Ripoti za Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa miaka iliyopita; ambayo bado hayajatekelezwa au yapo kwenye hatua za utekelezaji hadi ilipofikia wakati wa kuandaa taarifa hii.

3.1 Majibu ya Ripoti za Ukaguzi za Miaka Iliyopita

Mwezi Julai, 2016 nilipokea majibu ya Serikali ya ripoti ya mwaka uliopita kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Ninapenda kutambua juhudi zilizofanywa na Mlipaji Mkuu wa Serikali katika kujibu na kuandaa mpango wa utekelezaji wa masuala na mapendekezo yaliyotolewa kwa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma. Tathmini ya majibu imeonyesha kuwa mapendekezo mengi bado hayajatekelezwa na mengine yapo kwenye hatua za utekelezaji. Kwa hali hiyo, hatua za ziada zinahitajika katika utekelezaji wa mapendekezo hayo ili menegimenti za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine ziweze kuwajibika juu ya matumizi ya rasilimali za umma.

Napenda kurejea mapendekezo yote niliyoyatoa katika ripoti zilizopita ambayo hayajatekelezwa au yametekelezwa kwa kiwango kidogo na Mashirika ya Umma husika kama inavyoonekana kwenye viambatisho V(a) na V(b).

SURA YA NNE

MASUALA YALIYOPEWA UZITO KATIKA UKAGUZI

4.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha masuala muhimu yaliyojitokeza wakati wa Ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine pamoja na Mapendekezo ya nini kifanyike ili kutoa ufumbuzi wa masuala hayo. Masuala hayo yamegawanyika katika sehemu mbili, yale yaliyozihusu taasisi moja moja na yale yaliyozihusu taasisi mbalimbali kwa ujumla.

4.1 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

4.1.1 Kukosekana kwa Mkataba na Uthibitisho wa Udhamini Kutoka kwa Serikali kwa Mkopo wa Shilingi bilioni 44.29

NHIF ilitoa mkopo wa Shilingi bilioni 44.29 kwa ajili ya kujenga kituo cha afya cha Chuo Kikuu cha Dodoma.

Hata hivyo, imebainika kuwa, mkopo huo haukuwa na mkataba wala uthibitisho wa udhamini kutoka serikalini. Kuwapo kwa mkataba kungesaidia kuweka wazi haki na wajibu wa kila upande katika mkopo huu na utaratibu wa riba na urejeshaji wa mkopo.

Kukosekana kwa mkataba na uthibitisho wa udhamini wa serikali kunaweza kuusababishia mfuko kupoteza fedha za wanachama endapo mkopaji atashindwa kuwa mwaminifu, na itakuwa vigumu kupata haki mahakamani.

Menejimenti ya NHIF inashauriwa kuhakikisha mkataba wa mkopo unaingiwa kati yake na mkopaji.Pia uthibitisho wa udhamini unapatikana kutoka serikalini. Pia, NHIF inashauriwa kuhakikisha inaingia katika mkataba kabla ya kutoa mkopo wowote mbeleni.

4.1.2 Kutorejeshwa kwa Gharama za uendeshaji za Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) Shilingi bilioni 1.20

Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) ulisaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikiitaka Serikali kutoa fedha kwa ajili ya kuendesha malengo ya Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ambayo ilihusisha gharama za kawaida za uendeshaji Mfuko.

Mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2015, NHIF ilipaswa kuwa imerejeshewa na Serikali Shilingi bilioni 1.20 kutokana na gharama ilizotumia kwenye miradi ya CHF kama ilivyoainishwa kwenye Hati ya Makubaliano. Hata hivyo, gharama hizo hazikuweza kurejeshwa na Serikali.

Kushindwa kwa Serikali kuilipa NHIF kumeuongezea Mfuko mzigo mkubwa wa kifedha. Hivyo, kusababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na kushindwa kupanua wigo wa shughuli zake.

Menejimenti ya NHIF inashauriwa kuchukua hatua za ziada ili kuhakikisha Serikali inarejesha fedha husika.

4.1.3 Kukosekana kwa Hatimiliki za Viwanja Vyenye Thamani ya Shilingi Milioni 550.71

Katika mwaka wa fedha 2013/14 na 2014/15 NHIF ilinunua viwanja saba (7) vyenye thamani ya Shilingi milioni 550.71 katika mikoa saba ya Tabora, Simiyu, Geita, Kigoma, Singida, Lindi na Kigoma. Hata hivyo, tumebaini Hatimiliki hizo hazipatikani.

Kukosekana kwa Hatimiliki kunasababisha kukosekana kwa uhalali wa umiliki wa viwanja husika. Menejimenti ya NHIF inashauriwa kuongeza juhudi za ziada ili kuzipata hatimiliki za maeneo husika.

4.2 Benki ya Wanawake Tanzania (TWB)

4.2.1 Usimamizi Mbovu wa Taratibu za Kutoa Mikopo

Kuna taratibu ambazo mkopaji anatakiwa kuzitimiza kabla ya mchakato wa kutoa mkopo haujaanza. Pia, benki inatakiwa kuhakikisha vibali na uidhinishaji katika ngazi zote unazingatiwa ikiwa ni pamoja na tathmini ya dhamana zilizowekwa na mkopaji. Taratibu hizi zinafanywa ili kulinda maslahi ya benki na kuzuia vitendo vyovyote vya udanganyifu ambavyo vinaweza kufanywa na mkopaji.

Ukaguzi wa utendaji wa benki kwa mwaka wa fedha 2014/15 umebaini hitilafu zifuatazo zinazohusiana na usimamizi wa mikopo na nyaraka.

i. Mikopo yenye jumla ya Shilingi milioni 655.00 imetolewa kwa makampuni manne bila kuthibitisha uwepo wa makampuni hayo kwa Msajili wa Makapuni kinyume na Aya ya 3.3.3 ya Muongozo wa usimamizi wa mikopo wa benki (TWB). Badala yake, benki ilitakiwa kujipatia marejesho ya mwaka ya kampuni husika ili kujithibitishia uwepo wao.

ii. Kifungu cha 2.1.1 cha makubaliano ya mkopo na Aya ya 1.1.1.4 ya Mwongozo wa usimamizi wa mikopo wa TWB vinataka baadhi ya nyaraka kama hati ya dhamana isiyohamishika (mortgage deed), stakabadhi ya mkopo (debenture) na hati ya dhamana ya mali inayohamishika (chattel debenture) kusajiliwa na Msajili wa Hati/Nyaraka za

umiliki au Msajili wa Makampuni kama sehemu ya uthibitisho (documentation).

Hata hivyo, imebainika kuwa hakuna dhamana iliyowekwa kwa mkopo wa shilingi milioni 200 uliotolewa kwa mteja mmoja kwa mwaka wa fedha 2014/15 tofauti na matakwa ya miongozo ya utoaji mikopo.

iii. Kifungu cha 7.5.2 cha Sera ya Mkopo ya mwaka 2014 (iliyorekebishwa) kinataka uthaminishaji ufanyike kwa kila mali iliyowekwa kama dhamana ya mkopo. Hakuna ushahidi unaoonesha kuwa uthamini ulifanyika kwa dhamana zilizowekwa kwa mikopo yenye jumla ya Shilingi milioni 330 iliyotolewa kwa wateja wanne (4).

iv. Mikopo ya shilingi milioni 355 imetolewa kwa wateja sita (6) ambao leseni zao zimemalizika muda wake wa matumizi.

v. Mikopo ya waajiriwa (salary loans) ya shilingi milioni 134 imetolewa kwa waajiriwa watano (5) bila kuwa na uthibitisho wa udhamini (guarantee) kutoka kwa waajiri wao kinyume na matakwa ya kifungu cha 8.9.7 cha Sera ya Mikopo ya TWB ya mwaka 2014 (illiyorekebishwa). Pia, imebainika kuwa katika wateja waliokopeshwa, wanne (4) kati yao ni wafanyakazi wa benki za NMB, NBC na Barclays Tanzania.

Mapungufu katika nyaraka yanaweza kusababisha benki ikashindwa kurejeshewa fedha zilizokopeshwa. Pia, inawezekana kuna viashiria vya rushwa katika utoaji wa mikopo kwa kuwa ni vigumu sana kwa wafanyakazi wa benki moja kuchukua mkopo kutoka benki nyingine bila uthibitisho wa udhamini kutoka kwa waajiri wao.

Menejimenti ya TWB inashauriwa kuboresha udhibiti katika utoaji mikopo kwa kuhakikisha hatua zote muhimu na nyaraka

zinafanyika kabla ya uidhinishaji. Pia, tahadhari zaidi zinahitajika kuchukuliwa dhidi ya mikopo iliyotolewa kwa waajiriwa wa benki ili kuhakikisha, pamoja na mambo mengine, kama kweli walikuwa wakifanya kazi na benki hizo na uthibitisho wa udhamini utolewe na waajiri wao.

4.2.2 Kutokidhi Matakwa ya Kiwango cha Chini cha Mtaji

Kanuni namba 5 ya Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha (Utoshelevu wa Mtaji – Capital Adequacy) inaitaka benki au taasisi ya fedha zenye ukomo wa maeneo ya kutoa huduma (with limited scope of services) kuanza kutoa huduma na kuhakikisha wakati wote zina kiasi cha chini cha mtaji kisichopungua shilingi bilioni 5. Imebainika kuwa mtaji wa benki katika mwisho wa miezi ya Januari, Februari, Septemba, Oktoba, Novemba na Desemba 2015 ulienda chini ya kiwango cha chini cha shilingi bilioni 5.

Kanuni namba 9 ya Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha (Utoshelevu wa Mtaji – Capital Adequacy) inaitaka benki au taasisi ya fedha, wakati wote kudumisha kiasi cha chini cha mtaji wa msingi (core capital) usiopungua asilimia kumi na mbili na nusu ya jumla ya mali zinazoambatana na vihatarishi na mali zilizo katika hali hatarishi zilizo nje ya urari wa kimahesabu (off-balance sheet exposure) na mtaji wa jumla usiopungua asilimia kumi na nne na nusu ya jumla ya mali zinazoambatana na vihatarishi na mali zilizo katika hali hatarishi zilizo nje ya uhalali wa kimahesabu (off-balance sheet exposure).

Hata hivyo, kwa mwezi wa Desemba 2015, utoshelevu wa mtaji wa msingi na mtaji wa jumla (total capital) wa benki ulikuwa asilimia 12 ambayo ni chini ya kiwango cha chini cha mahitaji ya mtaji.

Kushindwa kwa benki kuzingatia kanuni zilizowekwa kunaweza kuisababishia benki adhabu ikiwa ni pamoja na kupokonywa leseni.

Menejimenti ya TWB inashauriwa kuhakikisha inafuata matakwa ya kiwango cha chini cha mtaji kwa kufuatilia mwenendo wa mtaji (monitoring capital position) kila siku na kuchukua hatua thabiti kudumisha kiwango cha chini cha mtaji.

4.3 Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)

4.3.1 Bidhaa zenye Thamani ya Shilingi Milioni 450.57 Hazijawasilishwa Hospitali na Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

Mapitio ya ankara kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) yameonesha kuna ankara 48 za tangu mwaka 2010 zikiwa na jumla ya Shilingi bilioni 2.29. Hospitali ya Muhimbili walilipa kiasi chote cha fedha. Hata hivyo, imebainika kuwa bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.84 ndizo zimefika na kupokelewa na Hospitali ya Taifa Muhimbili mpaka kufikia Juni 2016, na kuacha bidhaa zenye thamani ya Shilingi milioni 450.57 zikiwa hazijafikishwa Muhimbili. Kutokufika kwa muda kwa vifaa vya matibabu kunasababisha usumbufu kwa hospitali katika utoaji wa huduma ya tiba.

Menejimenti inashauriwa kuchunguza suala husika na kufanya usuluhishi wa taarifa na MSD na kufanya ufuatiliaji wa bidhaa ambazo hazijaletwa.

4.4 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

4.4.1 Miradi isiyokamilika kwa muda mrefu - Utoaji wa Huduma ya Mawasiliano Vijijini

UCSAF imewezesha kifedha miradi 443 iliyopo katika mikoa yote ya Tanzania bara. Miradi hiyo inafanywa na watoa huduma ya mawasiliano kama TTCL, Airtel, MIC (Tigo), Vodacom na Zantel.

Kukamilika kwa miradi yote kumechukua muda mrefu sana, ambapo, kati ya miradi 443 ni miradi 217 tu (sawa na asilimia 49) imekamilika mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka 2015/16 ikiacha miradi 226 ambayo bado haijakamilika. Mingi kati ya miradi ambayo haijakamilika ni ile inayofanywa na kampuni za Vodacom na TTCL.

Juhudi za ufuatiliaji wa miradi ambayo haijakamilika inatakiwa kuongezwa kuhakikisha hakuna ucheleweshaji zaidi na kushughulikia tatizo la ucheleweshaji kwa mujibu wa masharti ya mkataba.

4.5 Shirika la Posta Tanzania (TPC) - 2014/15

4.5.1 Kudorora kwa Mwenendo wa Biashara wa Shirika la Posta Tanzania

Mapitio ya Shirika la Posta Tanzania (TPC) yamebaini kuwa shirika linakumbana na changamoto za aina mbalimbali ikiwemo ukosefu wa fedha kwa ajili ya shughuli za utendaji na madeni ya muda mrefu,kwa mfano deni la shilingi bilioni 3.87 linaloidai Serikali kuhusiana na malipo ya pensheni kwa wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) iliyovunjika. Kukosekana kwa mapitio, mipango ya kimkakati na ya biashara, pamoja na miundombinu duni ya huduma ya posta (kama vile kukosekana kwa mifumo ya kielektroniki ya mipango ya rasilimali (ERP)) ni mambo ambayo yamesababisha biashara kudorora.

Biashara ya Shirika la Posta itaendelea kuanguka kama mageuzi hayatafanyika kushughulikia changamoto zinazolikabili shirika.

Shirika la Posta linahitaji mapinduzi makubwa ya kimkakati likilenga watu, michakato, teknolojia, na fedha. Pia, Serikali inatakiwa kulirejeshea Shirika kiasi cha Shilingi bilioni 3.87 kilichotumika kuwalipa wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

4.5.2 Kushindwa Kulipa Ada na Mirabaha Shilingi bilioni 1.38

Shirika la Posta Tanzania (TPC) lilishindwa kulipa kiasi cha Shilingi bilioni 1.38 kwa Mamlaka ya Udhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA) ikiwa ni mjumuisho wa madeni ya ada ya mwaka na mirabaha kwa mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na miaka iliyopita. Katika mwaka wa Fedha 2015/2016 kiasi cha Shilingi milioni 286.8 hakikulipwa kama fedha ya mrabaha na Shilingi milioni 9 kama fedha ya ada ya mwaka, kiasi cha Shilingi bilioni 1.08 kinawakilisha madeni ya miaka iliyopita. Hii ni kinyume na kifungu cha 157 cha sheria ya mawasiliano ya kielektroniki na posta ya mwaka 2010 na Kanuni ya 28(1) mpaka (3) ya Mawasiliano ya kielektroniki na posta ya mwaka 2011 ambavyo vinahitaji shirika la Posta Tanzania kuhakikisha linalipa mrabaha na ada kila mwaka kwa Mamlaka ya Udhibiti Maasliliano Tanzania (TCRA).

Iwapo Shirika la Posta Tanzania litashindwa kuzingatia sheria na kanuni kwa kulipa mirabaha na ada kama inavyotakiwa, TCRA inaweza kuwapa adhabu au kusimamisha leseni ya biashara. Hivyo basi menejimenti inashauriwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zote na kuhakikisha kwamba deni lote linalipwa kwa Mamlaka(TCRA).

4.6 Benki ya Twinga (TBCL)

4.6.1 Tatizo la Uendelevu wa Benki ya Twiga

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2014, benki ya Twiga ilipata hasara ya shilingi bilioni 13.08. Pia kwa mwaka wa fedha ulioishia 31 Desemba 2015, benki ya Twiga ilipata hasara ya Shilingi bilioni 3.4. Aidha, katika mwaka ulioishia 31 Desemba 2014, benki ilikuwa na upungufu wa mali ya wana hisa (Equity) shilingi bilioni 20.62. Pia katika mwaka unaoishia 31 Desemba 2015, benki ilikuwa na upungufu wa mtaji kwa wana hisa wenye thamani ya Shilingi bilioni 18.7. Hali hii inaleta mashaka juu ya uwezo wa benki hii kuendelea kujiendesha bila mashaka. Aidha, mtaji wa msingi wa benki katika miaka miwili ni chini ya kiwango cha chini (kidogo) kinachohitajika cha thamani ya shilingi bilioni 5 kama kinavyosomeka kwenye kifungu cha 17 cha sheria ya benki na taasisi za fedha. Pia, sheria hii inahitaji benki kuhakikisha kwamba, nyakati zote inakuwa na mtaji wa msingi usiopungua asilimia 10 na mtaji wa jumla usiopungua asilmia 12.

Naishauri menejimenti ya benki kufanya uchunguzi na kuanisha sababu zilizopelekea benki kufanya vibaya. Pia, kubuni mikakati itakayo saidia kuleta kuokoa utendaji wa benki.

4.7 Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)

4.7.1 Kuchelewa kwa Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kujenga Nyumba za Walimu

Mamlaka ya Elimu Tanzania ilipanga kujenga nyumba 53 za walimu katika sehemu mbalimbali zisizofikika kwa urahisi, ambapo, bajeti ya Shilingi bilioni 7.5 ilitengwa. Mradi huo ulitarajiwa kukamilika tarehe 30 Juni 2016. Hata hivyo, mamlaka ilifanikiwa kujenga nyumba 15 kwa kuchelwa (ujenzi huo ulianza Agosti 2016 mpaka Desemba 2016). Kuchelewa kwa mradi huu kulisababishwa na serikali kuchelewesha kuwasilisha fungu la

pesa zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu na mchakato wa kuwatafuta wazabuni wa ujenzi wa nyumba hizo.

Serikali inashauriwa kuweka fungu la kutosha katika muda sahihi kwa mamlaka ili kukamilisha miradi yake na kuondoa tatizo la makazi ya kutosha kwa walimu.

4.8 Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA)

4.8.1 Kucheleweshwa kwa Miradi ya Maendeleo

TANAPA ilishindwa kukamilisha miradi minane ya maendeleo kama ilivyoainishwa kwenye mikataba yenye gharama ya shilingi milioni 756.89.

Ilibainika kwamba utekelezaji wa miradi hiyo ulisimamishwa kutokana na migogoro ya ardhi pamoja na mkandarasi kutotimiza wajibu wake kama ilivyooneshwa kwenye mkataba. Kuchelewa kukamilika kwa miradi ya maendeleo kunaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama za ziada kufikia ukamilishaji miradi hii.

Menejimenti inashauriwa kuhakikisha kwamba matatizo yote yanayozuia utekelezaji wa miradi yanatatuliwa ili kuhakikisha miradi inakakamilika ndani ya muda.

4.8.2 Uwezekano wa kupoteza Mapato Kwenye Mikataba ya Upangishaji

Hoteli, nyumba za kupangisha, na kambi za kulala watalii wanapaswa kuilipa Mamlaka tozo kwa ajili ya kuendesha biashara ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya TANAPA. Kuna njia mbili

za kutoza tozo hizo, yaani, asilimia 10 ya mapato yanayopatikana kwa kila mteja kwa siku au kiwango maalumu kilichokubalika. Ukaguzi ulibaini kuwa, taarifa za wateja wanaolala kwenye hifadhi zinahifadhiwa na kutolewa na wamiliki wa hoteli, nyumba za kupangisha kambi zilizopo. Mamlaka haina utaratibu wa kuhakiki usahihi wa taarifa husika wanazopata kutoka kwa wamiliki wa sehemu hizo za malazi. Hii inapelekea Mamlaka kutegemea zaidi na kutumia taarifa kutoka kwa wamiliki wa hoteli hizo. Hali hii inaashiria kupotea kwa mapato ya Mamlaka kutokana na Menejimenti ya Hifadhi kutokuwa na uwezo wa kuhakiki usahihi na ukamilifu wa taarifa kutoka kwa wamiliki wa hoteli hizo.

Menejimenti ya Mamalaka inashauriwa kuwa na chombo cha kuiwezesha kuhakiki usahihi na ukamilifu wa taarifa za wageni kama zinavyotolewa na wamiliki wa hoteli hizo. Pia, kuwe na kiwango maalumu cha tozo hizo ili kuondokana na udanganyifu unaoweza kufanywa na wamiliki wa mahoteli na mabanda ya kulaza watalii.

4.8.3 Wizara Kushindwa Kulipa Deni la Pango Shilingi 2.4 bilioni

Wizara ya mambo ya nje imepangisha moja ya majengo ya TANAPA katika mkoa wa Arusha na kutumia jengo hilo kama ofisi yake. Hata hivyo, Wizara imeshindwa kulipa kodi ya jengo hilo kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja, ambapo mpaka tarehe 31 June 2016 Hifadhi ya TANAPA inadai kiasi cha Shilingi bilioni 2.4.

Menejimenti ya TANAPA inashauriwa kuweka juhudi zaidi na kufuatilia ili kuhakikisha Wizara inalipa ada ya pango inayodaiwa kama inavyoelezwa kwenye makubaliano.

4.9 Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA)

4.9.1 Uendelevu wa Hifadhi ya Ngorongoro

Hifadhi ya Ngorongoro ilianzishwa ikiwa na malengo mengi, yakiwemo kuendeleza na kuhifadhi maliasili iliyopo katika Hifadhi, kulinda maslahi ya wakazi wa asili wa NCAA na kukuza utalii. Hifadhi hii ilipoanzishwa, Mamlaka ilikuwa na idadi ya wakazi asili wasiozidi 20,000 wakiwa na mifugo yao, kadhalika, hapakuwa na nyumba za kudumu.

Sensa ya makazi ya mwaka 2012 ilionesha kwamba Hifadhi ya Ngorongoro ina jumla ya wanakijiji wanaofikia 80,000 ambao wanategemea kuongezeka kwa asilimia 4 kila mwaka. Kuna makazi ya kudumu yaliyoandikishwa yenye nyumba za kisasa na vijiji vingine vinachukuliwa kama miji. Mnamo mwaka 1976, kata ya Ngorongoro ilikuwa na vijiji vine (4). Hadi kufikia Aprili 2016, kulikuwa na vijiji 36 vilivyounda kata 13. Makazi haya yanahitaji miundombinu na huduma zote za kijamii kama vile shule na vituo vya afya. Hata hivyo, hakuna vigezo vilivyowekwa ili mtu kuweza kujiunga na jamii ya ufugaji. Hali hii inahamasisha watu wengi kuhamia katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Kutokana na hali hii, NCAA inaweza kupokea watu wengi zaidi na hatimaye kuweza kusababisha migogoro mingi ya ardhi. Pia, kuweka ugumu wa jinsi ya kufanya shughuli za kuhifadhi maliasili iliyopo katika Hifadhi, kulinda maslahi ya wakazi wa asili na kukuza utalii.

Menejimenti ya NCCA inashauriwa kuwa na mpango wa matumizi ya ardhi. Pia, kuhakikisha hatua za kuzuia makazi ya binadamu na maendeleo katika eneo la hifadhi ya Ngorongoro.

4.9.2 Matatizo ya Wanafunzi Waliofadhiliwa na Hifadhi

Baraza la wafugaji la Ngorongoro (NPC) hufadhili wanafunzi wa jumuiya ya wafugaji masikini. Hata hivyo, katika ufadhili huu kaguzi ilibaini yafuatayo: -

a) Kulikuwa hakuna ushahidi unaoonesha kwamba kamati ya maendeleo, elimu na utendaji zilijadili majina ya wanafunzi kutoka kwenye jamii masikini ya wafugaji kabla ya kupitishwa na kamati ya wafugaji (NPC) kama inavyohitajika na aya ya 1.9 ya Muongozo wa Kudhamini Wanafunzi. Bajeti ya baraza ya mwaka 2015/2016 imetoa orodha ya majina ya wanafunzi waliodhaminiwa na baraza katika shule na vyuo mbalimbali, lakini hakuna ushahidi wowote wa jinsi majina hayo yalivyopatikana.

b) Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, wanafunzi 1,036 walidhaminiwa na NPC, ambapo, kiasi cha Shilingi milioni 846 kililipwa na Baraza kwa ajili ya shule za msingi, sekondari, VETA, vyuo vya kati na vyuo vikuu bila kusaini mkataba kama inavyohitajika kwenye muongozo.

c) Kulikuwa hakuna nyaraka sahihi zilizowekwa na Baraza kama hifadhi za msingi (data base) kwa ajili wanafunzi wote waliodhaminiwa na wanaoendela kudhaminiwa na Baraza mpaka sasa. Kwa mfano, orodha ya wanafunzi iliyotolewa na bajeti ya Baraza haikufanana na sampuli ya shule/vyuo vilivyotembelewa katika kipindi cha ukaguzi. Kwa mujibu wa kumbukumbu za bajeti ya Baraza, idadi ya wanafunzi watano walidhaminiwa na Baraza la AIA 5, LITA Tengeru ni 20, na Shule ya Sekondari Embarway ni 194, wakati namba halisi kwa AIA ni 10, LITA Tengeru ni 3 na Shule ya Sekondari Embarway ni 152.

Kutokuzingatia muongozo wa udhamini, kunanyima haki kwa wanafunzi wenye kuhitaji msaada. Kutokuwepo kwa utaratibu maalum wa kutunza kumbukumbu (kanzi data) za wanafunzi wote waliodhaminiwa na Baraza kunaweza sababisha ulipwaji hewa wa ada.

Menejimenti za Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Baraza la Wafugaji (NPC) zinanatakiwa kuhakikisha kanuni na miongozo yakudhamini wanafunzi inafuatwa. Pia, taarifa za wanafunzi waliodhaminiwa zinahifadhiwa na taarifa zinaboreshwa kuonesha uhalisia.

4.10 Ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa wa Arusha (AICC)

4.10.1 Hasara Iliyopatikana Kufuatia Ukiukaji wa Mkataba na Mfuko wa Pensheni wa LAPF Shilingi Milioni 473.76

Ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa wa Arusha (AICC) unamiliki hekta 3.8 za ardhi iliyosajiliwa namba ya kiwanja 24 katika kitalu namba Z kilichopo Kaloleni mkoani Arusha, ambapo, kulikuwa kina jumla ya nyumba 72 zilizojengwa.

Mnamo mwaka 2012, nyumba hizi zilibomolewa ili kupisha ujengaji wa duka la kisasa lililokuwa na makadirio ya gharama ya awali ya shilingi bilioni 40.5. Kutokana na mkataba uliosainiwa tarehe 6 Disemba 2012, duka hilo la kisasa lilikuwa lijengwe na AICC katika makubaliano ya ubia na Mfuko wa Pensheni wa LAPF. Ripoti ya uthaminishaji iliyotolewa na kampuni ya Africa Property Limited mnamo Februari 2012 ilionesha kuwa thamani ya soko ya nyumba zilizobomolewa ilikuwa shilingi bilioni 1.85.

Hata hivyo, mpaka kufikia Januari 2017, kiwanja hicho kilikuwa hakijaendelezwa kufuatia kusimamishwa kwa mradi na Mfuko wa Pensheni wa LAPF waliojitoa kwenye makubaliano yaliyoingiwa mnamo tarehe 16 Julai 2014 kupitia barua yenye kumbukumbu namba LAPF/A.26/01/30.Barua hiyo ilidai kwamba Mfuko wa Pensheni LAPF ulikuwa umeifikia kiwango cha juu cha uwekezaji.

Kufuatia kubomolewa kwa mali, AICC inapoteza shilingi milioni 473 kila mwaka, kiasi ambacho kingekuwa kinakusanywa kutoka kwenye nyumba 72.

Menejimenti ya AICC inashauriwa kutafuta msaada wa kifedha kutoka kwenye vyanzo mbalimbali kutekeleza mradi huo. Pia, inashauriwa kukaa na LAPF na kuna jinsi gani ya kurudisha hasara iliyotokea.

4.10.2 Mapato Yaliyopotea kwenye Mali za Uwekezaji ya Shilingi Bilioni 1.53

Katika mapitio na kufanya tathmini ya matumizi na hali ya kazi ya jengo linalomiliiwa na AICC, ilibainika kuwa mali nyingi zipo wazi, hivyo, hazijatumika kwa zaidi ya mwaka mmoja. Ngorongoro, Serengeti na Kilimanjaro yana nafasi za wazi za mita za mraba 7,507 ambazo zingeweza kuzalisha shilingi bilioni 1.153 kila mwaka. Pamoja na hayo, kulikuwa na nyumba mbili za makazi karibu na barabara ya zimamoto zilizokuwa wazi. Tathmini ilionesha kwamba nyumba hizo zingeweza kuzalisha mapato ya Shilingi milioni 15.6 kila mwaka kama zingepangishwa. Kuongezeka kwa nafasi za wazi za ofisi kunasababishwa na mmoja wa mpangaji muhimu, Utaratibu wa Mahakama za Kimataifa za Uhalifu (MICT), [zamani Mahakama ya Kimataifa ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda (ICTR)], ambayo ilikuwa inachukuwa ukubwa wa mita za mraba 11,106 na kupungua mpaka mita za mraba 3,269.

Menejimenti inatakiwa kuanzisha kampeni kabambe kutafutia soko sehemu za ofisi zilizopo wazi kwa kukodishwa.

4.10.3 Majengo Yenye Mmiliki Zaidi ya Mmoja

Shughuli ya uhakiki wa mali ilibainisha kuwa, moja ya mali ilihamishwa kwenda AICC mnamo tarehe 15 Aprili 1983 kama ilivyo kwenye tangazo la serikali namba 51 ambalo kwa sasa

linatumika na Chuo cha Uongozi cha Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAMI). Japokuwa jingo hilo lilihamishiwa AICC, lakini chuo hicho cha ESAMI kina hati miliki ya kisheia na ipo chini ya umiliki wake. Hii ilitokana na kutokuwepo kwa utaratibu wa wazi wa kuhamisha umiliki kutoka kwa Serikali.

Menejimenti inatakiwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu juu ya jambo hili na kusuluhisha umiliki wa kiwanja na jingo husika.

4.11 Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA)

4.11.1 Ukosefu wa Maendeleo ya Utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya ADS-B

Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) iliingia mkataba na kampuni ya COMSOFT GMBH kwa ajili ya kufunga mifumo na mitambo ya kuongoza yenye thamani ya sarafu ya ulaya milioni 1.58 sawa na Shilingi bilioni 3.4 mnamo mwaka 2013.

Katika mapitio ya mkataba huo na utekelezaji wake, iligundulika kwamba kumekuwa hakuna maendeleo yoyote kwenye kutekeleza mradi wa awamu ya kwanza ya Mfumo wa udhibiti wa Anga (ADS-B) ulioanza Mei 2013. Utekelezaji huu umesimama tangu kipindi cha 2014/2015 kutokana na ukosefu wa vitu muhimu vya kuongozea na ili kusaidia mradi huo kufanya kazi, aidha imebainika pia mzabuni, COMSOFT GMBH ametangaza kufilisika.

Uchunguzi zaidi uligundua kuwa mzabuni alikuwa hajawasilisha dhamana ya utendaji, hivyo, kuwa ngumu kwa Mamlaka kuokoa fedha ambazo zimeshalipwa.

Kutokufuata kwa mpango wa kurekebisha hatua za kurekebisha zilizopo kwenye mpango (Correction action plan) walizokubaliana na ICAO na ushauri wa kikaguzi wa ICAO kunaweza kuhatarisha usalama wa Anga.

Menejimenti inashauriwa kufanya tathmini ya changamoto za utekelezaji wa mradi na kuchukua hatua sahihi ili kuboresha shughuli za udhibiti wa anga.

4.11.2 Kasi Ndogo ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Usalama na ICAO

Ukaguzi wa kina wa mfumo ulifanyika hapa Tanzania na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO) mnamo Mei 2013. Matokeo ya ukaguzi yalionesha kuwa Mamlaka ilipata asilimia 38 ya alama chini ya wastani wa viwango vya kimataifa ambavyo vinahitaji angalau asimilia 60 kwenye Utekelezaji Madhubuti (EI) wa uangalizi wa mfumo wa usalama wa nchi kwa ajili ya mambo manane muhimu ya (CEs) hali ya mfumo wa usafiri wa anga ya nchi. Iligundulika pia kuwa, kati ya matokeo 529 ya utafiti na maswali ya itifaki kuhusu Utekelezaji Madhubuti (EI), Mamlaka ilimaliza na kushughulikia 226 tu (asilimia 42.72) na kuacha 303 (asilimia 57.28) hayajashugulikiwa.

Ni maoni yetu kwamba kutofuatwa kwa Mpango Sahihi wa Utekelezaji (CAP) iliyokubaliana na ICAO and mapendekezo yake ya ukaguzi, kunaweza kuhatarisha usalama wa anga.

Mamlaka inashauriwa kumalizia utekelizaji wa Mipango Sahihi wa Utekelezaji (CAPs) kama ilivyopendekezwa kutoka kwenye ukaguzi ICAO na kuweka ushahidi unaohitajika ili kudumisha

wastani wa kimataifa kwa ajili Utekelezaji Madhubuti wa asilimia 60.

4.12 Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP)

4.12.1 Uwezo mdogo (asilimia 6) wa kukidhi malazi ya wanafunzi wote

Katika mwaka wa fedha 2015/16 Chuo kilikuwa na jumla ya wanafunzi 5,347, ambapo 2,755 ni wanawake na 2,592 ni wanaume katika kampasi zake zote ambazo ni Dodoma na Mwanza. Ukaguzi ulibainisha kuwa Chuo kilikuwa na hosteli moja tu iliyopo katika kampasi yake ya mjini Dodoma iliyokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 312 kati ya wanafunzi 3,945 waliokuwa wamesajiliwa. Uwezo huu wa malazi ni sawa na asilimia 7.9 tu. Katika kampasi ya Mwanza, kulikuwa na wanafunzi 1,402 ijapokuwa hakuna hosteli yoyote ile ambayo ni sawa na asilimia 0 ya uwezo wa malazi.

Kwa asilimia ya uwezo wa malazi iliyopo, ufaulu wa wanafunzi unaweza kuathirika.Aidha linaweza kuwa tatizo kubwa zaidi kwa wanafunzi wa kike kutokana na kuwepo kwa uwezekano mkubwa wa kukumbana na unyanyasaji wa kijinsia.

Menejimenti inashauriwa kuweka mpango wa kujenga hosteli za chuo ambazo zinaweza kukidhi angalau asilimia 80 ya wanafunzi wote chuoni ilikuongeza ufaulu kwa wanafunzi na kuondooa hatari kwa wanafunzi wa kike.

4.13 Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)

4.13.1 Kiwango cha Juu Sana cha Utoro cha Asilimia 81.76

Kupitia mkutano wa 107 wa Uongozi wa Bodi, Menejimenti ya chuo cha CBE iliagizwa kuchunguza sababu za wanafunzi kufeli

kwenye masomo yao kama matokeo ya muhula wa kwanza yalivyobainisha katika mwaka wa masomo 2015/16. Wanafunzi 1,089 tu kati ya 5009 walifanikiwa kufaulu kwenye mitihani ya Muhula wa kwanza, sawa na asilimia 21.7.

Menejimenti ilitanabaisha kuwa utoro wa walimu na wanafunzi kama chanzo kikubwa cha kufeli kwa wanafunzi. Hivyo menejimenti ilipendekeza kuanzishwa kwa jalada la mahudhurio ili kufuatilia walimu na wanafunzi wanapoingia na kutoka katika vipindi vya masomo. Tathmini ya mahudhurio, hata hivyo, imebaini kuwapo kwa utoro wa asilimia 81.76 katika mwaka wa fedha 2015/2016.Kiwango cha chini kilikuwa asilimia 30.56.

Utoro unaathiri utendaji wa kitaaluma wa wanafunzi pamoja na hadhi na ubora wa chuo. Hali hii itaathiri utendaji na mapato kwa Chuo. Pia itasababisha wateja watarajiwa na wadau kuchagua vyuo mbadala kwa misingi ya kushuka kwa hadhi ya chuo.

Menejimenti inashauriwa kuchukua hatua kali na za haraka katika kutatua tatizo la utoro. Kiwango cha utoro kilichobainishwa kinaashiria ukosefu wa dhamira kwa menejimenti ya chuo katika kudhibiti masuala yanayoathiri chuo.

4.14 Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)

4.14.1 Kodi ya Zuio Haikutozwa Shilingi Bilioni 1.36

Kifungu kidogo Na. 1 cha Kifungu Na. 83 cha Kodi ya Mapato 2008 kinahitaji mlipaji kutoza kodi ya zuio inayotokana na ada zote za huduma na malipo ya mkataba. Hata hivyo, tumebaini kuwa TANESCO halikuzuia kodi ya zuio yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.36.

Kwa kutotoza kodi ya zuio, si tu kunaipotezea serikali mapato, bali kunaweza kusababisha adhabu na riba ambayo inaweza, kwa kiasi kikubwa, kuongeza gharama zisizo za lazima kwa Kampuni.

Menejimenti inakumbushwa kuzuia kodi ya zuio inayotokana na ada za huduma na malipo ya mkataba.Aidha, kuwasilisha TRA kuepuka matokeo ya baadaye yahusianayo na kutofuata kanuni na sheria za kodi.

4.14.2 Limbikizo la Madeni ya Wateja ya Thamani ya Shilingi Bilioni 24 Kutoondolewa

TANESCO limekuwa likihamisha data za akaunti za wateja wake kutoka mita za kawaida za zamani kwenda mita mpya za LUKU. Ukaguzi ulibani kwamba, limbikizo la wateja wengi wenye deni la jumla la shilingi bilioni 24 halijalipwa na hakuna dalili kwamba deni hilo litalipwa.

Hali hii inaikosesha kampuni mapato. Pia inaweza kuathiri shughuli zake. Hali kadhalika, inaweza kuashiria kuwapo kwa mianya ya rushwa baina ya wateja na wafanyakazi wa TANESCO ambayo inapelekea wateja kuunganishiwa tena umeme bila kulipa bili zao.

Menejimenti inashauriwa kuchukua hatua muhimu ambazo zipo ndani ya uwezo wake kuhakikisha fedha zinakusanywa.

SURA YA TANO

MAPITIO YA MIKAKATI NA UENDESHAJI WA KIUFANISI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

5.0 Utangulizi

Usimamizi wa kimkakati unajumuisha mipango endelevu, ufuatiliaji, uchambuzi, na tathmini ya shughuli zote muhimu kwa ajili ya shirika kuweza kufikia malengo na madhumuni yake. Usimamizi wa kimkakati unahusisha kuchambua uwezo na udhaifu wa ndani na nje; kutengeneza mipango na tathmini ya utekelezaji wake, pamoja na kutathmini mafanikio na kufanya mabadiliko ili kufikia malengo.

Katika muktadha wa kibiashara, ufanisi katika uendeshaji ni uwiano kati ya mtaji uliowekwa katika kuendesha biashara na mapato yatokanayo na biashara. Ufanisi katika uendeshaji unajumuisha mikakati kadhaa iliyotumika ili kutimiza lengo la msingi la kutoa bidhaa zenye ubora au huduma kwa wateja katika gharama nafuu na kwa wakati muafaka. Pia, inahusisha upatikanaji wa thamani zaidi kutoka kwenye rasilimali au uendeshaji wa taasisi kwa lengo la kuongeza tija.

Tathmini yangu ya mikakati na ufanisi katika uendeshaji inajumuisha mashirika 11 ya umma ambayo ni:

(i) Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO);
(ii) Shirika la taifa la hifadhi ya jamii (NSSF);
(iii) Mamlaka ya Ukanda wa Uwekezaji Tanzania (EPZA);
(iv) Mfuko wa Pensheni (LAPF);
(v) Mfuko wa Pensheni (PPF);
(vi) Mfuko wa Pensheni wa Sekta ya Umma (PSPF);
(vii) Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA);

(viii) Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda (TIRDO);
(ix) Chuo kikuu dar es salaam (UDSM);
(x) Chuo cha Ufundi Stadi Tanzania (VETA); na
(xi) Shirika la Bandari Tanzania (TPA).

5.1 Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

5.1.1 Usimamizi wa Kampuni Binafsi za Uzalishaji Umeme na Gharama Zake

Katika jitihada za kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa uhakika wa umeme nchini, Shirika limeingia mikataba na makampuni matano binafsi yanayozalisha umeme.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Shirika linanunua umeme kwa bei ya wastani wa Shilingi 544.65 kwa kila uniti na kuuza kwa Shilingi 279.35. Hivyo, kwa kila uniti moja, shirika linapata hasara ya Shilingi 265.3 kama inavyooneshwa kwenye jedwali Na. 2 hapa chini:

Jedwali Na. 1: gharama za uzalishaji za makampuni binafsi ya kuzalisha umeme

Kampuni	Aina ya Mafuta	Uwezo MW	Mtambo (%)	Bei ya Umeme (US$/kWh)	Gharama za uzalishaji (US$/Mon)
EPP's					
Aggreko	Petroli	100	75	0.38	1,806,255
Symbion 112	Mafuta ya ndege	112	75	0.38	2,827,283
Symbion DOM & Arusha	Petroli	105	75	0.39	3,779,213
IPP's					
Songas-Gas	Gesi asilia	189	92	0.03	5,266,169
IPTL (Interim)	Mafuta mazito	100	75	0.23	2,678,233

Chanzo: TANESCO

Kabla ya kusitishwa kwa mkataba na Symbion, Shirika lilikuwa linalipa jumla ya Dola z a Marekani milioni 16.36 kama gharama za umeme (capacity charges) kwa makampuni matatu yanayozalisha umeme wa dharura na mawili ya binafsi kama inavyonekana kwenye jedwali hapo juu. Kwa sasa, Shirika linatumia Dola za Marekani milioni 9.75 kwa mwezi kununua umeme kutoka Aggreko, Songas na IPTL gharama za umeme zinazolipwa na TANESCO kwa mwezi ni Dola za Marekani milioni 9.75.

Ili kuliwezesha Shirika nashauri:

i. Bei za umeme zinazopitishwa na EWURA zizingatie gharama halisi zinazotumiwa na TANESCO kuzalisha umeme au kununua toka kwa makampuni binafsi ya uzalishaji umeme. Vile vile, bei itayopitishwa izingatie gharama za uendeshaji wa shirika na uwezo wa kufanya uwekezaji kwenye miundombinu ili huduma ya umeme iendelee kuwa ya uhakika.

ii. Manunuzi ya umeme toka kwenye makapuni binafsi ya uzalishaji umeme yafanywe kwa uwazi na ushindani kama ianvyotakiwa na sheria ya manunuzi ili kuwezesha TANESCO kupata bei nafuu.

iii. Serikali iiwezeshe TANESCO fedha ili iweze kuwekeza kwenye uzalishaji umeme wa bei nafuu hivyo kusaidia kuepukana na utaratibu wa kununua toka vyanzo vya gharama kubwa.

5.1.2 Kuchelewa kuendeleza miradi yakuzalisha umeme kwa njia ya maji

a) Ujenzi wa mradi wa maji wa kuzalishia umeme katika korongo la Stiegler (Selous)

Mradi wa korongo la Stiegler ulikuwa katika mpango mkakati wa maendeleo ya sekta ya umeme wa mwaka 2012. Kabla ya kuingizwa kwenye mpango mkakati, kampuni ya ujenzi ya M/s. Oderbecht kutoka Brazil illifanya upembuzi yakinifu wa mradi Agosti 2011 na kuja na mapendekezo yafutayo:

i. Mradi una manufaa zaidi kiuchumi ukilinganisha na mingine.

ii. Mradi upo katika mbuga ya Selous ambayo iko chini ya maeneo tengefu ya urithi wa dunia chini ya uangalizi wa UNESCO hivyo ruhusa maalumu inatakiwa ipatikane kabla ya kuendeleza mradi huu mbugani.

iii. Gharama kamili ya kujenga mradi ni Dola ya Marekani bilioni 2.4.

Nimebaini kuwa RUBADA walisaini Memoranda ya Makubaliano na kampuni ya Oderbecht tarehe 9 Julai 2012. Hata hivyo, mpaka sasa kilichofanyika pekee ni tathmini ya eneo la mradi. Tathmini zingine kama madhara ya mradi kwenye mazingira na jamii bado hazijafanyika. Nyongeza ya mamemoranda ya makubaliano kwa miaka mitatu zaidi ilisainiwa 05 Desemba 2016.

Mapitio ya taarifa mbalimbali yanaonyesha kuwa mradi huu ukikamilika utakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 2,100. Mpango mkakati wa sekta ya umeme wa mwaka 2012 unaonyesha kuwa mradi unatakiwa kujengwa kwa awamu tatu: Stiegler 1 megawati 300 - kukamilika 2024; Stiegler II megawati 600 - kukamilika 2026; na Stiegler III Megawati 300 - kukamilika 2028.

Pia, nimebaini kuwa RUBADA inakabiliwa na changamoto ya kifedha kuweza kuuendeleza mradi. Vilevile kwa kuwa eneo la mradi lipo ndani ya eneo la urithi wa dunia chini ya

uangalizi wa UNESCO, serikali inatakiwa kufanya jitihada za ziada ili kuweza kupata kibali cha kuendeleza mradi huo.

Ninashauri

i. RUBADA ishirikishe Wizara ya Nishati na Madini, TANESCO na wadau stahiki katika hatua zote za uendelezaji mradi.

ii. Serikali iziwezeshe RUBADA/TANESCO kupata vyanzo vya kuaminika vya fedha ili waweze kuwekeza kwenye mradi unaotegemewa kuwa wa bei nafuu zaidi ukilinganishwa na umeme unaotumiwa toka kwa makampuni binafsi ya uzalishaji umeme.

iii. Serikali ifanye jitihada za makusudi na mapema ili kuweza kupata vibali stahiki toka UNESCO ili kuendeleza mradi kwenye eneo tengefu la urithi wa dunia.

5.1.3 Ujenzi wa Mradi wa Kuzalisha Umeme Eneo la Songwe

Mradi wa Bonde la Mto Songwe unahusisha uzalishaji umeme kwa kutumia maji eneo la mpakani mwa Tanzania na Malawi na umepangwa kufanyika kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2017 kwa gharama ya Dola ya Marekani milioni 550. Sambamba na kuzalisha umeme, mradi huu pia una lengo la kudhibiti mafuriko na kutumia maji kama sehemu ya kilimo cha umwagiliaji.

Nilibaini kuwa Shirika halina udhibiti wa moja kwa moja kwenye ujenzi wa mradi huo. Jambo hili linaweza kuchelewesha ukamilishaji wa mradi ambao unamilikiwa kwa ushirikiano kupitia Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe ambayo inahusika na oparesheni za kila siku na usimamizi wa ujenzi wa miundombinu kwa niaba ya Serikali za Tanzania na Malawi.

Kwa sasa nchi za Tanzania na Malawi zinasubiri Serikali zao kuridhia makubaliano ya uanzishwaji wa Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe kwa ajili ya usimamizi wa mradi.

Pia, mradi unakabiliwa na changamoto za kifedha hivyo Kamisheni inatakiwa kuhakikisha inakusanya fedha kutoka kwa wahisani ili kufanikisha ujenzi wa mradi huu. Kwa sasa mradi unakadiriwa kuwa utakamilika kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 829.

Naishauri Serikali kupitisha Makubaliano ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe kuwezesha mradi kufanyika kwa ufanisi. Pia Serikali, ihusishe Shirika kwenye ujenzi wa bwawa na ununuzi wa mitambo ya uzalishaji ili iweze kutoa ushauri wa kitaalamu pindi utakapohitajika.

5.1.4 Uhalisia wa Bei ya Umeme Inayotozwa na TANESCO

Bei za nishati ya umeme inayotozwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) zinadhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) kila robo mwaka baada ya mapitio ya gharama halisi za uzalishaji.

Nilibaini kuwa mapitio ya kila robo mwaka ya bei ya nishati ya umeme hayahusishi madeni yaliyojitokeza kabla ya kuanzishwa kwa utaratibu wa mapitio ya bei ya umeme ya robo mwaka. Hivyo, utaratibu huu hauiwezeshi TANESCO kulipa madeni yote inayodaiwa.

Pia nilibaini kuwa bei ya umeme inayopitishwa na EWURA haionyeshi gharama halisi zilizotumiwa na TANESCO jambo linaloathiri uwezo wa TANESCO katika kulipa madeni yanayolikabili Shirika.

Ninashauri EWURA kupitia kwa umakini gharama za umeme ili kuhakikisha kuwa gharama zote za uzalishaji wa umeme zinahusishwa, ili hatimaye, kusaidia upatikanaji wa faida baada ya uwekezaji wenye lengo la kuboresha huduma na kuongeza matokeo chanya kwa TANESCO.

5.1.5 Mapungufu Katika Ukusanyaji Madeni

Ukaguzi wangu ulibani kwamba, pesa nyingi za TANESCO ni madeni ambayo hayajakusanywa. Mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2016 jumla ya deni la umeme kwa Serikali na taasisi zake zilifika Shilingi bilioni 144.854, sawa na asilimia 67.4 ya deni lote la umeme. Deni lililobaki kwa wateja binafsi ni Shilingi bilioni 70.063 sawa na asilimia 33.

Ni wazi kuwa, kutokulipwa kwa madeni ya umeme na taasisi za umma na binafsi kunaathiri uwezo wa TANESCO kujiendesha kwa ufanisi na kulipa madeni kwa wadai wake.

Nashauri:

i. TANESCO ifanye jitihada madhubuti za kukusanya madeni kwa wateja wake, hasa Serikali na Taasisi za Umma.

ii. Serikali iiwezeshe TANESCO kulipwa madeni yake kwa kutoa maelekezo kwa Taasisi zake kulipa madeni ya umeme kwa wakati.

5.1.6 Wizara ya Nishati na Madini Kutolipa Deni la Kodi ya Pango Shilingi Bilioni 1.12

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa, Wizara ya Nishati na Madini iliingia makubaliano na TANESCO ya kupanga jengo kwa muda wa miaka 10 kwa ajili ya matumizi ya ofisi kwenye jengo la TANESCO lililopo barabara ya Samora, Dar es Salaam.

Muda rasmi wa kuanza makubaliano hayo ilikuwa tarehe 1 Januari, 2013 kwa kodi ya Shilingi milioni 26.60 kwa mwezi. Hata hivyo, Wizara haijalipa kiasi chochote tangu mkataba uliposainiwa, kiasi ambacho hakijalipwa kimefikia Shilingi bilioni 1.12 Jitihada zilizofanywa na menejimenti za kuhakikisha Wizara inalipa deni hilo hazijazaa matunda mpaka sasa.

Kiasi hicho ambacho hakijalipwa kinazidi kudumaza uwezo wa kifedha wa TANESCO na kuongeza ukata wa Kampuni hiyo.

Menejimenti ya TANESCO inashauriwa kuongeza jitihada za kufuatilia Wizarani ili deni hilo lilipwe. Pia, Wizara ya Nishati na Madini ambayo ni Wizara mama ya TANESCO ihakikishe haiwi chanzo cha ukata wa fedha unaoikumba kampuni yake.

5.2 Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)

5.2.1 Kiwango cha Chini cha Ukaliwaji wa Majengo

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) uliwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye majengo na kupangisha kwa wateja kama vile hoteli, kampuni, watu binafsi na nyingine kutumika na Mfuko kama ofisi.. Iligundulika kuwa, kiwango cha ukaliwaji katika majengo tisa (9) ya uwekezaji kilikuwa chini ya kusudio la kiwango cha soko cha asilimia 80 ambapo kiwango cha ukaliwaji wa mali hizo kilikuwa kati ya asilimia 0 mpaka 43. Rasilimali hizi za uwekezaji zinajumuisha Hoteli ya Mwanza, Kigoma, Jengo jipya Biashara la Old Moshi - Arusha, Jengo jipya la Biashara la Kaloleni - Arusha, Kahama (Jengo jipya), Njiro Arusha, Jengo kubwa la kibiashara Kilimanjaro (Kilimanjaro Commercial Complex), Mafao House Ilala na Jengo kubwa la kibiashara Morogoro (Morogoro Commercial Complex).

NSSF ilieleza kwamba, itapunguza uwekezaji katika majengo na kutatua tatizo hilo kwa kuongeza kiwango cha upangishaji. Pia, ofisi za mikoani zimepewa jukumu ya kupangisha wa majengo katika mikoa husika. Kwa hali hii, ni wasiwasi wangu kwamba, thamani ya pesa haitapatikana kutoka kwenye mali hizo za uwekezaji.

NSSF inashauriwa kama ifuatavyo;

i. Kuendelea kutangaza nafasi za kupangisha katika mali hizo za uwekezaji ili kuongeza kiwango cha upangishaji; pia, kupunguza uwekezaji katika majengo.

ii. Kuhakikisha kuwa uwekezaji wowote wa majengo, huhitaji kuhusisha utafiti wa hali ya juu na uchambuzi yakinifu wakati wa kuandaa mipango ya uwekezaji. Lengo likiwa ni kuangalia uwezekano wa majengo haya yanayopangishwa kujaa ili kuhakikisha uwekezaji huu unaleta matokeo chanya..

5.2.2 Usimamizi na Udhibiti Juu ya Mikopo ya Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo

Niligundua kwamba NSSF ilisimamisha kutoa mikopo kwa wanachama wa Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo Mwezi June 2016 ili kuimarisha usimamizi na kuhakikisha kuwa kuna ukusanyaji wa mikopo. Kwa mujibu wa Kanuni za usimamizi wa mikopo, mikopo ilihitajika kupewa kwa Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo ambazo zilikidhi vigezo. Hata hivyo, mikopo iliyotolewa katika kipindi kilichopita kabla ya kusimamisha utoaji wa mikopo, kulikuwa na mapungufu yafuatayo:

i. Mikopo ya Shilingi Bilioni 1 Ilitolewa kwa Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo Zaidi ya Kiwango cha Ukomo

Niligundua NSSF ilitoa Shilingi bilioni 21.3 kwa Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo cha Bunge (National Assembly SACCOS); na Shilingi bilioni 2.2 kwa Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo ya Jumuiya ya Ndugumbi (Ndugumbi Community SACCOS). Utolewaji huu wa mikopo ulizidi kiwango cha ukomo kwa Shilingi bilioni 1. Menejimenti ya NSSF ilieleza kwamba mikopo kwa wanachama wa Bunge ilitolewa kama mpango maalum wa kuvutia wanachama wapya kwenye mfuko.

ii. **Mikopo kutolewa kwenye Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo zaidi ya asilimia 50 ya mali zote**

Niligundua kwamba Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo saba vilipewa mikopo zaidi ya asilimia 50 ya mali zake zote tofauti na kiwango kilichopitishwa. Jedwali la 2 linaonesha mikopo hiyo iliyotolewa:

Jedwali Na. 2: Mikopo juu ya asilimia 50 ya mali zote za Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo

Jina	**Thamani ya Mali zote**	**Asilimia 50 ya mali za Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo 'Million**	**Mkopo uliotolewa 'Million**
Mafanikio Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo	Shilingi milioni 651 mpaka kufikia tarehe 31 Desemba 2013	325.50	490
Masoko Madogo Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo	Shilingi milioni 305 mpaka kufikia tarehe 31 Desemba 2013	152.50	500
Ngima AMCOS Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo	Shilingi milioni 163 mpaka kufikia tarehe 31 Desemba, 2014	81.50	50
UVIKASA TZS	Shilingi milioni 494 mpaka kufikia tarehe 31 Desemba 2014	247	500
VETA Mikumi Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo	Shilingi milioni 83 mpaka kufikia tarehe 31 Desemba 2014	41.50	500
Jumla		**848**	**2,490**

iii. **Kutokuwapo kwa Ushahidi wa Kulipwa kwa Ushuru wa Stempu**

Niligundua kuwa Ushuru wa Stempu ulikuwa haujalipwa kwa vyama vinne vya Ushirika vya Akiba na Mikopo ambavyo vilipewa mikopo.. Hii ni kinyume na matakwa ya Kifungu Namba 42(2) cha Sheria ya Ushuru wa Stempu Sura ya 189 (iliyofanyiwa marekebisho 2006). Vyama hivyo ni Masoko Madogo Madogo chenye Shilingi milioni 500, Chama cha Ngima chenye Shilingi milioni 500, Chama Mafanikio chenye

Shilingi milioni 490 na Chama cha Mount Meru Hotel chenye Shilingi milioni 260.

Kutokufuatwa kwa Sheria ya Ushuru wa Stempu kwa kutokulipa Ushuru wa Stempu kwenye mikataba kunaiweka NSSF katika hatari ya kupewa adhabu na TRA.

iv. **Vyama vya Ushirika cha Akiba na Mikopo Kutolipa Mikopo**
Mikataba ya mikopo inahitaji Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo kulipa mikopo yake kila mwaka kwa NSSF. Niligundua kuwa Vyama vya Ushirika cha Akiba na Mikopo 14 vilikuwa havijalipa deni la Shilingi bilioni 4.8 tangu mwaka jana. Tulitaarifiwa kuwa NSSF wamechukua hatua za Kisheria kwa vyama hivyo vyote vilivyoshindwa kulipa mikopo hiyo.

Niligundua kuwa, malipo mengi ya vyama vya Ushirika cha Akiba na Mikopo yalikuwa hayafuati mpangilio wa malipo ya mwanzo. Kutokulipwa kwa deni lisilo na riba husika na wanachama wa vyama kunaleta wasiwasi juu ya kutolewa kwa mikopo hiyo na uwezekano wa kulipwa.

v. **Mikopo ya Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo kutolewa kwa Wanachama Wasio Wanachama wa NSSF**
Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo ya WADOKI kilipokea mkopo kutoka NSSF wa Shilingi milioni 838 kwa ajili ya kukopesha wanachama wa NSSF kufuatana na orodha ya wanachama wa NSSF uliowekwa kwenye maombi ya mkopo. Hata hivyo, wanachama 80 wasio wa NSSF walilipwa Shilingi milioni 200 tofauti na Makubaliano ya Mkopo. Aya namba 2 (2.2) inasema, "Mkopaji hapa anatakiwa kuhakikisha Mkopo uliopatikana kutoka NSSF utatakiwa kukopeshwa kwa wanachama wa NSSF kama ilivyoambatanishwa katika kiambatisho namba 1 cha Mkataba wa Mkopo."

Pia, niligundua kuwa, baadhi ya wanachama wa NSSF waliojumuishwa kwenye orodha ya awali iliyotumwa kwa ajili ya maombi ya mkopo hawakupata mkopo; na baadhi yao walipata chini ya maombi yao.

Menejimenti ya NSSF inatakiwa kufanya yafuatayo:

i. Kufuata kanuni na mahitaji ya Sera za Mikataba ya Mikopo wakati wa utoaji wa mikopo kwa wanachama wa Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo.
ii. Kuanzisha udhibiti madhubuti ili kuhakikisha malipo ya mikopo iliyotolewa yanafanyika kama inavyohitajika.

5.2.3 Udhaifu Uliogundulika kwenye Uwezekaji wa Ardhi

Taarifa za Fedha za NSSF zilionesha kuwa uliwekeza kwenye viwanja (Benki ya Ardhi) kwa ujumla vyenye thamani ya Shilingi bilioni 97.2. Niligundua upungufu kuhusu ununuaji na uwepo wa ardhi zilizonunuliwa kama ifuatavyo:-

i. Kulikuwa hakuna mipango na upembuzi yakinifu kuhalalisha sababu za kuwekeza katika rasilimali kinyume na aya ya 3.3 ya Sera ya Uwekezaji ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ya mwaka 2012 inayohitaji NSSF kuwekeza rasilimali zake katika uwekezaji unaolipa zaidi ili kuweza kuleta mafanikio kwa wanachama wake. Pia, niligundua mali zote za viwanja/mashamba zilikuwa bado hazijaendelezwa.

ii. Sikuweza kupata hati ya umiliki ya viwanja/mashamba vinne (4) kwa sababu vipo katika mzozo wa umiliki. Viwanja hivi vilikuwa ni Nunge Beach kilichopo Bagamoyo chenye ukubwa ekari 67.35; kiwanja namba 146/4 Barabara ya Old Moshi kilichopo Halmashauri ya Jiji Arusha chenye ukubwa wa ekari; Clement Mabina Farm Bugando Magu chenye ekari; na kiwanja namba 98 Barabara ya Nyerere (Pugu) Temeke chenye mita za mraba 8,825.

iii. Mfuko uliingia mkataba na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa ajili ya kununua viwanja 692 (viwanja 405 Kiseke na 287 Bugarika) kwa Shilingi 1,887,018,700. Hata hivyo, ni viwanja 156 tu vilielekezwa Kiseke; wakati hakuna kilichoelekezwa kwa upande wa Bugarika. Pia, tarehe 8 Septemba 2011, Mfuko ulialika kampuni ya HABCONSULT Limited ili kutoa huduma

iv. Kulikuwa na shamba namba 113 lililonunuliwa kwa Shilingi bilioni 1,260 Mapinga katika Manispaa ya Kinondoni chenye ukubwa wa hekta 127; lakini ni hekta 58 tu zilizokuwa zimetengwa na kufanyiwa kazi.

Ukaguzi uligundua kuwa hapakuwa na uangalifu wa kutosha kabla ya kununua viwanja/mashamba hayo ili kutathmini thamani yake katika soko, umiliki, na ukubwa wake; na hivyo, kuondoa mashaka kuwa Mfuko ulinunua viwanja hewa.

Menejimenti inashauriwa kuchukua hatua stahiki kuhakikisha viwanja/mashamba yaliyonunuliwa yanarudisha faida ya uwekezaji kama yalivyo malengo ya sera ya uwekezaji.

5.2.4 Mapungufu kwenye Mkataba wa Mshauri kwenye ununuaji wa Pan Africa Energy Limited ya Dola za Marekani 946,500 na Shillingi milioni 551.61

NSSF waliingia mkataba namba NSSF/CS/20/2014-2015 mnamo tarehe 12 Februari 2016 na Yakubu and Asssociates Chamber lengo la mkataba ikiwa ni kutoa huduma ya ushauri ili kuwezesha kupatikana kwa mshirika kampuni ya Pan Africa Energy Limited kwa ada ya utaalamu ya Dola za Marekani 946,500 na Shilingi milioni 551.61 kwa ajili ya matumizi ya ziada na kodi za ndani. Yafuatayo ni mapungufu yaliyogundulika:-

i. Kanuni namba 253 na 258 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 (PPR, 2013) imeweka vigezo vya kuchagua njia

mbalimbali na kusisitiza kutaarifu Bodi ya Udhibiti wa Manununuzi kuhusu kazi zenye utata kabla ya washauri kuwasilisha mapendekezo. Uhiari wa kuweka wazi maslahi haukuwepo wala kutangazwa. Hii ni kinyume na kanuni tajwa.

ii. Mshauri alikosa uzoefu uliohitajika kama ilivyoelekezwa kwenye Hadidu za Rejea iliyohitaji uzoefu wa mali zisizohamishika za ndani na mambo ya mazingira, Ushauri wa kodi za ndani na nje pamoja na leseni na kanuni za mfumo wa *hydrocarbon*. Pia iligundulika kuwa Kampuni ya Yakubu and Associate Chamber ndiyo ilikuwa imesajaliwa mwaka huo huo wa kukaribisha zabuni na washauri walikuwa hawana uzoefu na mazingira ya ndani.

iii. Mshauri alitakiwa kukagua taarifa ya uchunguzi iliyoandaliwa chini ya mkataba namba NSSF/CS/20/2014-2015 ulioingiwa mnamo tarehe 11 Desemba 2014 kwa ajili ya kutoa huduma ya ushauri wa ununuzi wa kampuni ya Pan Africa Energy Limited. Kanuni namba 257(2)(a) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 (PPR, 2013) iliyotumika na Bodi ya Zabuni ili kuhalalisha utoaji wa zabuni hiyo kama muendelezo wa kazi ya zamani haikuwa sahihi.

iv. Mkataba ulikuwa umekwisha muda wake tangu tarehe 26 Aprili 2016, lakini uliongezwa muda kupitia Kanuni namba 111(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 (PPR, 2013) inayomruhusu Afisa Masuuli kuongeza muda wa mkataba na kuelezea sababu ya kufanya hivyo. Mshauri aliwasilisha bili namba 01031604 ya tarehe 1 Machi 2016, lakini mpaka kufikia tarehe 7 Oktoba 2016 malipo yalikuwa hayajafanyika.

Maoni yangu ni kwamba, NSSF haikufuata vigezo vya kuchagua Mshauri kama vilivyoainishwa kwenye Kanuni za Manunuzi ya Umma na Hadidu za Rejea (ToR) zilizoandaliwa na Bodi ya Wadhamini.

Menejimenti ya Mfuko inashauriwa kuvunja/kusimamisha mkataba kuendana na kifungu namba 67.1 kwa sababu za Mshauri kutokuwa na uzoefu tosha unaohitajika kufanya kazi hiyo.

5.2.5 Shamba la Dungu na Mradi wa Uwekezaji Tuangoma

Mfuko uliingia mikataba mbalimbali yenye thamani ya Shilingi bilioni 165.4 kwa ajili ujenzi wa kijiji cha setilaiti katika Shamba la Dungu/Tuangoma Kigamboni katika Manispaa ya Temeke Dar es Salaam. Mfuko ulikuwa umeshaingia gharama ya Shilingi bilioni 73.4; Yafuatayo ni mapungufu yaliyoonekana:-

i. Kutokuwepo kwa Upembuzi Yakinifu kuhusu Miradi

NSSF ilitekeleza miradi bila kufanya upembuzi yakinifu ambao ungeupa Menejimenti uhakika wa uwekezaji husika. Kwa sababu hiyo, nilishindwa kupata misingi na vigezo vilivyoshawishi maamuzi ya Menejimenti kuwekeza, malengo ya uwekezaji na mipango ya kurudisha fedha zilizowekezwa.

ii. Eneo Lisilokuwa na Uhalisia la Shamba la Dungu

Katika kipindi cha kuanza mradi, NSSF iligundua kuwa sehemu ya ardhi ilikuwa inamilikiwa na Shirika la Nyumba (NHC); hivyo, baadhi ya ujenzi ulihamishiwa Tuangoma. Hata hivyo, Menejimenti haikuweza kutoa nyaraka za ununuzi wa viwanja vya Tuangoma na kama vilikuwa vina ukubwa sawa, vinauzika kwenye soko na kiwango cha kurudisha uwekezaji kama ilivyo kwa Dungu. Pia, maamuzi ya Bodi ya Wadhamini au Menejimenti kuhamishia majengo Tuangoma hayakupatikana kwa ajili kupitiwa na wakaguzi.

iii. **Utoaji wa Zabuni Nyingi kwa Ajili ya Kusambaza Maji Shamba la Dungu**

Niligundua kuwa NSSF ilitoa taarifa ya kumzawadia Mzabuni Canopies International kwa zabuni namba PA/004/2014-2015/HQ/W/27 kwa ajili ya kusambaza maji katika Shamba la Dungu tarehe 7 Septemba 2016; lakini shughuli hii ilikuwa tayari imeshazawadiwa kwa wazabuni watatu (3) kwa thamani ya Shilingi bilioni 4.363, hivyo, kuwa ngumu kupata uhalali wa zabuni ya ziada. Kulikuwa hakuna ufafanuzi ulioelezea uharaka wa zabuni hii na ni kwa jinsi gani mkataba uliopo ungeathiri utoaji wa zabuni hii na eneo gani mradi utatekelezwa.

Kuna hatari kwamba Mfuko unaweza kutopata marejesho mazuri ya thamani ya uwekezaji wa miradi inayoendelea Dungu na Tuangoma.

Menejimenti ya NSSF inashauriwa kuchunguza mradi wa Shamba la Dungu/Tuangoma ili kupata uhalisia wa eneo lake; na kusuluhisha tuzo zote za mikataba mingi iliyotolewa kwenye usambazaji wa Mtandao wa maji katika Shamba la Dungu.

NSSF inashauriwa kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kutekeleza mradi wowote ili kupata uhakika wa kupata marejesho mazuri ya uwekezaji katika miradi yake.

5.3 Mamlaka ya Ukanda wa Kutengeneza Bidhaa za Kuuza Nje ya Nchi (EPZA)

5.3.1 Kutokujitosheleza kwa Ufuatiliaji na Tathmini za Leseni za Wawekezaji wa EPZA

Kifungu cha 14 (1) cha Sheria ya Kanda ya Maalum ya Kiuchumi (SEZ) ya 2012 inataka Mamlaka kuanzisha, kuendeleza na kusimamia uendeshaji shughuli za kanda maalumu za kiuchumi

kwa niaba ya serikali. Aidha, Kanuni ya 5(a) ya Kanuni ya Kanda Maalumu za Kiuchumi, 2012 inataka Mamlaka kudhibiti, kusimamia na kufuatilia shughuli za kila siku za taasisi za kibiashara zilizopo katika Ukanda Maalum wa Kiuchumi, na wakazi waliopo katika kila kanda maalum ya kiuchumi ili kuhakikisha Sheria na Kanuni zinafuatwa.

Ukaguzi ulibaini ya kwamba EPZA haikuwa na mfumo wa kutathmini uwekezaji, utendaji na utekelezaji wa matakwa ya leseni pamoja. Kwa mwaka huu wa fedha, tulibaini kwamba Mamlaka haikufanya ziara hata mara moja kwenye maeneo ya uwekezaji na uzalishaji.

EPZA wanashauriwa:-

(a) Kufuatilia na kutathmini wawekezaji ili kuhakikisha maendeleo na utendaji wa jumla wa EPZA kwa uchumi wa Taifa.

(b) Kuanzisha Idara ya ufuatiliaji na tathmini ili kutekeleza jukumu la usimamizi, udhibiti, na ufuatiliaji wa shughuli za kila siku.

5.3.2 Ukosefu wa Ushirikiano wa Taarifa (data) kati ya TRA na EPZA

Ili kupata msamaha wa kodi, wawekezaji wanapaswa kuwasilisha orodha ya bidhaa zinazohitaji misamaha ya kodi kwa Mamlaka ya EPZA ambayo inafanya tathmini na kupendekeza kwa Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA) kwa ajili ya kupitishwa. Ukaguzi ulibaini kuwa EPZA ilikuwa na wawekezaji 158 ambao wamesajiliwa na kuripotiwa TRA. Hata hivyo, mfumo wa EPZA na mfumo wa TRA haukuwa na muunganiko wa pamoja katika utendaji. Pia, hakuna taratibu za ufuatiliaji uliowekwa kuweza kupatanisha taarifa kati ya hizi Mamlaka mbili. Kutokana na hili, EPZA haiwezi kuamua kwa usahihi kiasi cha misamaha ya kodi kwa wawekezaji na jinsi misamaha hiyo inavyotumika.

Ukosefu wa ushirikiano wa taarifa baina ya EPZA na TRA unadhoofisha uwezo wa EPZA kupatanisha misamaha ya kodi wanayopewa wawekezaji na TRA dhidi ya taarifa zao.

EPZA wanapaswa kuwasiliana na TRA ili kupata taarifa sahihi na muhimu za wawekezaji na miradi yao, kuwezesha taarifa zote muhimu kupatikana kwa wakati hasa katika kipindi cha usimamizi.

5.3.3 Utendaji Duni wa Wawekezaji Wenye Leseni

Serikali ilianzisha programu ya EPZ ya mwaka 2002 ikiwa na malengo ya kuanzisha uuzaji wa nje kwa uwekezaji unaofanywa ndani ya ukanda ulioainishwa ili kujenga ushindani wa kimataifa kwenye bidhaa zinazouzwa nje, hatimaye kuleta ukuaji wa uchumi.

Mnamo mwaka 2006, kanda maalum za kiuchumi (SEZs) zilianzishwa kama mkakati wa kufikia Uchumi wa Kati mwaka 2020'. Malengo yake yalikuwa:- Kukuza maendeleo ya haraka na muhimu katika ukuaji wa uchumi; kupata mapato yatokanayo na kuuza bidhaa nchi za nje; kutengeneza ajira; na kuvutia uwekezaji binafsi katika aina ya uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja'(FDI)' na uwekezaji wa ndani '(DDI)' inayotokana na sekta ya uzalishaji na sekta ya huduma.

Kama sehemu ya taratibu za kupata leseni, mwekezaji huandaa andiko la mradi ambao unafanyiwa tathmini; ambapo mitaji ya uwekezaji na ajira zitakazotengenezwa zitakuwa sehemu ya vigezo ambavyo baadaye vinakuwa mikataba ya kiutendaji kati ya EPZA na mwekezaji husika baada ya kupatiwa leseni.

Ukaguzi ulipitia mafaili 13 kati ya 57 ya wawekezaji hai wenye leseni. Uhakiki wetu ulibainisha kwamba mtaji halisi wa uwekezaji ulikuwa Shilingi bilioni 43.4 sawa na asilimia 33 ya jumla ya ahadi mtaji wa uwekezaji wa Shilingi bilioni 132.4.

Wakati ajira halisi iliyotokana na uwekezaji ni 3,850, sawa na asilimia 87, dhidi ya ahadi ya ajira 4,439 kama ilivyoainishwa katika pendekezo la mradi na wawekezaji. Hii ilisababishwa na EPZA kushindwa kutekeleza mkataba wa utendaji kati ya EPZA na mwekezaji baada ya leseni kutolewa.

Kuna hatari ya Mamlaka kushindwa kutimiza malengo yake ya kimkakati katika suala uwekezaji wa mtaji na utengenezaji wa ajira kutokana na kushindwa kutekeleza mikataba ya kiutendaji na wawekezaji.

EPZA inashauriwa kuanzisha mfumo wa kuwashawishi wawekezaji kuzingatia mapendekezo yao yaliyowasilishwa wakati wa maombi ya leseni na kusaini mkataba wa utendaji na wawekezaji.

5.4 Mfuko wa Pension wa LAPF

5.4.1 Sera kwa Ajili ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Uwekezaji

Aya 5(2) (f) ya Mwongozo wa Uwekezaji kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa mwaka 2015 unazitaka Bodi za Wadhamini za kila mfuko kuhakikisha, katika kiwango cha chini, sera za uwekezaji zinakuwa na taratibu za kufuatilia na kutathmini uwekezaji. Taratibu hizo zitauwezesha Mfuko kujua matatizo na iliposhindwa kufikia malengo na kuchukua hatua za haraka kurekebisha hali husika. Kuweka taratibu katika sera kunasaidia kufanya utekelezaji kwa kuwa inakuwa lazima kwa menejimenti au/na wale wanaohusika na utawala bora.

Nimebaini kuwa sera ya uwekezaji ya LAPF haijitoshelezi kwa kazi za ufuatiliaji na tathmini ya uwekezaji. Hii ni kwa kuwa zinalenga kwenye marejesho/mapato (returns) peke yake na kuacha mambo mengineyo. Hivyo, uwekezaji umekuwa ukifanyiwa tathmini kwenye mapato ya marejesho peke yake. Hii haijitoshelezi kwa kuwa imelenga uwanda mmoja tu wa

uwekezaji unaozalisha mapato; na kuacha uwanda wa uwekezaji unaoendelea kufanyika ambao ni chanzo cha mapato ya baadaye na nyanja nyingine ambazo, kwa namna moja au nyingine, zinaathiri uhakika wa mapato katika uwekezaji. Sera ya uwekezaji ya LAPF haijatazama ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya uwekezaji, tathmini ya asilimia ya ukamilifu wa malipo kwa wakandarasi dhidi ya ukamilifu wa ujenzi wa miradi. Sera haijaongelea hoja ya urejeshaji wa mikopo na ulipaji wa kodi wa wapangaji.
Menejimenti ya LAPF inashauriwa:

- Kuongeza nyanja za kufuatilia na kutathmini uwekezaji ili kuwa na ufanisi/ubora katika utendaji (effective performance) na kufikia malengo yake.
- Kuipitia sera ya uwekezaji kuhusiana na ufuatiliaji na tathmini ili kuongeza uwanda na kujumuisha nyanja ambazo zinaathiri utendaji wa Mfuko katika utekelezaji wa bajeti ya uwekezaji, tathmini ya asilimia ya ukamilifu wa malipo kwa wakandarasi dhidi ya ukamilifu wa miradi husika ya ujenzi na kuongelea urejeshaji wa mikopo na ulipaji wa kodi wa wapangaji.

5.4.2 Udhaifu katika kufuata Matakwa ya Sheria ya SSRA

Mfuko wa LAPF unatakiwa kufuata vifungu mbalimbali vya sheria ya SSRA. Ukaguzi umebaini maeneo mbalimbali ambapo sheria husika haikufuatwa kama ifuatavyo:

- Kifungu cha 271(d) cha Sheria ya SSRA kinataka mifuko kuwasilisha taarifa inayoonyesha michango ya wanachama ambayo haijalipwa kwa kipindi kinachozidi siku thelathini (30) mara moja. Ukaguzi umebaini kuwa taarifa za robo mwaka peke yake ndizo zilizowasilishwa SSRA na Benki Kuu (BOT). Kifungu husika, kinataka taarifa za michango peke yake ndizo

ziwasilishwe mapema badala ya taarifa za robo mwaka peke yake kama inavyofanyika.

- Kifungu cha 53(1) cha Sheria ya SSRA kinataka taarifa ya mwaka kuwasilishwa SSRA miezi sita (6) baada ya kumalizika mwaka wa fedha. Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2015, ripoti ya mwaka ilitakiwa kutumwa tarehe 30 Disemba 2015. Ukaguzi umebaini kuwa, ripoti ya mwaka ilisainiwa na Bodi ya Mfuko Februari 2016. Hii inaonesha kuwa ripoti ilitayarishwa na kuwasilishwa baada ya kipindi kilichoainishwa na Sheria.

Hii inaonesha kutofuatwa kwa matakwa ya sheria ya SSRA; ambapo, inaweza kusababisha adhabu.

Menejimenti inashauriwa kutii matakwa ya Sheria ya SSRA ili kuondokana na matatizo yanayoweza kusababishwa na kutokutii Sheria husika.

5.4.3 Ufanisi Mdogo katika Kukusanya Kodi ya Pango

Mfuko wa Pensheni wa LAPF uliingia mikataba ya kupangishia wapangaji ambapo wapangaji; walihitajika kulipa kodi ya pango mwanzoni. Hata hivyo, iligundulika kuwa jumla ya Shilingi milioni 774 zilikuwa zinadaiwa zaidi ya miezi mitatu. Shilingi milioni 261 zilikuwa zinadaiwa kwa zaidi ya miezi kumi na miwili.

Hali hii inaathiri kwa kiasi kikubwa hali ya kifedha ya Mfuko; hatimaye itaathiri uwezo wake kwa ujumla. Hii ni kwa sababu mapato yanayotokana na kodi ya pango yanachangia kwa kiasi kikubwa mapato kwa ujumla.

Menejimenti inashauriwa kufuatilia kwa umakini ukusanyaji wa kodi ya pango unafanyika na kwa wakati.

5.4.4 Uwekezaji katika Kampuni Tanzu

Mfuko wa Pensheni wa LAPF unamiliki hisa kwa asilimia 80 kwenye kampuni ya Mwanza Commercial Complex Company

Limited (MCCCL) na asilimia 60 kwenye kampuni Msamvu Properties Company Limited (MPCL). Hisa zilizobaki za kampuni ya Mwanza Commercial Complex Company Limited (MCCCL) zinamalikiwa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza na za Msamvu Properties Company Limited (MPCT) zinamilikiwa na Halmashauri ya Mji wa Morogoro.

Kwenye taarifa za MPCT, Halmashauri ya Mji wa Morogoro ilichangia ardhi iliyokuwa na thamani ya Shilingi bilioni 2.9, wakati Mfuko ulikubali kutoa fedha zote zilizohitajika kujenga kituo cha mabasi. Kwenye taarifa ya MCCCL, Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilichangia ardhi iliyokuwa na thamani ya Shilingi bilioni 6.2, wakati Mfuko ulikubali kutoa fedha zote zilizohitajika kujenga duka kubwa la kisasa. Kufikia tarehe 30 Juni 2016, Mfuko wa Pensheni wa LAPF ulichangia Shilingi bilioni 7.3 kwenye kampuni ya MPCT na Shilingi bilioni 65.9 kwenye kampuni MCCCL.

Aya ya 12 katika Mkataba wa Makubaliano (MoU) wa Mfuko na Halmashauri ya Mji wa Morogoro na aya ya 14 katika Mkataba wa Makubaliano (MoU) wa Mfuko na Halmashauri ya Jiji wa Mwanza inajumuisha kifungu kinachosema “kampunzi hizo zitahamishiwa kwenye Halmashauri husika pindi Mfuko utakaporudisha fedha ilizowekeza pamoja na riba zilizokubalika na pande zote”. Hakuna maelezo zaidi yaliyopo kuhusiana na suala hili kwenye mikataba hiyo.

Hata hivyo, Menejimenti ya Mfuko wa Pensheni wa LAPF ina maoni kwamba kifungu hicho kilichopo kwenye mkataba hakina uhalali na hakuna mali itahamishwa kama ilivyoelekezwa baadaye. Pia, Menejimenti kuwa inaamini mpango huu haujumuishi huduma ya ada (service concession arrangement) kwa mujibu wa IFRIC 12; ambapo Serikali (kupitia Halmashauri) haijaweka bei ya kutoza watumiaji wa standi ya mabasi. Bei zinawekwa na Bodi na kupitishwa na wanahisa wa AGM.

Wakati utaratibu wa kimahesabu wa kampuni tanzu unaweza kuwa sahihi kulingana na uhalisia dhidi ya utaratibu (substance over form), inaweza kupingana kwenye upande wa kisheria na wadau baadaye; ambapo, matokeo yake yanaweza kuleta kutokuelewana.

Menejimenti inatakiwa kupitia Mkataba wa Makubaliano (MoU) na kufanya marekebisho ili kuonesha kwa wazi kuwa hakuna uhamisho wa uwekezaji kwenye kampuni tanzu utafanyika hapo baadaye.

5.5 Mfuko wa Pensheni PPF

5.5.1 Mapungufu katika Kurejesha Mikopo na Wadaiwa

PPF inatoa mikopo kwa wadau mbalimbali kama vile wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo, Serikali, taasisi binafsi na kwa wafanyakazi mbalimbali kama ilivyoanishwa kwenye Sheria ya SSRA na miongozo ya uwekezaji ya mifuko ya pensheni.

Marejesho ya mikopo ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo yanafanyika kupitia mishahara ya wafanyakazi kwa wale wafanyakazi wa Serikalini. Kutokana na mabadiliko katika mfumo wa malipo ya mshahara wa Hazina. Hazina sasa inaweka mishahara moja kwa moja kwenye akaunti za wafanyakazi, hali hii inapunguza uwezo wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo kupokea marejesho ya mkopo moja kwa moja. Kwa taasisi binafsi, malipo yalipaswa yafanyike mara moja. Tumegundua mapungufu yafuatayo katika marejesho:-

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2016 wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo walipewa mikopo yenye julma ya shilingi bilioni 42.81. Ukaguzi ulibaini kwamba Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo 14 kumi na vinne vilikuwa na

madeni ya nyuma yaliyokomaa yenye thamani ya shilingi bilioni 2.78 lakini hayajalipwa. Pamoja na jitihada zilizofanywa na menejimenti kufuatilia marejesho haya, kuna hali inayoashiria kwamba PPF inaweza kushindwa kupokea marejesho hayo kutoka kwenye mifuko ya SACCOS kwa kuwa mifuko hiyo mingi iko katika taasisi za Serikali.

Jedwali lifuatalo linaonesha mikopo ambayo imeiva kutoka Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo lakini bado hajalipwa:

Jedwali Na. 3: Mikopo ya SACCOS Ambayo Haijalipwa

Na.	Jina la Chama	Kiasi cha deni	Kiasi kilicholipwa	Kiasi kinachodaiwa
		Shilingi bilioni	Shilingi bilioni	Shilingi bilioni
1	Chama Vya Kuweka na Kukopa cha SUA	0.61	0.51	0.11
2	Chama IFM	1.91	1.78	0.13
3	NYUMBU	0.49	0.34	0.15
4	Chama cha TPRI	1.53	1.09	0.44
5	Chama cha MLIMANI	0.41	0.38	0.03
6	Chama cha TIB	1.10	0.99	0.11
7	Chama cha TPAWU	0.28	0.18	0.09
8	Chama cha OUT	0.17	0.09	0.07
9	Chama cha DIT	0.34	0.31	0.03
10	Chama cha TSN	1.97	1.15	0.82
11	Chama cha NDC	2.17	1.75	0.42
12	Chama cha RELI	1.26	0.95	0.31
13	Chama cha DUCE	0.10	0.09	0.01
14	Chama cha SANAPA	0.07	0.05	0.02
	Jumla	**12.42**	**9.67**	**2.75**

Chanzo: Taarifa kutoka Mfuko wa Pensheni PPF

Fedha inapokuwa kwenye madeni kwa muda mrefu inaharibu na kuathiri utendaji wa Mfuko. Pia, kitendo cha Serikali kushindwa kutoa hati fungani kwa wakati kama inavyotakiwa, kinahatarisha

uwezo wa Mfuko kupokea marejesho ya mikopo kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, pamoja na NIDA; ambapo mikopo hii imedhaminiwa na Serikali.
Menejimenti ya Mfuko inashauriwa kuendelea kuchukua hatua na kupanga mikakati madhubuti ili kuhakikisha Kiasi cha mikopo wanachodaiwa wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo inalipwa. Pia iendelee kufanya mawasiliano na Wizara ya Fedha ili kuhakikisha hati fungani zinatolewa kwa ajili ya kulipa deni.

5.5.2 Udhaifu katika Kufuata Matakwa ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti ya Hifadhi za Jamii

Kifungu cha 27(1)(d) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti ya Hifadhi za Jamii kinataka mifuko kuwasilisha mara moja taarifa inayoonesha michango ya wanachama ambayo haijalipwa kwa kipindi kinachozidi siku thelathini (30).

Ukaguzi umebaini kuwa PPF haikupeleka ripoti inayoonesha michango ya wanachama ambayo haijalipwa kwa siku zinazozidi 30. Imebainika kwamba menejimenti imekuwa ikituma taarifa za robo mwaka kama inavyotakiwa na mwongozo wa uwakezaji ya mifuko ya jamii lakini haiendani na sheria za SSRA. Pia, nilibaini kwamba msimamizi (Mamlaka ya Udhibiti ya Hifadhi za Jamii) amekuwa ikitilia mkazo ripoti ya robo mwaka tu; na kutotilia mkazo taarifa inayoonyesha michango ya wanachama ambayo haijalipwa kama inavyotakiwa na sheria ya Mamlaka ya Udhibiti ya Hifadhi za Jamii. Menejimenti ya Mfuko ilikubali kufanya majadiliano na Mamlaka ya Udhibiti ya Hifadhi za Jamii ili kupanga utaratibu wa kutuma ripoti hizi kama inavyotakiwa na sheria ya Mamlaka ya Udhibiti ya Hifadhi za Jamii 27(1)(d).

Hii inaonyesha kuwa PPF haikufuata matakwa ya sheria ya Mamlaka ya Udhibiti ya Hifadhi za Jamii. Hali hii ambapo inaweza kusababisha adhabu kwa Mfuko hivyo kuathiri shughuli zake.

Menejimenti inashauriwa kufuata matakwa ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti ya Hifadhi za Jamii ili kuondokana na matatizo yanayoweza kusababishwa na kutokutii Sheria husika.

5.5.3 Kushindwa Kufikiwa kwa Malengo ya Mwaka ya Miradi ya Uwekezaji

Kifungu cha 14 cha Sera ya uwekezaji wa PPF kinauhitaji mfuko kujitathmini wenyewe kwa kulinganisha malengo ya muda waliojiwekea dhidi ya utendaji halisi. Tathmini inasaidia kuwezesha mfuko kujikita kwenye kufikia malengo waliojipangia.

Nilibaini ya kwamba, katika mwaka wa fedha 2015/2016 PPF hawakuweza kufikia malengo ya bajeti ya uwekezaji kwa shilingi bilioni 131.55 (Bajeti ya shilingi bilioni 207.74 kulinganisha na kiasi halisi kilichotolewa cha shilinig bilioni 76.19) sawa na asilimia 63 ya matumizi yaliyopangwa ya miradi hiyo ya uwekezaji.

Matumizi ya kiwango cha chini cha bajeti ya dhamana za fedha yalichangiwa kwa kiasi kikubwa kwa kutokutoa hati fungani za makampuni kwenye soko; ambapo, Shilingi bilioni 18.03 zilibajetiwa na shilingi bilioni 14.14 hazikuweza kutumika.

Utendaji mdogo wa uwekezaji wa mali umesababishwa na bajeti ya isiyo isyoangalia vipaumbele. Nina wasiwasi kwamba, PPF haitaweza kufikia malengo iliyojiwekea; hivyo kuhatarisha azma yake ya malengo ya kimkakati ya uendeshaji wa kiutendaji. Hivyo, Menejimenti inashauriwa kuchukua hatua madhubuti ili kuhakikisha kazi ambazo hazijatekelezwa zinatekelezwa kama ilivyopangwa.

5.5.4 Kiwango cha chini cha upangishaji wa majengo ya PPF

PPF wameajiri wasimamizi wa majengo kwa ajili ya uwekezaji wake wa majengo yaliyoko sehemu mbalimbali nchini. Wasimamizi majengo hao wamepewa majukumu ya kuleta wapangaji na kuhakikisha kodi ya pango inakusanya na mfuko.

Katika kutathmini kiwango cha upangishaji majengo, nilibainisha kwamba baadhi ya sehemu za majengo haya hayajapangishwa kwa kadiri ya malengo yao. Kwa kuwa na kiwango cha chini cha ukodishaji wa dola za kimarekani 12 kwa mwezi, mfuko unapoteza kiasi cha dola za kimarekani 43,000 kwa mwezi, sawa na dola za kimarekani 516,000 kwa mwaka. Hii inashiria ugumu wa kuweza kuongeza thamani kwenye mfuko. Jedwali lifuatalo linaonesha hasara iliyoingiwa:

Jedwali Na. 4: Hasara iliyoingiwa na PPF

Na	Jina la Jengo	Eneo linaloweza kupangishwa	Eneo linalotarajiwa	Eneo lililopangishwa	Uwiano wa upangishaji	Uwiano unaokadiriwa	Hasara kwa dola za kimarekani
1	Jengo la PPF na egesho la magari	13,567	12,210.3	9,900	72.97%	90.00%	27,723.60
2	Jengo la PPF Plaza Mwanza	3,664	3,297.6	3,089	84.31%	90.00%	2,503.20
3	Jengo la PPF Plaza Arusha	7,515	3,757.5	2,670	35.53%	50.00%	3,050.00
	Jumla						**33,277**

Chanzo: Taarifa za Mahesabu za Mfuko wa Pensheni PPF

Menejimenti ilieleza kwamba wanafanya kazi kwa ukaribu sana na wasimamizi majengo ili waweze kufikia malengo ya upangishaji majengo kwa asilimia 90. Aidha, menejimenti inafanya tathimini na kusimamia utendaji kazi wa wasimamizi wa majengo katika kila kipindi cha robo mwaka.

Nina shaka kwamba, majengo yasiyo na wapangaji yatasababisha kukosekana kwa mapato. Kadhalika, nina mashaka na utendaji

kazi wa wasimamizi majengo ambao umesababisha mfuko kutoweza kufikia malengo yake kuhusiana na kiwango cha upangishaji.

Menejimenti inashauriwa kufanya yafuatayo:

i. Kuendelea kuwafuatilia wasimamizi majengo kwa ukaribu ili kuweza kutathmini uwezo wao wa kuleta wapangaji na kuhakikisha kodi zinakusanywa.
ii. Kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha malengo ya upangishaji waliojiwekea yanafikiwa.

5.5.5 Mapato kwenye miradi ya uwekezaji

Kifungu cha 9(1) cha sehemu ya miongozo ya uwekezaji ya mipango ya Hifadhi ya jamii kinaihitaji Bodi ya Wadhamini ya kila mpango kuhakikisha kwamba uwekezaji wowote wa tofauti na dhamana za serikali unaleta mapato ya zaidi kuliko mapato ya hati fungani.

Hata hivyo, ukaguzi wetu ulibaini kwamba, PPF ina uwekezaji wa miradi yenye kuleta mapato ya chini kuliko dhamana za serikali katika wakati wa utekelezaji. Haya ni matokeo ya kutokuwa na mchanganuo unaojitosheleza wa uwekezaji katika majengo.

Menejimenti inadai kwamba kuwekeza katika majengo ni njia madhubuti ya kutunza mtaji. Pia, makadirio ya mapato yaliowekwa yamezingatia makadirio ya makusanyo ya mapato tu bila kuzingatia ongezeko la thamani la majengo.

Kuna hatari ya mfuko kupoteza nafasi ya kupata viwango vikubwa vya mapato kwa kutowekeza serikalini. Huu ni uwekezaji usiokuwa na mashaka na una mapato makubwa kulinganisha na kuweka kwa watu binafsi.

Menejimenti inashauriwa kufanya tathimini ya kutosha kuhusiana na uwekezaji wa majengo kwa kujumuisha umri utarajiwao wa majengo na kuweka makadario yanayoweza kufikiwa kwa kuangalia ongezeko la thamani katika kipindi kilichoainishwa na kufanya mlinganisho ulio sawia.

5.5.6 Utoaji wa Mikopo kwa SACCOS Zaidi ya Ukomo wa Kutoa

PPF inatoa mikopo kwa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (**SACCOS**) kwa kutumia vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na taarifa za fedha zilizokaguliwa ili kuweza kutumika katika kukopa ambayo inasaidia kutambua hatari ya mikopo kwenye uwekezaji.

Hata hivyo, imebainika kwamba Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo cha SANAP kilipatiwa mkopo wa shilingi milioni 500 badala ya shilingi milioni 234.40. Kiasi cha mkopo kilichotolewa zaidi ni shilinig milioni 265.6 zaidi ya kiwango cha mkopo kilichotakiwa kulingana na taarifa za fedha zilizokaguliwa.

Kutoa mkopo zaidi ya kiwango kinachostahili kunaongeza hatari ya uwezakano wa kutokulipwa kwa mkopo huo. Hivyo, PPF inashauriwa kuhakikisha mikopo yote inatolewa katika kiwango kinachostahili kufuatana na sera ya mikopo ya Mfuko.

5.6 Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (PSPF)

5.6.1 Uwekezaji Usiofanya Vizuri

Mfuko wa pensheni wa watumishi wa umma ulianza ujenzi wa nyumba za bei nafuu ziapatazo 1,144 mnamo mwaka 2008. Mfuko ulipanga kutekeleza mradi kwa awamu nne. Awamu ya kwanza nyumba 668, awamu ya pili nyumba 141, ya tatu nyumba 200, na awamu ya nne nyumba 135.

Mfuko ulianza utekelezaji wa sehemu ya kwanza ya mradi kwa kujenga nyumba 666 katika mikoa ya Dar es salaam, Mtwara, Morogoro, Shinyanga, Tabora na Iringa kwa gharama ya TZS 29.7 bilioni. Nyumba hizo zilitakiwa kuuzwa ndani ya miaka miwili baada ya kukamilika mwezi Julai 2014 kwa kadirio la faida ya TZS 5.1 bilioni kwa kipindi chote cha mradi. Aidha, nilibaini kuwa mfuko uliuza nyumba 304 kati ya 666. Nyumba ziliuzwa ni asilimia 46 tu.

Pia nilibaini kuwa PSPF imekuwa na changamoto katika uuzaji wa nyumba. Changamoto hizo inawezekana zilisababishwa na kukosekana kwa huduma za kijamii.

Menejimenti ya mfuko inashauriwa kufanya yafuatayo;

i. Kuhakikisha wanaweka huduma za kijamii kwenye miradi ya Kihonda, Morogoro, Tabora, Buyuni – Dar es Salaam.

ii. Kuwa na Mpango mkakati kwa ajili ya kuuza nyumba zilizobaki na kukusanya mapato ya nyumba zilizouzwa kwa mkopo.

5.6.2 Ukiukwaji wa Taratibu za Uwekezaji

Mamlaka ya Mifuko ya Hifadhi za Jamii na Benki kuu ya Tanzania ilitoa muongozo wa uwekezaji kupitia kifungu 26(2) cha Sheria ya Mamlaka ya Mifuko ya Jamii namba 8 ya 2008 ambayo imeainisha kikomo cha kukopa na maeneo yanayoruhusiwa kwa mifuko ya hifadhi za jamii kufanya uwekezaji, benki na taasisi za fedha. Viwango vilivyowekwa ni asilimia 20-70 ya jumla ya mali kwenye dhamana za serikali na asilimia 10% ya mikopo.

Tulibaini kwamba Mfuko wa pensheni wa watumishi wa umma uliwekeza asilimia 3.32 kwenye dhamana za serikali ya jumla ya

mali zote na mkopo kwa serikali wa asilimia 25.69 ya jumla ya mali zote kinyume na ukomo kama sheria inavyosema.

Pia, kifungu namba 27 cha sheria ya mamlaka ya kudhibiti mifuko ya jamii kinaitaka mifuko ya jamii yote kutumia fedha za wanachama kwa ajili ya manufaa ya wanachama na si vinginevyo. Hii inamaanisha kwamba, viwango vilivyowekwa inabidi viangaliwe wakati wote.

Kutokufuatwa kwa viwango vilivyopangwa kunaweka michango ya wanachama wa Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Umma kwenye hatari ya kupoteza; hivyo wanachama kupoteza mafao yao.

Uongozi unashauriwa kufuata maelekezo ya Mamlaka ya Kudhibiti Mifuko ya Jamii. Pia, iweze na kuandaa mikakati ambayo itawanufaisha wanachama na kuwaondolea matatizo yasiyo ya lazima.

5.6.3 Tathmini ya uwezo wa Mfuko

Taarifa ya tathmini ya uwezo wa wa Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Umma ya mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2014 ambayo iliandaliwa na Muhana & Co Actuaries & Consultants ilionyesha kuwa Mfuko una jumla ya fedha za Shilingi milioni 1,306,707; na deni halisi lilikuwa Shilingi trilioni 12.46 Hivyo kufanya upungufu wa shilingi trilioni 11.15.

Ukaguzi Ulibaini Mambo Yafuatayo;

i. Jumla ya madeni yote yaliyothaminishwa yalikuwa ni shilingi milioni 12,460,217. Hii inajumuisha kiasi cha shilingi milioni 7,224,634 ambayo ni deni la Serikali; shilingi milioni 4,553,294 deni la wafanyakazi 99 waliopo hadi Juni 30, 2016; na shilingi milioni 2,671,340 ikiwa ni malipo kwa wafanyakazi waliostaafu kati ya mwaka 2004 hadi Juni 30, 2014. Haya ni

malipo ya kiinua mgongo na stahiki zao za kila mwezi ambazo hazikulipwa na riba zake.

ii. Barua kutoka Wizara ya fedha yenye kumbukumbu namba CJA.452/479/01 ya tarehe 3 Novemba mwaka 2015 kwenda Benki kuu ya Tanzania kuomba dhamana maalumu ya kiasi cha shilingi milioni 2,671,340. Serikali, kupitia kikao cha Baraza la Mawaziri kilichofanyika tarehe 5 Machi 2015, ilipitisha dhamana maalum kwa ajili ya kulipia kiasi cha deni cha shilingi milioni 2,671,340 ambalo Serikali inadaiwa na Mfuko wa Hifadhi za Jamii wa PSPF. Inajumuisha malipo yaliyofanywa na PSPF kwa wafanyakazi 99 waliostaafu kuanzia mwaka 2004 hadi 30 Juni, 2015 ikiwa ni kiinua mgongo na stahiki zao za kila mwezi ambazo hazikulipwa na riba zake.

iii. Ripoti ya ya tathmini inaonyesha makadirio ya mapato na matumizi kutoka PSPF kwa ajili ya kutathmini hali ya kifedha ya muda mrefu na mfupi. Ripoti ilibaini kushuka kwa mapato kwenye uwekezaji. Jedwali lifuatalo linaonesha makadirio ya mzunguko wa fedha kuanzia mwaka 2015 hadi 2019.

Jedwali Na. 5: Makadirio ya Mzunguko wa Fedha

Mwaka	Mapato ya michango 'Shilingi bilioni	Mapato kwenye uweekezaji 'Shilingi bilioni	Jumla ya Mapato 'Shilingi bilioni	Faida za matumizi 'Shilingi bilioni	Total outgo* 'Shilingi bilioni	Makusanyo kwenye Mfuko 'Shilingi bilioni	Jumla ya makusanyo halisi ya mapato Shilingi bilioni
2015	0.65	0.11	0.76	0.84	0.88	1.19	1.19
2016	0.74	0.10	0.84	0.93	0.97	1.06	0.99
2017	0.77	0.08	0.85	1.02	1.06	0.85	0.75
2018	0.83	0.06	0.89	1.09	1.14	0.60	0.50
2019	0.89	0.03	0.92	1.21	1.26	0.26	0.21

Chanzo: Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Umma

Ukaguzi ulibaini kuwa kuna umuhimu wa kuibadili sheria ya Mafao ya Kustaafu ya Watumishi wa Umma ya mwaka 1999 kuhusiana na madeni ya watumishi ya kabla ya mwaka 1999. Kifungu cha 75 cha sheria hiyo kinataka majukumu, haki, na madeni yaliyokuwa yakitekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Pensheni kabla ya kuwepo sheria hii kuhamishiwa kwenye Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma

Pia, kifungu namba 46 cha Sheria hiyo kinasema kuwa, ***"Kama Mfuko kwa wakati wowote ukishindwa kulipa kiasi chochote ambayo ulitakiwa kulipa chini ya Sheria hii, jumla ya kiasi kinachohitajika kulipwa kitatolewa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kama mkopo; na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma utafarudisha fedha kwa Serikali hapo baadaye".***

Kifungu hiki kina maana kuwa fedha zitakazolipwa kwa Mfuko kutoka Mfuko mkuu wa Serikali zitakuwa ni deni na zitatakiwa kurudishwa pindi hali ya Mfuko wa Pesheni kwa Watumishi wa Umma itakapoimarika. Kutokana na mapendekezo kadhaa yaliyofanyika, sharia hii kwa sasa haiendi na hali halisi hivyo inahitaji kurejewa.

Kuchelewa kwa Serikali kulipa madeni yake, kutasababisha Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma kutoweza kutatua matatizo yake ya kifedha.

Ili kuweka mkazo na kuipa nguvu barua tajwa hapo juu pamoja na makubaliano mbalimbali na Serikali, ninashauri Sheria ya sasa kubadilishwa ili kutambua hali ya sasa ya madeni ya kabla ya mwaka 1999 (pre-1999 employee liabities) kisheria.

Menejimenti inashauriwa kuwasiliana na Wizara ya fedha ili kuhakikisha serikali inalipa madeni yake na kutoa dhamana sisizo za kifedha ili kuimarisha hali ya kifedha ya mfuko.

5.7 Mamlaka ya Udbiti Mawasiliano Tanzania (TCRA)

5.7.1 Mitambo Michache Inayohamishika ya Kusimamia Masafa

Kiwango cha mfumo kimekuwa kikiongezeka hali inayolazimisha TCRA kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa masafa (*spectrum monitoring system*) unaoambatana na zana bora na za kisasa.

Katika kupitia na kutathmini mahitaji ya ufuatiliaji mfumo wa masafa (Spectrum Monitoring System), nilibaini kwamba TCRA ina mitambo miwili inayohamishika badala ya mitambo sita inavyohitajika ili kukidhi mahitaji ya kanda zote sita za TCRA ambazo ni Zanzibar, Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma. Pia, nilibaini kwamba kati ya mitambo hiyo miwili, moja uliopo Zanzibar una programu ambayo haiendani na program iliyokuwepo sasa ya Scorpion Spectrum Monitoring inayoendeshwa na TCI International Inc kwani ina uwezo wa kwenda hadi GHz 3.

Kukosekana kwa mitambo inayohamishika katika kanda za TCRA mbali na Dar es Salaam kunahatarisha ufuatiliaji wa ufanisi wa matumizi ya masafa. TCRA itashindwa kusimamia mfumo wa masafa marefu mitambo ya masafa katika kanda nne.

Kutokana na umuhimu wa mitambo hiyo, ninashauri kwamba, ni muhimu kufanya tathimini ya mahitaji katika kila kanda ili kuhakikisha idadi ya mitambo inayohitajika inapatikana ili kuongeza ufanisi na ubora katika usimamizi wa masafa.

5.7.2 Kuwepo kwa Makampuni Ambayo Hayajaandikishwa Kwenye Mfumo wa dot (.) tz

Kanuni ya 10 (1) ya Mawasiliano ya Posta na Kielekroniki ya mwaka 2011 inataka chombo chochote cha umma au taasisisi

yoyote ya binafsi iliyosajiliwa Tanzania kujiandikisha na kutumia mfumo wa dot (.) tz.

Mapitio ya mchakato wa usajili kwa mfumo wa .tz tulibaini kwamba, baadhi ya makampuni binafsi bado hayajaanza kutekeleza sheria hii ambapo bado yanatumia mifumo ya kigeni ambavyo inaendeshwa nje ya nchi. Pia, idadi ya makampuni yanayohitaji kubadili mfumo wa nje bado haijajulikana.

Hali hii inaonesha kwamba kuna tatizo kubwa la uratibu kati ya tzNIC na mashirika mengine ya Serikali kama vile BRELA na TRA. Leseni ya biashara zinatolewa na BRELA na taarifa ya mapato ya robo mwaka ya makumpuni yote inawasilishwa na makampuni husika kwa TRA bila ya uthibitisho wa usajili wa mfumo wa dot (.) tz, hivyo, kutokuwa na usalama wa taarifa za Serikali.

TCRA inashauriwa kuanzisha kanzidata ***(database)*** ya kuhakikisha idadi ya taasisi zinazohitajika kubadilisha mifumo ya tovuti zao (website domain) zinatambuliwa na kuhakikisha makampuni ya umma na ya binafsi yanajitokeza kujiandikisha na kuhakikisha TCRA inashirikiana na taasisi nyingine kama tzNIC, BRELA na TRA ili kuhakikisha makampuni yote yanajisajili kwenye mfumo wa .tz.

5.7.3 Kutojulikana kwa Thamani ya Mchango wa Kiufundi

Tanzania Network Information Centre (tzNIC) ilianzishwa mnamo mwaka 2006 na taasisi mbili ambazo ni TCRA na Ushirika wa watoa huduma za intanet **(TISPA)** katika mfumo wa ushirikiano wa umma na sekta binafisi (PPP). Ilianzishwa kama shirika lisilo la biashara lenye lengo na jukumu la kusimamia uendeshaji na usajili kwa mfumo wa dot (.) tz. Katika uanzishwaji wa taasisi hiyo, TCRA ilitakiwa kugharamia uanzishwaji wa tzNIC na TISPA walikuwa na jukumu la utoaji wa msaada wa kiufundi kwa tzNIC.

Hata hivyo, hadi sasa mchango wa kiufundi ulitolewa na TISPA haujathaminiwa ili kujua thamani yake kifedha. Hali hii inaongeza wasiwasi mkubwa juu ya jumla ya mchango wa TISPA katika uendeshaji wa kituo. Hivyo kusababisha kutofahamika kwa usahihi jumla ya thamani michango yote.

Ni maoni yangu kuwa, uthaminishaji wa michango ya wadau wote wawili ni muhimu kwa ajili ya uwazi na kutambua juhudi zinazofanywa na kila mmoja katika kuhakikisha operesheni za tzNIC zinaendeshwa vizuri. Hivyo, nashauri TCRA na TISPA kujadili na kutathmini mchango wa kiufundi unaotolewa na TISPA ili kuwezesha kujua thamani ya michango kwa ujumla.

5.7.4 Kushindwa Kuanzisha Mpango Kazi Unaorahisisha Utekelezaji wa Kujisalili Kwenye dot(.) tz

Baada ya kufanikisha mchakato wa ugawaji mwaka 2010, tzNIC ilipewa mamlaka yote na shirika la kutoa Majina na Namba za Mtandao (Internent Corporation for Assigned Names and Numbers - ICANN) kufanya shughuli zote la kiutawala na za kifundi kwenye mawasaliano ya .tz country code Top Level Domain (ccTLD).

Mapitio ya utaratibu uliotumika kuanzisha tzNIC ulibainisha kwamba hapakuwa na ushahidi kwamba upembuzi yakinifu ulifanyika kabla ya uanzishwaji wa tzNIC. Pia, hapakuwa na mpango kazi (business plan) unaorahisisha ukutekelezaji wa mradi wa tzNIC.

Ukosefu wa mpango kazi na upembuzi yakinifu unaongeza vihatarishi kwenye utekelezaji wa mradi na uwezekano wa kushindwa kufikia malengo. Hali inasababisha kutokidhi malengo ya Serikali na yale ya sekta binafsi kama wadau wakuu wa huduma ya mtandao.

Nawashauri TCRA na TISPA kuandaa mpango wa biashara (business plan) wa kina ambao utasaidia kuboresha operesheni za tzNIC.

5.7.5 Kutokuwa na Ufatiliaji Taarifa za Matumizi ya Intaneti na Muda wa Maongezi

Kanuni ya 4(2)(b)-(d) ya Kanuni za Mawasiliano ya Posta na Kielektroniki (TTMS) ya mwaka 2013 inaitaka TCRA kuwa na kifaa kinachohakiki taarifa za mapato yanayopatikana kutoka kwenye makampuni ya mawasiliano ya simu.

Mapitio ya kazi zinazofanywa na Mifumo (moduli) iliyopo kwenye kifaa maalumu cha kukusanyia taarifa za mawasiliano ya simu (TTMS) yalibainisha kuwa hakuna mfumo (moduli) wenye uwezo wa kutambua na kufuatilia taarifa za matumizi ya intaneti na matumizi ya muda wa maongezi. Katika mahojiano, menejimenti ya TCRA ilijibu kwamba, kimsingi, TTMS ilianzishwa kwa lengo la kufuatilia mawasiliano (telecommunication traffic). Kutokana na ongezeko la mahitaji, kuna uwezekano wa kuboresha kwa kuongeza mifumo zaidi; ambapo, kwa hivi sasa, kuna majadiliano yanayoendelea kati ya TCRA na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kufanikisha jambo hili.

Kutokuwa na uwezo wa kufatilia matumizi ya intanenti na muda wa maongezi kunaongeza wasiwasi juu ya uwezo wa TCRA kuthibitisha matumizi halisi ya intaneti na muda wa maongezi. Hivyo, kuathiri uwezo wa Serikali katika kupata taarifa sahihi kwa ajili ya kukusanya kodi ya mapato inayotokana na uendeshaji wa huduma za mawasilino ya simu.

Naishauri TCRA washirikiane na TRA na BoT ambao ndio walengwa wakuu wa ongezeko la mifumo ya mapato kwenye TTMS kuhakikisha wanafanya hivyo mapema iwezekanavyo ili

kusimamia mapato yanayotokana na matumizi ya intaneti na gharama za matumizi ya muda wa maongezi.

5.7.6 Muingiliano wa Masafa kwa Watumiaji

Mapitio ya ripoti za muingiliano wa masafa kutoka Julai 2015-Juni 2016 kwa ukanda ya TCRA ya Dar es salaam yalibaini kwamba kuna muingiliano wa mawasiliano kati ya masafa au mitandao. Hii ni kinyume na Kanuni 8(1) na 9(1)(a) ya Kanuni za Mawasiliano ya Posta na Kielektroniki (Mawasiliano ya Radio na Masafa ya Mawimbi) ya mwaka 2011.

Pia, nilibaini ukosefu wa mwongozo kwa mtumiaji ambao ungetumika kuongeza ufahamu wa namna bora ya kufanya kazi ndani ya masafa yaliyotolewa; na kwamba, utaratibu pekee unaotumiwa na Mamlaka kufuatilia na kuhakikisha hakuna muingiliano wa mawasiliano ni kufanya ziara kwa wahusika. Hali hii inaongeza uwezekano wa waendeshaji wasiosajiliwa kujiunga na kujitoa mara kwa mara hali inayoongeza ungumu kwa TCRA kuwatambua.

Ni maoni yangu kuwa katika mgawanyo wa masafa, masafa ya redio yapo karibu na masafa ya anga ya ndege. Hivyo, kuna haja ya kupunguza muingiliano ili kuongeza usalama wa matumizi.

Ninashauri TCRA iandae mwongozo wa watumiaji ambao utatumika kama njia ya kuongeza ufahamu wa namna bora ya kufanyia kazi masafa yaliyotolewa. Aidha, mara kwa mara iwakumbushe watumiaji namna bora ya urushaji wa matangazo ndani ya mipaka ya masafa waliyopewa ili kupunguza muingiliano kwatumiaji.

5.7.7 Kukosekana kwa Kanzidata ya Kuhifadhi Matumizi ya Mifumo ya Mawasiliano

Mapitio ya michakato ya usimamizi wa masafa yalibaini kwamba, TCRA haikuwa na kanzidata (database) ya redio call, mifumo vya

usalama kwenye nyumba, na mfumo wa ufatiliaji magari. Hivyo, kufanya kiasi cha mapato yaliyoripotiwa na TCRA kutoendana na hali halisi. Hii ni kwa kuwa Mamlaka inategemea uamuzi binafsi na wa hiari wa makampuni au watu binafsi wenye kumiliki na kutumia mifumo hiyo.

Nilibaini kwamba hapakuwa na ratiba ya mpango wa ukaguzi ambayo ingeweza kuonesha mahali, idadi ya wakaguzi, makampuni husika, muda uliotumika kufanya kazi ya ukaguzi, muda kati ya kaguzi na kaguzi, pamoja na ripoti zilizotolewa kwa shabaha ya kutambua idadi ya mali na sehemu zilizopatiwa huduma hizo.

Hiari ya kutaarifu umiliki unaonyesha udhaifu katika mfumo wa kubaini utambulisho na ufuatiliaji wa redio call, mifumo ya usalama kwenye nyumba na mfumo wa ufuatiliaji kwenye magari. Ukosefu wa kanzidata unasababisha udhaifu katika usimamizi wa mifumo ya mawasiliano; hivyo, kusababishha kuwepo kwa watumiaji wasioandikishwa.

Nawashauri TCRA kuwatambua watumiaji wote wa mifumo ya mawasiliano na kuwaweka katika kanzidata ya pamoja ili kurahisisha shughuli ya usimamizi na ukusanyaji mapato.

5.7.8 Shughuli za Mkongo wa Taifa Kutosimamiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Mamlaka ya Mawasiliano ya Taifa ina jukumu la kusimamia mawasiliano, huduma za utangazaji wa matangazo, mawasiliano ya kielektroniki, huduma za posta na masafa ya taifa. Mkongo wa taifa ni moja ya mifumo ya kielektroniki ya mawasiliano, hivyo, una kila sababu ya kusimamiwa na Mamlaka ya mawasiliano.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa kuna mgogoro wa majukumu kati ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na TCRA. Hii ni kwa

vile, shughuli za mkongo kwa sasa zinaendeshwa na TTCL na Mamlaka kuwa na utaratibu kujiondoa katika majukumu hayo.

Ninaishauri Mamlaka ya Mawasiliano nchini kufanya mazungumzo na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ili kuweza kuweka wazi shughuli, usimamizi na majukumu yake kwenye sekta ya mawasiliano.

5.8 Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda (TIRDO)

5.8.1 Mapungufu katika Utekelezaji wa Mpango Mkakati na Malengo Yalioanishwa katika Mpango Kazi

Tumepitia utaratibu wa uandaaji wa Mpango kazi, bajeti, uandaaji wa mpango mikakati, na utekelezaji wake. Tumebaini mapungufu yafuatayo:

a) Mapungufu katika uandaaji wa mipango kazi

Katika kupitia nyaraka, nimegundua kuwa idara moja kati ya nne haikuandaa mpango kazi wake wa mwaka. Pia, mipango kazi ya idara tatu zilizobaki haikushabihiana na mpango mkakati wa taasisi hasa malengo na rasilimali fedha (bajeti) iliyohitajika kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa.

b) Kutofanyiwa kazi vipaumbele vilivyowekwa katika malengo yaliyomo kwenye mpango mkakati na majukumu ya taasisi;

Mapitio ya mipango kazi ya Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda yanaonesha kuwa shirika halikufanyia kazi vipaumbele vilivyoainishwa katika mpango mkakati wake wa miaka mitano (2011-2016). Shughuli zilitekelezwa pasipo kuonesha vipaumbele na jinsi gani zilitekelezwa. Hatimaye, walishindwa kuweka vigezo vya kupimia utendaji kazi katika mipango yao ya kazi. Hivyo, kusababisha ugumu katika kupima matokeo yaliyotokana na malengo waliyojiwekea.

Mapungufu katika kushabihiana kwa nyaraka za mipango kazi yanaleta ugumu katika kupima mafanikio yaliyofikiwa dhidi ya rasilimali fedha zilizotumika. Hili linazuia taasisi kuweza kujua changamoto walizokutana nazo ili kupanga mipango endelevu.

Menejimenti wa Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda unatakiwa kuhakikisha yafuatayo:

a) Mipango ya utendaji ya Mwaka inashabihiana na vipaumbele na malengo ya taasisi. Pia, mipango inatakiwa kuhusisha vigezo vya upimaji kazi dhidi ya matokeo; na

b) Mpango kazi wa mwaka uoneshe maeneo ya vipaumbele katika utekelezaji shughuli zilizopangwa na kwa muda uliowekwa.

5.8.2 Mapungufu katika Usimamizi na Tathmini ya Ufanisi

Mpango makakati wa Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda wa mwaka 2011-2016 unataka kuwepo kwa mchakato wa kufanya tathmini na ufuatiliaji ili kubaini ni kwa kiasi gani taasisi imeweza kufikia malengo iliyojiwekea. Katika mpango mkakati, kunatakiwa kuwa na tathmini katika ngazi mbili, yaani tathmini ya kila robo ya mwaka na ufuatiliaji ufanyike kila kati kati ya mwaka kwa kutumia mfuatiliaji wa nje.

Tumebaini kuwa tathmini na ufuatiliaji unaofanyika katika shughuli mbalimbali haukujitosheleza ili kufikia malengo yaliyoainishwa katika mpango mkakati.

Tumebaini pia kuwa Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda limefanya ufuatiliaji wa utendaji wa vikao vya kamati tendaji za wafanyakazi kulingana na miradi inayofanyika ambayo ni sehemu ya malengo yake. Hata hivyo, tumebaini kuwa ufuatiliaji huo ulilenga kazi zilizofanyika na si vigezo vya kiutendaji

vilivyowekwa wakati wanaandaa mipango kazi ya taasisi ya mwaka kwa kila lengo.

Menejimenti ya taasisi inashauriwa kuhakikisha kuwa usimamizi, tathmini, na ufuatiliaji vinafanyika ili kuhakikisha inafikia malengo yake kama ilivyopangwa kwenye malengo ya taasisi.

5.8.3 Mapungufu katika Usambazaji na Uendelevu wa Matokeo ya Tafiti

Katika kutekeleza Mpango wa taifa wa ukuzaji wa uchumi na kupunguza umasikini na dira, mpaka mwaka 2025, usambaji wa tekinolojia na matokeo ya tafiti ni nyezo muhimu katika kuharakisha maendeleo ya viwanda na kukuza ujasiriamali na wajasiriamali. Hii ni sababu inayohitaji kuboreshwa kwa Shirika la maendeleo na utafiti wa viwanda.

Katika kuangalia utoaji wa huduma wa Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda kwa taasisi mbalimbali na wadau, tumegundua kuwa kuna mapungufu katika utendaji kazi wa shughuli mbambali za Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda. Hakuna utaratibu mahsusi katika usambazaji na uendelezaji wa tafiti na teknolojia kwa wajasiriamali wadogo, wajasirimari wa kati na wadau wengine.

Katika kuhoji kuhusu kuwepo kwa ushahidi wa usambazaji wa teknolojia na taaluma zilizopo ndani ya Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda kwa wadau muhimu, Mamlaka ilionesha matokeo mbalimbali ya tafiti ambayo yamesambazwa kwa wadau. Teknolojia zilizosambazwa zinajumuisha: uchenjuaji wa mihogo, ukaushaji juani na uchenjuaji wa mabaki ya bidhaa za plastiki na uandaaji wa bidhaa za chakula. Tumebaini kuwa usambazaji wa teknolojia hauko mikononi mwa Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda kwa kuwa hakuna ushahidi wa

uendelevu wake, umiliki wake na hata mfumo wa usambazaji wa teknolojia hizo.

Uongozi wa Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda ulieleza kuwa umekuwa ukitumia maonesho na makongamano ya kibiashara kuueleza umma kuhusu majukumu yake. Hata hivyo, tulibaini kuwa hakukuwa na mikakati ya kimaandishi inayonyesha utaratibu wa kusambaza taarifa au matokeo yaliyotokana na tafiti zilizofanyika.

Uongozi unakosa taarifa kwa ajili ya kufanya maamuzi mbalimbali kwa sababu ya kukosekana na kutofanya uchunguzi ili kubaini matokeo ya tafiti zilizofanywa. Kuna hatari kuwa teknolojia za Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda na mchakato wa usambazaji wake hautakuwa endelevu na stamilihivu kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za baadaye.

Menejimenti ya Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda unashauriwa kufanya yafuatayo:

(i) Kuanzisha mfumo wa kuratibu na kusimamia ufanisi katika usambazaji wa matokeo ya tafiti za viwanda;

(ii) Kuhakikisha kuwa jukumu la usambazaji wa teknolojia ndani ya taasisi unafanyika kwa ufanisi

(iii) Kuangalia uwezekano wa kufanya uchunguzi wa matokeo ya tafiti zilizofanywa ili kupata takwimu ya thamani na athari kwa jamii.

5.9 Chuo Kikuu cha Dar es salaam - Mradi wa Mlimani City

5.9.1 Ucheleweshwaji wa Utekelezaji na Ukamilikaji wa Miradi

Ujenzi wa mradi wa Mlimani City ulianza tarehe 01 Oktoba, 2004 ukikadiriwa kukamilika tarehe 01 Septemba, 2016 au siku yoyote kwa makubaliano ya mkodishwaji na mkodishaji.

Tulibaini kwamba mradi mdogo wa hoteli ya nyota 3 (ambayo ina vyumba 100 kikiwemo chumba cha mikutano kinachochukua watu 1,000) na uboreshaji wa bustani ya botania, ikiwa ni sehemu ya mradi wa Mlimani City, haujakamilika kwa kipindi cha miaka 10 toka tarehe ya makubaliano ya kumaliza mradi.

Ni mtazamo wangu kuwa, hakuna ufatiliaji wa karibu, usimamizi na tathmini ya mkataba huo kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Kwa sababu hiyo, kuna uwezekano wa kushidwa kumalizia kazi iliyobaki kwa sababu ya ongezeko kubwa ya gharama ya kumalizia mradi toka kipindi kilichopangwa kupita.

Menejimenti ya Chuo Kikuu inashauriwa kuuangalia upya mkataba iliongia na Mlimani City Holding kuharakisha umaliziaji wa miradi.

5.9.2 Ukiukwaji wa Ulipaji wa Ada ya Chuo

Kifungu cha 1.1(j) ya mkataba pamoja na kifungu 10.1 ya Hati ya Ukodishaji wa Uwanja Kinaelezea kuwa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam kinapaswa kipate asilimia 10 ya mapato ya kodi ghafi.

Kinyume na kufungu tajwa hapo juu, Mlimani Holding Limited (MHL) hufanya mahesabu ya gawio la kodi ya Chuo Kikuu kwa kuzingatia asilimia kumi ya mapato ya kodi baada ya kutoa gharama za uendeshaji badala ya kujumuisha gharama za uendeshaji. Ukiukwaji huu unakifanya Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam kuwa katika hatari ya kupoteza kiasi kikubwa cha mapato kutoka katika mradi wa Mlimani City.

Tunashauri menejimenti ya chuo kufanya yafuatayo:

(a) Kufanya upya mahesabu ya gawio lake la asilimia 10 kutokana na mkataba na kuomba kulipwa na mpangaji kiasi kilichokuwa kimekosewa.

(b) Kuwasiliana na mpangaji na kufikiria kubadilisha mkataba ili kuweka vifungu ambavyo vitaruhusu idara ya ugakuzi ya

ndani ya chuo kuangalia mapato na gharama za uendeshaji za mradi.

5.9.3 Udhaifu wa Ufatiliaji na Usimamizi wa Mapato kutoka kwa Wapangaji Wadogo

Kifungu cha 11.2(l) cha hati ya makubaliano mpangaji (MHL) anapaswa kutopangisha mtu yoyote ambaye hajathibitishwa na Mpangishaji (Chuu Kikuu cha Dar-es-Salaam). Hii inaweza kutumika kama njia ya kudhibiti mapato yake.

Kinyume na makubaliano ya hapo juu, tumeona kwamba MHL amepangisha majengo kwa wapangaji wengine bila kupata kibali cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kuna mapungufu ya utekelezaji wa vipengele vya mkataba kwa upande wa Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam hivyo, kupelekea Chuo kushindwa kujua kwa usahihi mapato ya kodi kutoka kwa wapangaji wote.

Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam inashauriwa kutekeleza vifungu na vipengele vyote vya hati ya makubaliano ya upangaji kikiwemo kifungu 11.2(l) cha hati ya makubaliano ambacho kinakitaka Chuo Kikkuu cha Dar-es-Salaam kuwathibitisha wapangaji wadogo wadogo.

5.9.4 Kukosekana kwa Haki ya Kujua Kazi Zinazofanywa na MHL

Mapitio ya mkataba wa upangishaji wa ardhi kati ya Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam na Mlimani Holding Limited yamegundua kwamba mkataba haumpi mmiliki wa ardhi, haki ya kukagua kazi zinazofanywa na mpangaji. Katika hali hii, mpangishaji, ambaye ni Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam hawezi kujua endapo mpangaji, Mlimani Holding Limited, anakiuka mkataba katika uendeshaji au kuna baadhi ya wapangaji wa nyumba hawawekwi wazi na mpangaji huyu.

Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam kinashauriwa kuwasiliana na Mlimani Holding Limited ili kupata haki ya kukagua shughuli za miradi kwa manufaa ya pande zote mbili.

5.9.5 Kutobainishwa kwa Hatari Zitakazobaki Kipindi Mkataba Utakapoisha

Hatari zitakazojitokeza pindi mkataba utakapo isha wakati mali zitakapokua zinarudishwa serikalini.

Mapitio ya mkataba yamegundua kuwa mkataba huo hauelezei hali halisi ya ugawanaji mali pindi mkataba utakapoisha (Miaka 50 au 85 kutokana na makubaliano ya pande mbili). Hakuna makubaliano yoyote yanayoelezea mgawanyo wa mali na miondombinu itakayokuwepo wakati mkataba unaisha.

Kwa hali hii, kuna uwezekano wa kutokea kwa mvutano wa kisheria mwisho wa mkataba. Hali hii ikitokea, Chuo Kikuu kitakosa msaada wa kisheria. Uongozi wa Chuo kikuu cha Dar-es-Salaam unashauriwa kuingia katika mazungumzo na Mlimani Holding Limited ili kuweka vifungu vitakavyoonesha haki ya kila upande wakati wa mkataba utakapoisha.

5.9.6 Kutokusanywa kwa Dola za Marekani 57,607 kutoka kampuni ya Mlimani Holding Limited

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (USDM) kiliingia katika makubaliano na kampuni ya Ernest and Young kufanya ukaguzi maalumu ili kujua kiasi cha mapato ambacho chuo kinaidai kampuni ya Mlimani Holding Limited katika kipindi cha tarehe 1 Mei 2006 mpaka tarehe 30 Juni 2014.

Wakati wa ukaguzi niligundua kuwa kiasi cha Dola za Marekani 309,458 kilitakiwa kipokelewe na Chuo kutoka MHL, lakini usuluhisho wa mahesabu ulionesha MHL ililipa Dola za Marekani 213,850 kupitia uhamisho wa benki kwa njia ya kieletroniki na kubakisha Dola za Marekani 57,607.

Kuna ufuatiliaji duni kwa upande wa menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika kukusanya deni hilo. Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inashauriwa kuongeza nguvu katika kufuatilia na kukusanya deni wanalolidai MHL.

5.10 Chuo cha Ufundi Stadi (VETA)

5.10.1 Uendeshaji wa Shughuli za VETA

Mwezi Machi 2002 VETA walianza kutumia mfumo wa ugatuaji wa maamuzi ambapo uendeshaji na maamuzi yalitolewa kwenye Mikoa na Kanda. Hii ilitoa fursa kwa uongozi wa juu kujikita katika mambo-mkakati ya kitaasisi na kisera.

Tathmini yetu ya mfumo huu katika ufanisi, ubora na kiuchumi imegundua mapungufu ambayo yanahitaji kushughulikiwa na menejimenti ya chuo cha ufundi stadi.

(a) Mapungufu ya Uongozi wa Kamati ya Ushauri Katika Vituo

Sheria ya VETA ya mwaka 2004 inahitaji uanzishaji wa kamati ya ushauri katika vituo itakayowajibika na kuhakikisha mafunzo yanayotolewa na Chuo cha Ufundi Stadi yanaenda sambamba na mahitaji ya soko la ajira.

Nimebaini kwamba mikoa ya Manyara na Kagera haijaanzisha kamati za ushauri. Pia nimeona kwamba mikoa mingine ina kamati lakini hazifanyi kazi kama zinavyopaswa; kwani hazijawahi kufanya mkutano wa mwaka wala kufanya majukumu yao toka zilipoanzishwa.

Kutokafanya kazi kwa kamati hizi, kunaonyesha mapungufu ya uongozi wa Chuo cha Ufundi Stadi katika utoaji wa mafunzo.

(b) Utawanyaji Mbaya wa Mali za Chuo cha Ufundi Stadi

Kifungu cha 3(3) cha sheria ya Chuo cha Ufundi Stadi kimeipa uwezo wa kumiliki mali za vituo vya chuo cha ufundi. Nilibaini kuwa kodi za ardhi na matengenezo ya majengo ya chuo katika vituo vya mikoani, wakati usimamizi na umiliki ni wa makao makuu. Katika uendeshaji wa hali hii, kila mkoa utatakiwa ulipie kodi ya ardhi ya kiwanja chake. Tumegundua ofisi za mikoa zimeshindwa kulipa kodi ya ardhi ambayo inatengeneza deni linalokisiwa kuwa Shilingi bilioni moja; na ofisi hizo hazina uwezo wa kifedha wa kulipa kiasi hiki.

Ni maoni yetu kuwa usimamizi wa mali ni jambo ambalo linahitaji kufanywa na makao makuu ya Chuo cha Ufundi Stadi.

(c) Ukosefu wa Utoaji wa Mikataba ya Utekelezaji kwenye Mamlaka za Chini

Aya ya 2.2.1 ya Miongozo na Vyanzo vya Mapato ya ndani ya mwaka 2014 inawataka Mkurugenzi Mkuu, Mkurugenzi wa mkoa, Mkuu wa kituo kusaini mkataba wa utekelezaji unaoanisha malengo, madhumuni na mpango unaopaswa kutekelezwa katika kipindi cha utekelezaji.

Mapitio yangu na mahojiano niliyofanya na wajasiriamali na waratibu wa kozi za muda mfupi nchi nzima, yamegundua kwamba, kwa mwaka huu wa ukaguzi, hapakuwa na mkataba wa utekelezaji uliosaininiwa kati ya Mtendaji mkuu na watendaji wa mikoa wala waratibu wa vituo.

Ukosefu wa mkataba wa utekelezaji unaweza kupelekea Mamlaka kushindwa kufikia malengo ya mwaka.

VETA inashauriwa kutekeleza sheria na taratibu za ndani kama zilivyopangwa.

5.10.2 Usimamizi Usioridhisha wa Shughuli kwa Madaraka za Uzalishaji wa Maduhuli

Miongozo na Shughuli za Uzalishaji wa ndani ya Mamlaka ya Elimu na ufundi stadi (VETA) inataka mikoa na ofisi za vituo kuandaa na kusaini taarifa za usimamizi wa uzalishaji kila mwisho wa robo ya mwaka na mwisho wa mwaka kwa ajili kuidhinisha utendaji wa mradi.

Aya ya 1.3.4 (b) inahitaji pawe na usimamizi wa mfumo katika ngazi za mikoa na Taifa kwa msingi wa kuhakikisha kwamba miongozo inaeleweka vyema na inatekelezwa na wadau wote katika kila robo ya mwaka. Aya 3 inaeleza kwamba Miongozo na Shughuli za Uzalishaji wa ndani ya Mamlaka ya Elimu na ufundi lazima iboreshwe kulingana na muundo wa Mamlaka ya Elimu na ufundi stadi kwa kuanzisha timu ya usimamizi na kutathmini; ambapo MKurugenzi ya Fedha atasimamia na kutathimini utendaji wa miongozo na shughuli za uzalishaji wa ndani ya Mamlaka ya Elimu na ufundi kwenye vituo vyote vya Mamlaka ya Elimu na ufundi sitadi (VETA) kwa ushirikiano na ofisi za kanda husika.

Kinyume na taratibu zilizo elezwa hapo juu nilibainisha yafuatayo:-

(a) Taarifa za robo ya mwaka haziandaliwi nakupelekwa makao makuu kwa ajili ya kutathimiwa;
(b) Idara ya Fedha haina mipango ya kutosha wala taratibu za kusimamia hatari za fedha zinazoweza kujitokeza katika uzalishaji hivyo kuzuia mafanikio katika kazi zilizo kusudiwa.
(c) Hakuna ushahidi wa kuwapo kwa utaratibu wa kusimamia na kupata uhakika kwamba shughuli zilizo pangwa zimefanikiwa kwa ajili ya kubaini muingiliano wa shughuli.

Kutokuwapo kwa mfumo wa usimamizi na kutathmini kunaweza kusababisha udhaifu katika kutathmini na kusimamia kazi zilizopangwa hivyo kusababisha upimaji wa malengo dhidi ya matokeo kutofanikiwa.

Tunashauri Makao makuu ya chuo cha ufundi kuandaa na kutekeleza wa mfumo wa kusimamia, kutathimini na kutoa ripoti katika uzalishwaji wa mapato.

5.10.3 Kuchelewa Katika Kutekeleza na Kufikia Malengo Yaliyowekwa

Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Chuo kilipanga kutekeleza kazi mbalimbali za maendeleo zipatazo 48. Hata hivyo nimebaini kwamba ni kazi tatu (3) tu (sawa na asilimia 6) zilizotekelezwa na hivyo kupelekea kazi zipatazo 42 kutotekelezwa (sawa na asilimia 94).

Pia nilibainisha kazi zilizopangiwa bajeti mwaka uliopita, utekelezaji hafifu wa mpango wa mwaka wa manunuzi, upungufu wa vifaa vya kufundishia na uhitaji wa matengenezo ya miundombinu ya mamlaka.

Kushindwa kutekeleza kazi za maendeleo kunaonyesha kuwa chuo hakitaweza kufikia malengo iliyojipangia.

Menejimenti inaombwa kuweka mikakati ambayo itahakikisha usimamizi na udhibiti wa shughuli zilizopangwa.

5.10.4 Kutokutumika kwa Zana za Mafunzo na Vifaa vya Thamani ya Shilingi Milioni 321

Mnamo mwaka 2012, VETA - Pwani ilipokea vifaa mbalimbali vya mafunzo vyenye thamani ya Shilingi milioni 321 kutoka Korea ya Kusini kwa ajili ya mafunzo mahususi ya ushonaji na kuunganisha vitu. Hata hivyo, zana za mafunzo na vifaa hivyo vimehifadhiwa katika makontena yaliyotumia kusafirishia kwa zaidi ya miaka mitano.

Mipango na usimamizi duni wa vifaa na zana zisizotumika unaweza kusababisha upotevu wa thamani wa mali hizo ambazo zingeweza kutumika ili kufikia malengo ya mafunzo.

Menejimenti inashauriwa kusimika zana na vifaa hivyo vya mafunzo kwa ajili ya mafunzo lengwa ili kuhakikisha inafaidika na malengo ya vifaa hivyo.

5.11 Mamlaka ya Bandari Tanzania

5.11.1 Kupungua kwa ufanisi katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mamlaka ya bandari ilikuwa na Mpango Mkakati wa miaka mitano unaoanzia mwaka 2011/12 mpaka 2015/16. Nimepitia mpango mkakati na kubaini kuwa mamlaka ilikuwa na jumla ya miradi 52 yenye gharama ya dola za kimarekani milioni 2,377 ambayo ilitakiwa kukamilika ndani ya miaka mitano ya Mpango Mkakati. Nimebaini kuwa kati ya miradi 52, 16 haijatekelezwa, 14 ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji na 22 imetekelezwa. Kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi kunaweza kusababisha kutofikiwa kwa malengo yaliyowekwa kwenye Mpango Mkakati.

Mamlaka inashauriwa kuweka juhudi katika utekelezaji wa miradi yote ili kufanikisha malengo yaliyowekwa.

5.11.2 Mapitio ya Makubaliano ya Makusanyo ya Kuhifadhi Mizigo Bandarini

Mamlaka ya Bandari (TPA) iliingia kwenye makubaliano na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yenye lengo la kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya uhifadhi wa mizigo bandarini. Hata hivyo, mapungufu yafuatayo yalibainika:

i. Mapato ya Uhifadhi wa Mizigo Bandarini kutowasilishwa kwenye Akaunti ya Benki ya TPA

Aya E (ii) ya Memoranda ya Makubaliano (MOU) inaitaka TRA baada ya kukusanya mapato ya kuhifadhi mizigo bandarini kuyawasilisha kwenye akaunti ya benki ya Mamlaka ya Bandari ndani ya siku 14.

Hata hivyo, nilibaini kuwa kiasi cha Shilingi bilioni 98.7 kilichokusanywa na TRA kati ya mwezi Agosti hadi Desemba mwaka 2016 hakikuwasilishwa kwenye akaunti ya TPA kama makubaliano yanavyotaka. Jedwali lifuatalo linaonesha mchanganua wa kiasi hicho:

Jedwali Na. 6: Mapato ambayo hayakuwasilishwa kwenye akaunti ya TPA

MWEZI (2016)	BANDARI YA DSM 'Shilingi bilioni	TICTS 'Shilingi bilioni	BANDARI NYINGINEZO (Tanga & Mtwara) 'Shilingi bilioni	JUMLA 'Shilingi bilioni
AGOSTI	6.88	7.61	0.13	14.63
SEPTEMBA	19.19	7.98	0.54	27.71
OCTOBA	14.97	8.12	0.07	23.17
NOVEMBA	18.66	8.37	6.21	33.25
JUMLA	**59.71**	**32.09**	**6.96**	**98.76**

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

ii. TRA Kutokusanya Mapato ya Uhifadhi wa Mizigo kwenye Bandari Nyinginezo

Aya ya 2.1 ya Makubaliano (MoU) inaitaka TRA kukusanya Mapato ya Uhifadhi wa Mizigo katika bandari zote zilizopo nchini, Mapitio yangu ya taarifa mbalimbali yalibaini linafanyika kwenye bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga peke yake; huku likiacha bandari zilizoko Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa ambapo makusanyo yake yameendelea kufanywa na Mamlaka ya Bandari (TPA) kinyume na Memoranda ya Makubalino.

iii. **Kutokuwapo kwa Utaratibu wa Kushughulikia Ongezeko au Punguzo lisilostahili la Gharama za Uhifadhi wa Mizigo**

Aya ya 1.4 ya Makubaliano inataka wahusika wa makubaliano hayo kuandaa utaratibu wa namna ya kushughulikia ongezeko lisilostahili au punguzo lisilostahili la gharama za uhifadhi mizigo bandarini zilizotozwa kwa wateja.

Hata hivyo nilibaini kuwa hakuna utaratibu wa kushughulikia ongezeko aupunguzo la gharama hizo licha ya makubaliano tajwa hapo juu kutaka iwe hivyo.

Nashauri Mamlaka ya Bandari kukubaliana na Mamlaka ya Mapato juu ya namna yakutekeleza majukumu yaliobainishwa kwenye Memoranda ya Makubaliano baina yao ili kuhakikisha kila upande unatekeleza majukumu yake ipasavyo kuisaidia Mamlaka ya Bandari kufikia malengo yake ya kimkakati ya uanzishwaji wake.

5.11.3 Kupungua kwa Ufanisi Katika utendaji wa Mamlaka

Mapitio yangu yalibainisha kwamba, wakati wa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2016 TPA ilikuwa imejiwekea malengo ya kufikiwa ya kuongeza ufanisi wa shughuli zake. Sampuli ya vyombo vya maji viwili vilivyochaguliwa wakati wa mapitio yangu. Nilibaini kwamba mamlaka haikufikia malengo yake iliyojiwekea ya tani 900 kwa kila kundi kwa kila zamu. Kama inavyoonekana kwenye Jedwali nambaa 7 hapa chini:-

Jedwali Na. 7: Ufanisi katika Meli

Jina la chombo cha mali	Tarehe iliyotia nanga	Jumla ya mzigo ulioshushwa	Makundi yaliyotumika	Wastani Tani/genge/zamu	Malengo	Tofauti	Watani wa siku baada ya kutia nanga.
Blue Phoenix	31.10.2015	2,580.18	4	645.05	900	254.95	4
	01.11.2015	3,322.18	6	553.70	900	346.3	
	02.11.2015	3,388.78	6	564.80	900	335.2	
	03.11.2015	1,225.40	4	306.35	900	593.65	
Hilal Bey	05.12.2015	1,324.92	2	662.46	900	237.54	4
	06.12.2015	877.04	1	877.04	900	22.2	
	07.12.2015	1,393.60	2	696.80	900	203.2	
	08.12.2015	777.60	2	388.80	900	511.2	

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

Nilibaini kwamba zoezi la kusubiri malori ya kupakulia mizigo linachukua muda mrefu. Hali hii inasababisha vyombo vya maji kuchelewa kung'oa nanga.

Kuchelewa kwa mawakala wa mizigo kuleta malori ya kupakia mizigo kwa wakati kunaongeza idadi ya siku ambazo meli imetia nanga hivyo, kuathiri ufanisi wa bandari.

Naishauri menejimenti ya TPA kuwasiliana na wateja ili kujenga uelewa na kuwasisitiza wateja kuzingatia ratiba ya muda waliokubaliana kwa ajili ya kuwezesha Mamlaka kutoa huduma ya haraka ya moja kwa moja ili kuboresha utoaji huduma.

5.11.4 Tathmini ya Muda ambao Vyombo vya Maji vinakaa Bandarini

Nilipitia ripoti ya utendaji wa bandari ya Dar es Salaam inayoishia tarehe 30 Juni 2016 ambayo inaonyesha muda ambao

mizigo inakaa bandarini. Ripoti hiyo iliandaliwa kwa madhumuni ya kuangalia muda ambao unaotumika tangu wakati mizigo inashushwa mpaka wakati mzigo unaondoka bandarini. Bandari imejiwekea Muda wa wastani wa siku 5 kwa ajili ya mizigo yoyote kubakia ndani ya jengo au eneo la bandari. Nilibaini kwamba muda ambao mizigo inakaa bandarini ni kati ya siku 6.1 na siku 8.6 kama inavyooneshwa hapa chini:

Jedwali Na. 8: Repoti ya Utendaji Kazi

	Robo ya 1	Robo ya 2	Robo ya 3	Robo ya 4
Wastani wa Siku	6.9	7	8.6	6.1

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

Pia ilibainika kwamba mamlaka ilijiwekea malengo kwamba meli ikae siku 3 tangu inapotia nanga. Hata hivyo, nilibaini kwamba siku ambazo meli inatumia baada ya kutia nanga zilikuwa ni siku 4 wakati muda wa wastani unaochukuliwa kwa meli katika **Single Point Mooring (SPM)** ilikuwa ni kati ya siku 5 hadi 9. Jedwali lifutalo linaonesha muda meli inakaa bandarini:

Jedwali Na. 9: Wastani wa muda unaotumiwa na meli katika Single Point Mooring (SPM)

Jina la chombo	Tarehe ya kutia nanga	Tarehe ya kuondoka	Uzito wa Mzigo	Mzigo	Jumla ya siku iliyokaa
Phoenix Hope	02.8.2015	10.08.2015	95,211.671	Petroli	9
Pacific Sky	19.8.2015	28.8.2015	103,202.305	Petroli	9
Maersk Penguin	2.10.2015	8.10.2015	85,769.974	Petroli	6
Ashley Lady	16.10.2015	23.10.2015	101,626.064	Petroli	7
Shan Hu Zuo	4.3.2016	11.3.2016	68,292.529	Petroli	6
Selin	22.3.2016	28.3.2016	66,799.522	Petroli	5

Pia nilibainisha kuwa wakati mwingine vyombo vya majini vinatumia kati ya siku 3 mpaka 26 vikiwa inasubiri mamlaka iwaonyeshe sehemu ambayo inaweza kutia nanga kwa ajili ya kushusha mizigo yao.

Jedwali Na. 10: Meli zilizokaa kwa muda mrefu zikisubiri gati

Na.	Jina la Meli	Kufika kwa meli kwenye OA and NOR	Kufika kwa meli kwenye gati	Muda wa Kufikia gati	Tarehe ya iliyoondoka	Aina ya Mzigo
1	UACC HARMONY	21.07.2015	31.07.2015	10	04.08.2015	Dizeli
2	BURSA	31.07.2015	05.08.2015	4	09.08.2015	Dizeli
3	MELATI 7	19.08.2015	27.08.2015	8	31.08.2015	Mafuta ya Kula
4	PHOENIX HOPE	30.07.2015	02.08.2015	3	10.08.2015	Petroli
5	IPANEMA STREET	23.09.2015	8.10.2015	16	12.10.2015	Dizeli
6	RIBE MAERSK	27.09.2015	12.10.2015	15	17.10.2015	Mafuta ya Mitambo
7	HIGH LOYALTY	05.10.2015	17.10.2015	12	22.10.2015	Dizeli
8	ALPINE MARINA	02.10.2015	22.10.2015	20	25.10.2015	Petroli
9	BASTILLE STREET	11.02.2016	26.02.2016	15	3.03.2016	Dizeli
10	FAIRCHEM EAGLE	06.02.2016	3.03.2016	26	4.03.2016	Mafuta Ghafi
11	SILVER MONIKA	19.02.2016	9.03.2016	19	14.03.2016	Mafuta ya Kula
12	STI MYTHOS	03.03.2016	14.03.2016	11	19.03.2016	Dizeli
13	ARGO	03.03.2016	15.03.2016	14	17.03.2016	Mafuta Ghafi

Ongezeko la meli kukaa kwa muda mrefu linaweza kuathiri uwezo wa Mamlaka wa kupakua mizigo bandarini. Hii inaweza kupelekea meli kutotumia bandari hii kwa sababu ya mapungufu ya kiufanisi.

Menejiment inashauriwa kuhakikisha kuwa matatizo ya kiufanisi katika utemdaji yanatatuliwa kwa ajili ya kuboresha utendaji wa bandari.

5.11.5 Tathmini ya Uendeshaji wa Vituo vya Mafuta

Mamlaka inaendesha vituo viwili vya mfuta, kimoja kipo Kurasini (Kurasini Oil Jetty (KOJ)) na kingine kipo Kigamboni (Single Point Mooring (SPM)). Kituo cha SPM kinatumika kutoa mafuta machafu na kituo cha KOJ kinatoa mafuta ya vilainishi, petrol, diseli, mafuta ya taa, mafuta mazito na mafuta ya asili. nilibaini yafuatayo:

i. Kiwango Kidogo cha Utoaji wa Mafuta

Ripoti za kila mwezi za Agasti 2015, Oktoba 2015 na Machi 2016 mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2016 kwa kituo cha

Kurasini Oil Jetty (KOJ) and Single Point Mooring (SPM), zinaonyesha kuwa kiwango cha kutoa mafuta katika kituo cha KOJ NI 375 metriki tani kwa saa. Hii inaonyesha kiwango cha kusukuma mafuta kipo chini, hivyo, kusababisha siku za meli kutia nanga kuongezeka.

Ilielezwa kuwa muda wa kusukuma mafuta unategemea sababu nyingi kama vile umbali kutoka kituo kimoja cha mafuta mpaka kingine mpaka kwenye sehemu ya kupokelea, uwezo wa pampu na kipenyo cha bomba la mafuta.

Kiwango kidogo cha utoaji wa mafuta kinaathiri ufanisi wa Mamlaka kuweza kufikia malengo iliyojiwekea kuhudumia meli zilizopo bandarini.

ii. Kutofanya Kazi Kwa Mashine za Kupimia Mafuta (Flow metres)

Kituo cha KOJ kina mashine 16 za kupimia mafuta (Flow miters) 16; na zote hazifanyi kazi kwa muda mrefu. Mapitio ya metriki tani zilizotolewa kutoka katika kituo cha KOJ yalibaini kuwa wastani wa 202,476.76 metriki kwa mwezi (kwa miezi ya Agosti 2015, oktoba 2015 Machi 2016) zilitolewa kupitia kituo cha KOJ bila ya kupitia kwenye mashine za kupimia mafuta kwa sababu hazikuwa zikifanya kazi.

Kutokuwapo kwa mashine za kupimia mafuta kunapelekea kutokuwa na usahihi katika utoaji mafuta yaliyohifadhiwa; hivyo, kupelekea hasara kwa Mamlaka.

Menejimenti inashauriwa:

a. Kujadiliana na serikali ili Mamlaka iweze kutumia hifadhi za matanki ya TIPER ili kupunguza umbali kati ya meli na vituo vya mafuta, hivyo kupunguza siku ambazo meli itakaa na kutia nanga bandalini;

b. Kutekeleza ujenzi wa kituo cha hifadhi ya mafuta kama ilivyopangwa ili kuboresha menejimenti ya mfumo wa uhifadhi mafuta; na
c. Kuhakikisha Mashine za kupimia mafuta zinafungwa katika kituo cha KOJ ili kuwezesha ukusanyaji sahihi wa mapato ya mafuta.

5.11.6 Ukamilifu wa Madeni

Mapitio ya madeni ya watoa huduma ya kibiashara na mengineyo yamebaini kiasi kikubwa cha fedha kuliko kile ambacho kimeakisiwa kwenye vitabu vya hesabu (General Ledger). Kiasi kilichothibitishwa na watoa huduma ni Shilingi bilioni 105.50 wakati kiasi cha fedha kilichoakisiwa kwenye vitabu vikuu vya hesabu ni Shilingi milioni 687.23 hii inafanya tofauti ya Shilingi bilioni 104.81 ikiwa ni kiasi chini ya kiasi halisi ambacho kimeripotiwa na TPA. Pamoja na hayo, menejimenti ya TPA haikuwa ikifanya mara kwa mara usulihishi (reconciliation) kwa taarifa za watoa huduma. Hali hii imesababisha tofauti kubwa kati ya rekodi za watoa huduma na rekodi za TPA.

Ni maoni yangu kuwa, bakaa ya madeni ya kibiashara na madeni mengineyo imekosewa kwa kiasi kikubwa, hivyo haioneshi thamani halisi ya deni.

Menejimenti ya Mamlaka ya Bandari inashauriwa kufanya usuluhishi wa mara kwa mara wa madeni yaliyoakisiwa katika vitabu dhidi ya rekodi za watoa huduma ili kuhakikisha usahihi.

5.11.7 Mali za Kudumu Hazijathaminishwa

Taarifa ya kimahesabu (statement of financial position) imejumuisha mali za kudumu zenye thamani baki (carrying/book value) ya Shilingi bilioni 646 mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2016 ambayo inasabihi mfumo wa uthamini (accounted for using revaluation model).

Kanuni ndogo G ya Kanuni 4.28.2 ya Kanuni za Fedha za TPA inataka uthamini wa mali ufanyike kila baada ya miaka mitano. Hata hivyo, nimebaini kuwa, uthamini wa mwisho ulifanyika tarehe 30 Juni 2008. Mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2016 uthamini wa mali haukuwa umefanyika. Kwa kufuata Kanuni za Fedha za TPA za mwaka 2012, uthamini uliofuata ulotakiwa kufanyika tarehe 30 Juni 2013. Hii inaonyesha kuwa Mamlaka ya Bandari imeshindwa kufuata kanuni zake za fedha hivyo kutokidhi matakwa ya Kiwango cha Hesabu cha Kimataifa namba 16.

Ni maoni yangu kuwa, thamani ya mali haiakisi thamani halisi. Hivyo naishauri menejimenti ya TPA kufanya uthamini wa mali zake zote kwa mujibu wa matakwa ya Kanuni zake za Fedha.

5.11.8 Kutokulipwa Deni la Kodi Shilingi Bilioni 42.88

Mapitio yangu yamebaini nyakati ambazo Mamlaka ya Bandari haikukidhi matakwa ya Sheria na Kanuni za Kodi.

Baada ya kumalizika kwa mwaka, Mamlaka ya Bandari ilipokea taarifa ya ukaguzi wa kodi kutoka Mamlaka ya Kodi Tanzania iliyoonesha kiasi cha kodi ambazo mamlaka inadaiwa (kama vile Kodi Kadri ya Kipato chako - PAYE, Kodi Zuio, Kodi ya Mafunzo na Maendeleo - SDL na Kodi ya Ongezeko la Thamani) kwa miaka miwili ya 2013 na 2014, na haijatambua jumla ya deni la kodi katika vitabu vyake kwa miaka inayoishia tarehe 30 Juni 2015 na 30 Juni 2016 kwa kutumia misingi iliyotumiwa na Mamlaka ya Mapato. Kukosekana kwa taarifa za kuwezesha kujua kiasi cha deni la kodi la miaka ya 2015 na 2016 kunapelekea jumla ya madeni iliyoripotiwa kwenye taarifa za fedha (statement of financial position) kutokuwa sahihi.

Menejimenti ya TPA inahusisha limbikizo la deni la kodi na kushindwa kwa TRA kufuata makubaliano ya utumaji wa forodha

katika akaunti ya TPA. Kutokukidhi matakwa ya sheria na kanuni za kodi kunaweza kusababisha adhabu zinazoweza kuzuilika.

Menejimenti ya TPA inashauriwa kufuata sheria za kodi na kanuni zake. Pia, menejimenti inatakiwa kumaliza mzozo uliojitokeza kati yake na Mamlaka ya Kodi.

5.11.9 Matokeo ya Ukaguzi katika Teknolojia ya Habari na Mifumo ya Udhibiti

Mapitio ya Mifumo ya Teknolojia ya Habari na mifumo ya uhasibu yamebaini matumizi ya mfumo wa hesabu uliopitwa na wakati inayotambulika kwa jina la COBOL na mfumo wa kurekodi kwa mkono. Hii ni kusema kuwa, sehemu kubwa ya shughuli za kibiashara zinafanyika na kurekodiwa kwa mkono (manually) kupitia mfumo uliopitwa na wakati wa COBOL.

Mfumo huu uliopitwa na wakati una mapungufu mengi ikiwemo kukosekana kwa uunganifu na mfumo wa bili na mfumo wa mshahara. Mapungufu yanaongeza uwezekano wa makosa kutokea na taarifa zilizorekodiwa kwenye mfumo kutokuwa sahihi. Taarifa zinazopatikana kwenye mfumo huu huwa zinaingizwa kwa mkono. Hata hivyo, vitabu vidogo ainishi vya hesabu (sub-ledgers) havipatikani katika mfumo ili kutoa taarifa zaidi ya rekodi na kufanya ziaminike, hivyo, kufanya ripoti zinazotokana na mfumo wa hesabu wa COBOL kutoaminika.

Pia, nimebaini kuwa kuna meli 36 zilifika gatini katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na kurekodiwa kwenye mfumo wa Kusimamia shughuli za bandari (Harbour View Plus – HVP) lakini hazikurekodiwa katika mfumo wa bili, hivyo hakuna ankara iliyotolewa kwa meli husika. Pia, hakukuwa na mgawanyo wa majukumu katika mfumo wa bili. Mapungufu haya inawezekana ndiyo yaliyosababisha kutokutolewa kwa ankara kwa meli hizo.

Nashauri kuwa, udhibiti wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na mifumo ya jumla pamoja na ya matumizi ya mifumo (General and application) iboreshwe na Menejimenti ya TPA kuhakikisha meli zote zinzofika gatini zinapatiwa ankara sahihi.

SURA YA SITA

MAPITIO YA UFANISI WA SEKTA YA MADINI NCHINI TANZANIA

6.0 Utangulizi

Sekta ya madini, gesi na mafuta inahusu utafutaji na uchimbaji wa madini, Mafuta na gesi asilia. Nchi ya Tanzania imebarikiwa kuwa na utajiri mkubwa wa madini na gesi, lakini mchango wa sekta kwenye uchumi hauridhishi.

Katika mwaka huu wa fedha nimefanya ukaguzi katika sekta ya uchimbaji wa madini na gesi na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuboresha mchango wa sekta kwenye uchumi.

Ukaguzi wangu umehusisha taasisi zote za Serikali nchini zinazohusika na sekta ya uchimbaji kama vile Wizara ya Nishati na Madini, Wakala wa Jiolojia Tanzania, Wakala wa Ukaguzi Madini Tanzania, Shirika la Taifa la madini, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Kampuni ya STAMIGOLD na Shirika la Mafuta Tanzania.

Hii sura ina sehemu kuu mbili; ya kwanza inajadili tathmini na ushauri wangu kwenye sekta ya madini, na sehemeu ya pili inajadili tathmini na ushauri wangu kwenye sekta ya gesi. Hoja zimeandaliwa na kutengwa kitaasisi.

6.1 Taarifa za Ukaguzi Maalumu Kuhusu Sekta ya Madini

6.1.1 Wizara ya Nishati na Madini

6.1.1.1 Mapungufu katika Mikataba ya uchimbaji Madini

Nilipitia mikataba ya madini iliyoingiwa kati ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania na makampuni ya madini ya: Geita Gold Mining (GGM) inayoendesha mgodi wa dhahabu wa Geita, na Kampuni ya ACACIA inayoendesha migodi ya Buzwagi, Bulyanhulu na Mara Kaskazini.

Mapungufu ya msingi yalionekana katika taratibu zinazotumika kuingia mikataba, na mikataba husika kuwa na vifungu visivyolinda maslahi ya umma. Nimebaini kuwa, katika majadiliano, Serikali inategemea taarifa za uvumbuzi na upembuzi zilizofanywa na makampuni binafsi yanayoomba leseni bila kuwa na njia mbadala ya kuhakiki taarifa hizo; hivyo, kuipunguzia Serikali uwezo wa kutetea maslahi yake.

Pia, mikataba ya madini iliyopitiwa ilibainika kuwa na vifungu visivyolinda maslahi ya umma kama vile masharti yasiyoridhisha katika kuongeza mikataba, vifungu vinavyozuia mabadiliko ya sheria kuathiri mikataba husika, sera zisizoridhisha kwenye fedha za kigeni na forodha, motisha za kodi ziliozidi kwenye taratibu za kihasibu katika kutambua na kutohoa matumizi ya mitaji.

Serikali inashauriwa itumie kifungu kinachoruhusu kurejewa kwa mikataba kinachopatikana kwenye mikataba mingi ya madini (sanctity of fundamental clause) kinachotumika kurejea makubaliano yaliyoafikiwa na kuhakikisha kuwa Serikali peke yake haiwezi kufanya maamuzi yatakayoathiri matakwa ya wawekezaji kwenye madini ili kuyaita makampuni husika na kujadiliana nayo jinsi ya kuboresha maslahi ya pande zote. Vile vile, naishauri Serikali iboreshe usimamizi kwa makapuni binafsi yanayofanya kazi za kutafuta na kuvumbua miamba yenye madini

ili kuiwezesha Serikali kuwa na taarifa sahihi na za ziada zitakazoisaidia kwenye majadiliano na kufanya maamuzi.

6.1.1.2 Changamoto Katika Makusanyo ya Kodi na Mrahaba Kutoka kwa Wachimbaji Wadogo wadogo.

Sheria ya usimamizi wa madini ya mwaka 2010 inahitaji wamiliki wote wa leseni za kuchimba madini kulipia kodi migodi wanayomiliki na kulipa mrahaba kwa kadri ya uzalishaji wa migodi yao. Ukaguzi wangu umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa wachimbaji wadogo hawalipi kodi wala mirahaba. Nimebaini kuwa, kufikia tarehe 30 Juni 2016 kuna malimbikizo ya kodi za leseni za migodi inayofikia shilingi bilioni 9.8 kutoka kwa wachimbaji wadogo. Pia nimebaini kuwa wachimbaji wadogo wengi hawawasilishi taarifa za uzalishaji wao ili waweze kukadiriwa na kulipa mrahaba; na wachache wanaowasilisha. Nimebaini kwamba, changamoto hizo zinasababishwa na ukaguzi hafifu kwenye migodi utokanao na uhaba wa fedha, rasilimali watu na kutoa leseni kwa wachimbaji wasio na mitaji na utaalamu wa kuendeleza maeneo yao.

Ninaishauri Serikali, kupitia Wizara ya Nishati na Madini, kuongeza uwezo wa ofisi za madini kanda kwa kuzipatia fedha za kutosha na wafanyakazi ili ziweze kufanya kaguzi za mara kwa mara kwenye migodi ili kufuatilia wachimbaji wadogo wasiolipa kodi za umiliki wa maeneo ya madini na wasioleta taarifa za uzalishaji ili watozwe mrahaba. Pia, naishauri Serikali iongeze kigezo cha kutathmimi utaalamu na uwezo wa kifedha wa muombaji leseni kabla hajaidhinishwa kupewa leseni.

6.1.2 Wakala wa Jiolojia Tanzania

Wakala wa Jiolojia Tanzania ni taasisi iliyoandaliwa madhubuti na taifa kufanya tafiti za miamba na kushauri Serikali ipasavyo.

Imewezeshwa wataalamu na vifaa stahili ili kufanya kazi yake kwa ufanisi. Kwa sasa, Wakala unafanya kazi zote zinazohusiana na tafiti za miamba isipokuwa utafutaji wa madini (prospecting). Wajibu wa Wakala kufanya au kujihusiha na kazi za utafutaji madini umezuiliwa na Kifungu cha 21 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Katika kutekeleza hiyo sheria, kazi zote za utafutaji wa madini sasa hivi zinafanywa na makampuni binafsi; kisha kuwasilisha taarifa za uvumbuzi wao kwa Wizara ya Nishati na Madini.

Wizara, kwa kutumia taarifa ilizopokea toka kwa makampuni binafsi inatunuku leseni za uchimbaji na uzalishaji madini kwa kampuni hitaji. Ni maoni yangu kuwa, Wizara ya Nishati na Madini haina uwezo wa kufanya tathmini za kina kwenye taarifa zilizowasilishwa na makampuni binafsi kama vile ambavyo Wakala angefanya. Bila usimamizi makini wakati wa utafutaji wa madini, na bila uhakiki wa kina wa taarifa zinazowasilishwa kwa ajili ya kuomba leseni ya uchimbaji, ni mashaka yangu kuwa taifa linakosa misingi thabiti ya kutetea maslahi yake kwenye majadiliano.

Naishauri Serikali ipitie upya sheria ya madini ya mwaka 2010 hususani kifungu kinachozuia Wakala kujihusisha na utafiti wa kugundua madini (prospecting) na kukirekebisha kwa kuuongezea Wakala mamlaka ya kujihusisha na kusimamia tafiti za madini zinazofanywa na makapuni binafsi.

6.1.3 Wakala wa Ukaguzi Madini Tanzania

6.1.3.1 Changamoto Zinazokabili Uchimbaji wa Tanzanite

i. Madhara ya Kupunguza Tozo ya Mrahaba Kwenye Tanzanite.

Serikali kupitia sera ya madini ya mwaka 2009 na taarifa kwa umma No 146 iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 02 Aprili, 2010 ilizuia usafirishaji nje ya nchi wa Tanzanite ghafi chini ya gramu moja. Pamoja na hayo, maboresho stahiki yalifanywa kwenye sheria ya madini ya mwaka 2010 kwenye kifungu cha 87(1)(d).

Serikali kupitia kifungu tajwa hapo juu ilishusha mrahaba kwenye Tanzanite toka asilimia tano ikiuzwa au kusafirishwa ikiwa ghafi mpaka asilimia moja kama ikiuzwa au kusafirishwa baada ya kukatwa na kusafishwa nchini. Jitihada hizi zililenga kuongeza ajira kwa watanzania ili wawaeze kujiajiri kwenye ukataji na usafishaji wa Tanzanite. Pia, kuiongezea Serikali mapato ya mrahaba yatokanayo na kuongezeka kwa bei ya Tanzanite.

Kinyume na matarajio, ukaguzi wangu umebaini ongezeko dogo sana la bei kwenye Tanzanite inayokatwa na kusafishwa nchini hali inayopelekea kupungua sana kwa mapato ya Serikali kwa kuwa tozo lake ni dogo zaidi. Kwa kutumia taarifa za bei ya Tanzanite zilizotolewa na TANSORT mwezi wa saba 2016, bei ya Tanzanite iliyoongezewa thamani ndani ya nchi kwa daraja B na C ilikuwa juu kwa tofauti ndogo sana ikilinganishwa na ile iliyouzwa au kusafirishwa ikiwa ghafi. Isivyotegemewa kwa daraja A bei ya Tanzanite iliyosafirishwa au kuuzwa ikiwa ghafi ilikuwa na bei ya juu zaidi ukilinganisha na iliyokatwa na kusafishwa nchini.

Ukaguzi umebaini kuwa tekinolojia hafifu na uzoefu mdogo wa wataalamu wetu vinafanya kazi yao isifikie viwango vinavyotakiwa na kukubalika kimataifa; hivyo, kufanya thamani isiongezeke kama inavyotarajiwa.

Ni mashaka yangu kuwa thamani ya ajira zinazotengenezwa na shughuli ya kukata na kusafisha Tanzanite hailingani na kiasi ambacho Serikali inapoteza kwa kushusha mrahaba kwenye Tanzanite iliyoongezewa thamani nchini.

Ninaishauri Serikali itathmini dhumuni na malengo yake kwa kufanya tathmini ya faida na hasara zinazoletwa na sera ya kushusha mrahaba kwenye Tanzanite inayoongezewa thamani nchini kwa kuzingatia mustakabali wake kwenye maslahi mapana ya taifa.

ii. **Usafirishaji na Uuzwaji wa Tanzanite kwa Njia za Magendo**

Tanzania ni nchi pekee inayozalisha madini ya Tanzanite ulimwenguni kwa kuwa hayapatikani mahali pengine popote duniani.. Taifa limekuwa halinufaiki inavyotakiwa na utajiri huu kutokana na kukithiri kwa utoroshwaji na uuzwaji wa Tanzanite kwa njia za magendo. Mapitio ya taarifa ya wakala wa ukaguzi wa madini nchini ya kupambana na magendo kwenye Tanzanite yamebaini kuwa kati ya mwaka 2012 hadi 2016 gramu milioni 2.89 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.28 zilikamatwa kwenye viwanja mbalimbali vya ndege katika majaribio ya kutoroshwa nchini.

Majadiliano yangu na menejimenti ya Wakala wa Ukaguzi Madini nchini yalibaini kwamba tatizo la magendo kwenye Tanzanite bado ni kubwa sana. Na upambanaji wake unakuwa mgumu kutokana na uholela wa ulinzi katika eneo la Mererani, kutokuwapo kwa cheti cha asilia kuhalalisha uuzwaji wa Tanzanite, pamoja na doria hafifu kwenye maeneo ya mipaka.

Ninaishauri Serikali kuongeza ulinzi eneo la Mererani ili kupunguza mianya ya kutorosha Tanzanite, Pia, kuboresha mahusiano ya kidiplomasia na nchi zinazouza na kutumia

sana Tanzanite ili zihalalishe matumizi ya cheti cha uasilia (certificate of origin) kwenye kila Tanzanite inayoingia na kuuzwa nchini mwao. Naishauri pia Serikali iongeze uratibu na bajeti kwa taasisi zake zinazohusika na upambanaji kuzuia magendo kwenye Tanzanite.

6.1.4 Shirika la Madini Tanzania (STAMICO)

6.1.4.1 Tathmini ya Ushirikiano wa Kibiashara kati ya STAMICO na Tanzanite One Mining Limited (TML)

STAMICO na TML ziliiingia makubaliano ya ushirikiano wa kibiashara 20 Juni 2013 ili kuendesha pamoja mgodi wa Tanzanite kitalu C Mererani Simanjiro kwa makubaliano ya kwamba kila mmoja atamiliki asilimia hamsini ya hisa zote. Tathmini yangu kwenye ufanisi wa mahusiano hayo ya kibiashara umebaini changamoto zifuatazo:

i. Maamuzi ya Msingi Kutofanywa na Kamati ya Pamoja ya Kuendesha Mgodi

Mkataba wa ushirikiano wa kibiashara kati ya STAMICO na TML unahitaji kuanzishwa kwa kamati ya pamoja ya kuendesha mgodi (Joint Operation Committee). Moja ya kazi kubwa ya Kamati hiyo ni kujadili na kufanya maamuzi yote ya msingi yanayohusu kuendesha mgodi. Ukaguzi wangu ulibaini kwamba kikao cha kwanza cha kamati ya pamoja ya kuendesha mgodi kilifanyika 14 Juni 2015 ikiwa ni miaka miwili tangu mgodi kuanza uzalishaji, baada ya hapo, mapitio niliyofanya kwenye taarifa za vikao vilivyofuata nilibaini kuwa bajeti ya mwaka na manunuzi makubwa yanayofanyika hayajadiliwi kwenye kamati ya pamoja ya kuendesha mgodi. Hii inamaanisha kwamba, STAMICO hawashirikishwi kwenye maamuzi ya msingi ya kuendesha mgodi. Menejimenti ya STAMICO iliniambia udhaifu wa kamati hiyo unatokana na STAMICO kuwa na ushawishi mdogo

katika ubia huo kunakoletwa na kushindwa kuchangia mtaji mara anapotakiwa kufanya hivyo na mshirika wake.

ii. **Kukawia Kuanzishwa kwa Akaunti ya Pamoja ya Benki na Mfuko wa Ukarabati (rehabilitation) wa Mgodi**
Mkataba wa mahusiano ya kibiashara unataka ifunguliwe na itumike akaunti ya pamoja ya benki itakayohitaji ruhusa kutoka pande zote mbili ili kuidhinisha malipo. Hivyo, kuipa mamlaka kamati ya pamoja ya uendeshaji wa mgodi. Vile vile, makubaliano hayo yalihitaji kuanzishwa kwa mfuko wa ukarabati wa mazingira ya mgodi ili kusaidia kusawazisha mazingira pindi shughuli za mgodi zitapomalizika. Mapato ya mfuko huu yalipangwa kuwa asilimia moja ya mapato ghafi ya mgodi. Nimebaini kuwa akaunti zote mbili zimefunguliwa tarehe 30 Octoba 2016 ikiwa ni miaka mitatu tangu mradi uanze kazi. Hata hivyo mpaka wakati wa ukaguzi huu, Machi 2017 akaunti zilizofunguliwa zilikuwa hazijaanza kutumika wala hazijawekwa chochote.

iii. **Kutofanyika kwa Biashara ya Grafiti (graphite) na Marble**
Mkataba wa ushirikiano wa kibiashara unasema kwamba kutachimbwa, kuchakatwa na kuuzwa graphite, Marble na Tanzanite. Kwa sasa, graphite na Marble zinachimbwa pamoja na Tanzanite; isipokuwa zenyewe hazichakatwi na kuuzwa.

Ninaishauri Serikali iongeze mtaji STAMICO ili iweze kuongeza ushawishi kwenye miradi yake. Vile vile, ninaishauri STAMICO iongeze umakini katika kusimamia maslahi ya umma kwenye mikataba ya ushirikiano wa kibiashara.

iv. **Shughuli ya Uongezaji Thamani Tanzanite kwa Kampuni ya Nje kufanywa na Kampuni Endeshaji**

Kipengele 15.1(b-d) cha makubaliano ya ubia kati ya kampuni ya TML na STAMICO yanataka Tanzanite itakayochimbwa isafishwe na kukatwa na kampuni tofauti na inayoendesha mgodi. Ili kutimiza masharti hayo ya mkataba, STAMICO na TML waliajiri kampuni ya Urafiki Gemstone EPZ kwa mkataba wa miaka mitatu kuanzia 12 Desemba 2013 ili ifanye kazi za kukata, kusafisha na kutafuta masoko ya Tanzanite. STAMICO na TML walikubaliana watailipa kampuni ya Urafiki Gemstone EPZ gharama isiyozidi asilimia tano ya mauzo watayofanya.

Ukaguzi wangu umebaini kuwa tangu kusainiwa kwa mkataba na kampuni ya Urafiki Gemstone EPZ mnamo 12 Desemba 2013 hakuna kazi iliyofanywa na hii kampuni mpaka mkataba wake ulipomalizika Desemba 2016. Kipindi chote cha mkataba mpaka sasa uongezaji thamani na uuzaji wa Tanzanite umekuwa ukifanywa na kampuni ya TML ambayo inaendesha mgodi kinyume na makubaliano ya ubia. Uongozi wa TML ulitufahamisha kuwa kampuni ya Urafiki gemstone EPZ haikupewa kazi kwa sababu haikuwa na ujuzi wala utaalamu wa kutosha kufikia viwango vinavyohitajika kimataifa.

Ni mtazamo wangu kuwa makubaliano ya ubia yanakiukwa. Vilevile, uongezaji thamani na mauzo kufanywa na kampuni inayoendesha mgodi kunaweka mashaka kwenye uwazi wa mchakato na usahihi wa taarifa za mauzo

Ninaishauri kampuni ya STAMICO kutumia vyema kamati ya pamoja ya uendeshaji mgodi kuhakikisha shughuli za uongezaji thamani na masoko zinafanywa na kampuni yenye weledi tofauti na inayoendesha mgodi ili kuhakikisha maslahi ya pande zote yanalindwa.

v. **Mauzo ya Tanzanite kati ya Kampuni endeshaji na Kampuni tanzu**

Kampuni ya Sky Associates ilinunua hisa za umiliki wa kampuni ya TML inayoendesha mgodi wa Tanzanite toka kwa kampuni ya Richland Resources tarehe 30 Januari 2015.

Ukaguzi wangu wa mauzo ya Tanzanite kwa mwaka 2015 ulibaini mauzo ya karati 230,953 zenye thamani ya dola za kimarekani milioni 1.75 kuuzwa kwa kampuni ya Sky Associates ambayo ni Kampuni mama ya TML. Kwa kuzingatia mahusiano ya muuzaji na mnunuzi, ninapata mashaka na ushindani wa bei iliyotumika.

Pia, nimebaini kuwa TML inatafuta masoko na kuuza Tanzanite bila kupata ukubali wa mshirika wake STAMICO ambayo ni kinyume na kifungu cha 15.1(b-d) cha makubaliano ya ubia kati ya STAMICO na TML.

Ninaishauri Wizara ya Nishati na Madini, kupitia STAMICO, ihakikishe mauzo ya Tanzanite yanafanyika kwa uwazi mkubwa kupitia minada ya hadhara ili kuondoa nafasi zozote za kuuzwa kwa bei isiyo ya ushindani kati ya kampuni ndugu.

6.1.4.2 Mapitio ya Uendeshaji wa Mgodi wa Dhahabu wa Buckreef na Mkataba wa Ushirikiano Kati ya STAMICO na Tanzam 2000

Shirika la Madini Tanzania (STAMICO) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani hapa Tanzania (TANZAM 2000) waliingia makubaliano mwaka 2011 ya ushirikiano wa kibiashara kuendesha mgodi wa dhahabu wa Buckreef uliopo Geita kwa mgawanyo wa hisa asilimia hamsini na tano (55%) kwa kampuni ya TANZAM na asilimilia arobaini na tano (45%) kwa STAMICO. Nimepitia mkataba wa ushirikiano na uendeshaji wa mgodi na kubaini changamoto zifuatazo:-

i. **Uuzaji wa Mgodi na Mgawanyo wa Hisa Bila Vigezo**

Ukaguzi wangu umebaini kuwa TANZAM 2000 waliiilipa STAMICO kiasi cha dola za marekani 3,000,000 kama gaharama za ununuzi wa umiliki wa mgodi kwa asilimia hamsini na tano. Uongozi wa TANZAM 2000's ulinieleza kwamba thamani hiyo ilitokana na kiasi cha fedha kilichowekwa mnada (bid) na kampuni tanzu ya TANZAM 2000. Aidha, STAMICO haijatoa majibu yanayoridhisha wala kuthibitisha majibu ya TANZAM 2000. Ni mashaka yangu kuwa bila kufanyika kwa uthaminishaji mali wa kina ili kufahamu gharama halisi ya mradi, Serikali itakuwa inauza miradi yake chini ya thamani halisi.

Serikali, kupitia STAMICO, inashauriwa kuhakikisha kuwa bei ya ununuzi ya migodi ya madini inayokubaliwa kwenye mikataba ya ushirikiano wa kibiashara sharti itokane na upembuzi wa kina, uthaminishaji wa mali au makadirio ya madini yaliyopo ardhini.

ii. Kuchelewa Kuanza kwa Shughuli za Uchimbaji Mgodini

Nimebaini kuwa tokea kusainiwa kwa mkataba wa ushirikiano wa kibiashara mwaka 2011 mpaka wakati wa ukaguzi wangu mgodini mwezi Machi 2017, uchimbaji rasmi ulikuwa bado haujaanza. Majadiliano kati yangu na uongozi wa TANZAM 2000 yamebaini kuwa kuchelewa huko kumesababishwa na kushindwa kwa zoezi la majaribio ya kuchakata madini kwa njia ya mchujo toka kwenye mirundikano ya vifusi (heap leeching) iliyogharimu kampuni kiasi cha shilingi bilioni 2.3 pamoja na uvamizi unaofanywa na wenyeji/wazawa katika maeneo ya mgodi.

Mahojiano kati yangu na uongozi wa STAMICO pamoja na mapitio ya taarifa za fedha za TANZAM 2000 yalibaini vikwazo vya ukwasi kwa mwendeshaji kuchangia uchelewaji huo. Kufuatia uchelewaji huu, STAMICO walishitaki walipwe

fidia na TANZAM 2000; lakini shauri lilipingwa kwa hoja ya kwamba uchelewaji umesababishwa na wavamizi; na kwamba jambo hilo lipo nje ya uwezo wa muwekezaji. Hivyo ikaoenkana kana kwamba miradi hiyo ilichelewa kutokana majanga ya asili.

Serikali, kupitia STAMICO na Wizara ya Nishati na Madini, inashauriwa kufanya tathmini ya uwezo wa kifedha wa TANZAM 2000's wa kuendesha mgodi na kuhakikisha uchimbaji wa madini unaanza mapema iwezekanavyo.

6.1.4.3 Tathmini ya Uendeshaji Mgodi wa STAMIGOLD - Biharamulo

Serikali, kupitia STAMICO, ilichukua mgodi wa dhahabu wa Tulawaka kutoka kwa kampuni ya Pangea Minerals Ltd. Mkataba wa kuhamisha umiliki ulifikiwa tarehe 15 Novemba, 2013 na jina la mgodi likabadilika toka mgodi wa Tulawaka kwenda mgodi wa Biharamulo. Ili kuendesha mgodi, STAMICO iliunda kampuni mpya kwa jina la STAMIGOLD. Tathmini yangu ya ufanisi wa mgodi chini ya usimamizi wa kampuni ya STAMIGOLD ni kama ifuatavyo:

i. Wizara ya Nishati na Madini Kuchelewesha Ruhusa ya Leseni Kubwa ya Uchimbaji Madini kwenda STAMIGOLD

Kifungu cha 9(2) cha Sheria ya Madini ya 2010 kinahitaji kuwepo kwa kibali cha maandishi kutoka Wizara ya Nishati na Madini kabla umilikishwaji wa leseni kubwa ya kuchimba madini haijaamishwa kutoka kwa kampuni moja kwenda nyingine. Mapitio yangu yalibaini kuwa baada ya STAMIGOLD kuchukua mgodi walihitaji pia kurithi mkataba uliokuwepo awali kati ya Pangea Minerals Ltd na Serikali ili nao waweze kupata faida na motisha alizokuwa anapata muendesha mgodi wa kabla yake. Hata hivyo pamoja na kufatilia Wizarani na kuandika barua za kukumbushia, lakini bado kibali hakijatolewa.

Ni maoni yangu kuwa kuchelewesha kutoa kibali cha kuhamisha leseni ni kuwanyima haki STAMIGOLD kutumia fursa kama vile misamaha ya kodi zinazopatikana kwenye mkataba waliorithi kutoka African Barrick Ltd kuna athiri utendaji wa Kampuni hii ya Umma ukilinganisha na manufaa wanayopata makampuni binafsi.

Ninaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini iharakishe mchakato wa kuipatia STAMIGOLD kibali cha kutumia mkataba wa kuchimba madini aliokuwa anautumia Pangea Minerals Ltd.

ii. Leseni ambazo hazijaendelezwa muda mrefu

Nilibaini kuwa kampuni ya STAMIGOLD ina leseni 11 za utafutaji madini zilizotolewa kati ya 2007 hadi 2014. Leseni hizi zinahusisha leseni moja kubwa ya utafutaji madini. Kati ya leseni zote 11, ni moja tu yenye namba PL9548/2014 ya eneo lililopo Lyobahika ndio utafutaji madini unaendelea; nyingine zote bado. Mapitio ya mpango mkakati wa STAMIGOLD inaonyesha leseni ndogo tatu PL 9548/2014, PL 9549/2014 na 9578/2014 na moja kubwa SML 157/2003 ndiyo zipo kwenye mpango wa kuendelezwa, Hii inamaanisha zilizosalia hakuna matarajio ya kuendelezwa katika kipindi cha karibuni.

Majadiliano na menejimenti ya STAMIGOLD yamedhihirisha kuwa tatizo limesababishwa na uhaba wa fedha. Ni maoni yangu kuwa kuchelea kundeleza leseni hizi ni kuinyima Serikali mapato ambayo yangeweza kupatikana kama leseni hizi zingaliendelezwa.

Ninaishauri Serikali kuongeza mtaji wa STAMICO na STAMIGOLD na kuboresha menejimenti zake ili ziweze kuendeleza leseni zilizo chini yake.

iii. **Mgodi Kutopatiwa Umeme na TANESCO**

Mapitio yangu ya kutathmini ufanisi wa shughuli za mgodi ulibaini kuwa umeme unaotumika mgodini unazalishwa kwa kutumia majenereta. Taarifa ya kila mwezi ya uendeshaji mgodi inaonyesha kuwa mahitaji ya umeme kwa mwezi mgodini ni takriban kilowati milioni 1.1 ambazo zinazalishwa na lita 300,000 za mafuta ya dizeli ambayo inagaharimu takriban shilingi milioni 670. Uchambuzi uliofanywa na STAMIGOLD unaonyesha kuwa hizo kilowati zinazohitajika kama zikipatikana kutoka TANESCO, gharama zake ni takribani shilingi milioni 273.79 (gharama ikihusisha tozo zote zilizopo kwenye umeme kama VAT (18%) REA (3%) na EWURA (1%)

Kwa kutumia umeme wa TANESCO, STAMIGOLD itaokoa karibia nusu ya gharama inazoingia sasa kuzalisha umeme wa mafuta. Ni mtazamo wangu kwamba kupungua kwa gharama hizi kutakuwa na mchango chanya kwenye faida ya kampuni na mapato kwa taifa. Naishauri Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, unganishe mgodi wa STAMIGOLD kwenye gridi ya taifa ili kuupunguzia gharama za kujiendesha; na hivyo, kuuongezea fursa ya kupata faida zaidi.

iv. **Fedha ya Ukarabati wa Mazingira ya Mgodi Dola za Kimarekani Milioni 3.22 Kutopelekwa STAMIGOLD**

Kifungu 7.2 cha mkataba wa kuhamisha umiliki wa mgodi kinataka kampuni ya Pangea kuhamisha fedha za mfuko wa kukarabati na kurejesha mazingira katika hali yake ya awali. Uhamishiwe kwenye kampuni ya STAMIGOLD pale ambapo Pangea atakuwa anakabidhi mgodi kwa STAMIGOLD.

Mapitio yangu ya taratibu za kufunga mradi nilibaini kiasi cha shilingi milioni 19.98 kilikuwa kimetengwa kwa ajili ya kukarabati mazingira ya mgodi. Lakini katika hali isiyotarjiwa

kampuni ya Pangea iliweka bayana Dola za Kimarekani Milioni 16.76 baada ya makato yaliyoidhinishwa kimkataba ya Dola za Kimarekani Milioni 5.13. Kiasi kamili kilichoamishwa na kupokelewa na STAMICO kilikuwa Dola za Kimarekani Milioni 11.63.

Mashaka yangu yamo katika kiasi kilichosalia cha Dola za Kimarekani Milioni 3.22 kati ya kiasi kilichokuwa kimetengwa cha Dola za Kimarekani Milioni 19.98 na kiasi kilichowekwa bayana kwa mgawanyo Dola za Kimarekani Milioni 16.76. Ninaishauri Serikali, kupitia Wizara ya Nishati na Madini na STAMICO, kufanya ufatiliaji wa kina kuhakiksha kiasi kilichosalia kinalipwa.

6.1.4.4 Tathmini ya Uendeshaji wa Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira

Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira kwa sasa unamilikiwa na Serikali kupitia STAMICO. Kabla ya mwaka 2005, mgodi huu ulikuwa chini ya usimamizi wa STAMICO. Lakini kufuatia sera ya ubinafsishaji katika mwaka tajwa, asilimia sabini (70%) za umiliki wa mgodi huu zilihamishiwa kwenda kwa kampuni iitwayo 'Tan Power Resources Ltd'. Kisha, ikachukuliwa na Serikali kupitia Msajili wa Hazina mwaka 2008 na umiliki wa mgodi huu ukarudishwa chini ya STAMICO mwaka 2014. Nilitembelea Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira na kujiridhisha kuwa mgodi huu haujaanza tena kuchimba makaa ya mawe tokea ulipochukuliwa na Serikali. Mapitio yangu katika kuleta ufanisi wa uendeshaji wa mgodi huu yamebaini changamoto zifuatazo:

i. Vikwazo vya Kisheria katika Uendelezaji wa Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira

Mapitio yangu yamebaini kuwa cheti cha hisa cha Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira (KCML) bado hakijahamishiwa STAMIGOLD; na bado kinasomeka jina la Tan power Resources Ltd. Hali hii imesababishwa na kitendo cha

Mamlaka ya Mapato Tanzania kutotoa hati ya kuthibitisha ulipaji wa kodi (tax clearance certificate) kwa kampuni ya Tan power Resources. Vilevile, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kwa mujibu wa kifungu 18(2)(b) cha Kanuni za Ukaguzi na Tathmini ya Athari za Mazingira (the Environmental Impact Assessment and Audit Regulations) 2005, waliikataa taarifa ya Tathmini ya Athari za Mazinigra ya STAMICO (Environmental Impact Assessment (EIA) report kwa sababu hati ya hisa za kapuni hii ilikuwa bado inasomeka kwa jina Tan Power Resources Ltd.

Ni mtazamo wangu kuwa kukosekana kwa hati ya umiliki yenye jina la STAMICO inakwamisha juhudi za shirika kuendeleza mgodi na pia inawia vigumu shirika kuingia ubia na wawekezaji wengine.

Serikali, kupitia ofisi ya Msajili wa Hazina na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), inashauriwa kuingilia kati suala hilo kuhakikisha hati ya kutodaiwa inapatikana na hati ya hisa inatolewa kwa jina la STAMICO.

ii. **Changamoto za Kiutendaji Zinazoukabili Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira**

Ukaguzi wangu umebaini kuwa toka mgodi huu uhamishwe STAMICO mwaka 2014, hakuna fedha za maendeleo zimewahi kupelekwa. Suala hili limesababisha kushindwa kuanza kuzalisha. Vilevile, nimebaini kuwa hadi kufikia Juni 2016, TANESCO inaidai Kampuni ya Kiwira deni la muda mrefu kiasi cha shilingi bilioni 1.8; ili hali wafanyakazi wanaidai kampuni shilingi bilioni moja.

Serikali inashauriwa kutafuta suluhu ya changamoto zilizobainika ili kuzitatua kabla ya kuanza uzalishaji.

6.1.5 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

6.1.5.1 Kutoza Kodi kwa Kiwango cha Sifuri katika Kusafirisha Bidhaa za Madini Nje ya Nchi

Mapitio ya malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutoka kwenye migodi mikubwa minne (4) ya dhahabu Geita, Bulyanhulu, Mara Kaskazini, Pangea na mmoja wa Almasi wa Williamson kwa kipindi cha kati ya Mwaka 2012 mpaka 2016 yalibaini kuwa kulikuwa na marejesho makubwa ya kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiasi cha shilingi bilioni 1,144.

Marejesho hayo makubwa yametokana na mianya inayotolewa na kifungu 55(1) cha sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya mwaka 2014, sawia na sheria za zamani, ambazo, zote kwa pamoja ziliruhusu na bado zinaruhusu tozo ya kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha sifuri kwa bidhaa zinazosafirishwa kuuzwa nje ya nchi. Kwa kuwa soko kubwa la madini na vito liko nje ya nchi, madini yote yanayopatikana yanauzwa nje ya nchi na kupelekea kodi inayotokana na manunuzi (input tax) ya bidhaa za mtaji, mafuta na gharama nyingine yanayofanywa na makampuni ya migodi ndani ya nchi kuzidi ile inayotokana na mauzo (Output Tax). Hivyo, migodi hiyo kustahili marejesho ya kiasi kilichozidi kutokana na kifungu cha 83(2) cha sheria ya Kodi ya ongezeko la Thamani ya mwaka 2014.

Lengo la Serikali kutoza kodi ya ongezekeo la thamani kwa kiwango cha sifuri kwenye bidhaa zote zinazosafirishwa kuuzwa nje ya nchi ilikuwa ni kukuza viwanda vya ndani, mapungufu yaliyojitokeza ni kuwa Sheria hiyo haikuweka makundi kuonyesha ni bidhaa zipi zinazostahili motisha hiyo. Hivyo basi madini ambayo kwa namna yoyote lazima yauzwe nje ya nchi nayo pia yananufaika na motisha hiyo kama vile ambavyo bidhaa za kilimo na viwandani zinavyonufaika.

Serikali inashauriwa kupitia upya sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwak 2014 na kufanya marekebisho ili kuondoa tozo ya kiwango cha sifuri kwenye mauzo ya madini na vito nje ya nchi. Pia kujadiliana na makampuni ya uchimbaji madini kuhusu matokeo ya mabadiliko hayo kwenye Mikataba yao (MDAs).

6.1.5.2 Makampuni ya Madini Kutengeneza Hasara kwa Muda Mrefu

Mapitio ya taarifa za fedha na taarifa za malipo ya kodi za migodi ya dhahabu ya Bulyanhulu, Mara Kaskazini, Pangea pamoja na mgodi wa Almasi wa Williamson kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2012 mpaka 2016 yameonesha kuwa Serikali imekuwa ikipata hasara mfululizo. Hasara hiyo, kwa kiasi kikubwa, imesababishwa na kuruhusiwa kupunguza kiasi chote cha gharama zitokanazo na manunuzi ya bidhaa za mtaji (capital expenditure) kutoka kwenye mapato ya uzalishaji kwa mwaka husika.

Mikataba mingi ya madini inaruhusu kupunguza gharama za manunuzi ya bidhaa za mtaji (capital expenditure) kwa asilimia 80 hadi 100 katika mwaka ambao bidhaa imenunuliwa kuanzia hatua za utafiti mpaka uzalishaji. Hatua hii hupelekea kupata hasara mfululizo. Jedwali la hapa chini linaonesha baadhi ya makampuni makubwa ya madini yanavyopata hasara mfululizo kwa kipindi cha kati ya mwaka 2011 mpaka 2015.

Jedwali Na. 11: Mchangauo wa jinsi makampuni makubwa ya uchimbaji madini Tanzania yanavyopata Hasara

Mwaka wa Fedha	Geita Gold Mine 'Shilingi bilioni	Bulyanhulu Gold Mines Ltd 'Shilingi bilioni	Pangea Minerals Ltd 'Shilingi bilioni	North Mara Gold Mine 'Shilingi bilioni	Williamson Diamond Ltd 'Shilingi bilioni
2015	107.02	(2,362.36)	(959.03)	(101.35)	(135.54)
2014	77.75	(2,047.71)	(727.47)	(234.35)	(106.56)
2013	33.77	(1,349.19)	(785.83)	(317.25)	(188.34)
2012	219.17	(182.95)	(8.21)	75.91	(107.51)
2011	41.62	(579.32)	(196.47)	29.35	-
	479.34	**(6,521.53)**	**(2,677.02)**	**(547.69)**	**(537.95)**

Chanzo: TRA

Serikali inashauriwa kujadiliana na makampuni ya madini yanayopata hasara mfululizo ili Serikali iweze kutoza kodi kwa kiwango cha asilimia 0.3 ya mapato ghafi kama aya ya 3(3) ya Jedwali la kwanza la sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 (toleo la 2015).

6.1.5.3 Kuendelea Kutoza Kodi kwa Kiwango cha Chini Ikilinganishwa na Viwango Vinavyotozwa Sasa

Mikataba ya uchimbaji madini kati ya Serikali na makampuni ya uchimbaji katika migodi ya dhahabu ya Mara Kaskazini, Geita, Buzwagi na Bulyanhulu ilisainiwa kabla Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 haijatungwa, isipokuwa mkataba wa uchimbaji wa mgodi wa dhahabu wa Buzwagi uliosainiwa 2007. Viwango vya tozo za kodi katika mikataba hiyo vilitokana na sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 1973 na havijabadilishwa kuendana na sheria mpya ya mwaka 2004 kutokana na kuwapo kwa kwa kifungu kinachozuia mabadiliko ya viwango vya tozo za kodi kwenye mikataba hiyo. Kwa mfano, mikataba hiyo inaainisha viwango vya zuio la kodi katika ada ya usimamizi pamoja na huduma za kiufundi kati ya asilimia 3 mpaka 5. Hii ni tofauti na asilimia 15 kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004. Mikataba hiyo pia inataka ushuru wa halamashauri ulipwe kwa kiwango kisichozidi Dola za Kimarekani 200,000 kwa mwaka. Hii ni kinyume na kifungu cha 6 (1) (u) cha sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 inayotaka ushuru wa ndani ulipwe kwa kiwango cha asilimia 0.3 ya mauzo ya mwaka.

Serikali inashauriwa kujadiliana na makampuni ya uchimbaji madini kupitia kifungu cha utakaso wa mkataba kinachopatikana kwenye mikataba tarkibani yote ili kurekebisha viwango vya tozo za kodi kwa kuzingatia vigezo vya kiuchumi vinavyobadilika kufatana na muda tangu kusainiwa kwa mikataba hiyo.

6.1.5.4 Misamaha Kwenye Tozo na Ushuru wa Mafuta

Misamaha kwenye tozo na ushuru wa mafuta ilitolewa kwa makampuni ya madini ili kuyapunguzia gharama za uzalishaji umeme kwa ajili ya kuendeshea mitambo. Kifungu cha 8 cha Sheria ya Tozo za Ushuru wa Mafuta na Barabara ya mwaka 1985 kinampa waziri wa fedha mamlaka ya kutoa msamaha wa tozo ya ushuru wa mafuta kwa kutangaza kwenye gazeti la Serikali. Waziri, kupitia gazeti la Serikali Namba 190 lililochapishwa tarehe 15 Julai 2011, alitoa msamaha wa tozo ya ushuru wa mafuta kwenye mafuta yanayoagizwa au kununuliwa na makampuni makubwa ya madini yanoyojihusisha na uchimbaji wa dhabu nchini. Toleo hilo pia lilibatilisha matoleo yote yaliyowahi kutolewa awali kuhusiu misamaha ya kodi; na likaweka utaratibu wa kutumiwa na makampuni husika ili kuweza kupata msamaha huo. Tathmini yangu kwa makampuni makubwa manne ya Geita Gold Mine, Bulyanhulu, Buzwagi na Mara Kaskazini yanayojihusisha na uchimbaji wa dhahabu nchini imebaini kuwa kiasi cha shilingi bilioni 126.7 kama tozo za ushuru wa ndani na mafuta zilisamehewa kati ya mwaka 2015 na 2016.

Ninaishauri Serikali, kupitia Wizara ya Nishati na Madini na Shirika la Umeme Nchini, kuhakisha inapeleka umeme kwenye migodi mikubwa nchini ili kuiondolea Serikali sababu za kusamehe kodi kwenye mafuta, Vile vile, itasaidia kuongeza mapato kwenye Serikali yatayotokana na kuuza umeme kwenye makampuni hayo.

6.2 Taarifa za Ukaguzi Maalumu Kuhusu Sekta ya Mafuta na Gesi

6.2.1 Mapitio ya Mradi wa Bomba la Usafirishaji Gesi Asilia Kati ya Mtwara na Dar es Salaam

6.2.1.1 Ujenzi wa Bomba la Gesi kabla ya Kubaini Wateja

Bomba la kusafirisha Gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam lilijengwa na Kampuni ya China Petroleum and Technology Development Company (CPTDC) kwa gharama ya Dola za Kimarekani bilioni 1.283 ambapo kati ya hizo, dola za Kimarekani bilioni 1.225 zilipatikana kama mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Exim ya China. Marejesho ya mkopo huo yalitegemea kupatikana kwenye mauzo ya gesi asilia baada ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa bomba na kuanza kutumika kibiashara.

Mapitio ya mkataba wa mikopo, mkataba wa mauziano ya gesi asilia, na mkataba wa ujenzi wa bomba yamebaini kwamba, bomba la gesi lilijengwa kabla ya kutafuta wateja na kusainiana mkataba wa mauziano ya gesi asilia kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na wateja lengwa wa gesi asilia. Mapungufu haya yanaathiri malipo ya mkopo kwa vile mauzo halisi ya gesi asilia yatakuwa chini ya kiwango cha makadirio ya awali cha futi za ujazo milioni 138.8 kwa siku (mmscfd).

Pamoja na hayo, kwa sasa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ndilo mteja pekee wa gesi asilia; ambapo anatumia wastani wa futi za ujazo milioni 46.61 kwa siku. Hii ni tofauti na makubaliano ya awali ambayo ilikua TANESCO liweze kutumia takribani futi za ujazo milioni 80 kwa siku kama ilivyokuwa kwenye makubaliano ya mkataba wa mauziano ya gesi asilia (GA).

Hata hivyo, mradi huu ulijaribiwa kwa matumizi kwa kutumia kiwango cha wastani wa futi za ujazo milioni 46.61 kwa siku ikiwa ni kiwango cha chini sana ukilinganisha na ukubwa (capacity) halisi wa bomba. Hivyo, TPDC itawajibika endapo itatokea hitilafu yoyote itakayotokana na majaribio ya upitishwaji wa gesi asili kufanyika chini ya kiwango cha bomba la gesi hilo. Hii ni kwa sababu kipindi cha uangalizi wa bomba

(defect liability period) kwa sehemu kubwa kilishakwisha tangu mwezi Agosti mwaka 2016.

Napendekeza jitihada zaidi ziongezwe katika kuhakikisha wateja zaidi wa gesi asilia wanapatikana ili mkopo uweze kulipwa kabla ya marekebisho ya ulipaji ambayo yataongeza gharama kubwa kwa Serikali.

6.2.1.2 Matumizi ya Bomba la Gesi Asilia Chini ya Kiwango kwa Asilimia 94

Bomba la kusafirishia gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es salaam lilijengwa ili kuwezesha usafirishaji wa gesi asilia kwa ajili ya matumizi ya kuzalisha umeme, viwandani, kwa ajili ya kupikia majumbani na kwa matumizi ya kwenye magari.

Kwenye mapitio yangu niligundua kuwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ndilo mteja pekee aliyeunganishwa kwenye bomba la gesi asilia toka Mtwara. Na, zinatumika wastani wa futi za ujazo milioni 46.61 kwa siku sawa na asilimia sita (6%) tu ya ujazo wa bomba; ambapo, kiasi hicho ni pungufu futi za ujazo milioni 737.39 kwa siku ili kujaza bomba. Hii ni tofauti na mkataba wa mauziano ya gesi asilia kati ya TPDC na TANESCO kuweka wazi kwamba TANESCO itatumia gesi asilia kwenye mitambo yake sita (6) ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi I, Kinyerezi II, Ubungo I,Ubungo II, Tegeta na Symbion kwa kima cha chini cha matumizi cha futi za ujazo milioni 80 kwa siku na futi za ujazo milioni 138.8 kwa siku kama kiwango cha juu.

Hata hivyo, hadi sasa mtambo wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi I ndio pekee unaotumia gesi asilia kuzalisha umeme; na unatumia kiwango asilimia thelathini na nne (34%) ya kiasi cha gesi yote iliyolengwa kutumiwa na TANESCO.

Mitambo mingine mitano iliyokuwa imekadiriwa kutumia kiasi cha futi za ujazo milioni 92.19 kwa siku, sawa na asilimi sitini na sita

(66%) bado haijaanza kutumika; na haijulikani ni lini mitambo hiyo itaanza kutumia gesi asilia.

TANESCO bado lina mikataba ya muda mrefu na wazalishaji wakubwa wa umeme ambao ni kampuni ya Independent Power Tanzania Ltd (IPTL) na Songas; ambapo mikataba yao inaisha mwaka 2022 kwa ule wa IPTL na mwaka 2023 kwa Songas. Hii inaiongezea TPDC na TANESCO ugumu kwenye kutimiza vifungu walivyokubaliana kwenye mkataba wa mauziano gesi asilia (GA).

Ninashauri TPDC iwasiliane na TANESCO na Wizara ya Nishati na Madini ili wajadiliane ni kwa namna gani mitambo ya uzalishaji umeme ya TANESCO itaweza kumalizika kwa wakati ili bomba la gesi litumike kwa ufanisi na kuweza kulipa mkopo wa bomba la gesi kutoka Benki ya Exim ya China kwa wakati. Wakati huo huo, nguvu zaidi zielekezwe kwenye kutafuta wateja zaidi wa gesi asilia ili kuongeza mapato ya gesi na kuiwezesha TPDC kutimiza wajibu wa kulipa madeni inapostahili.

6.2.1.3 Wateja wa Gesi Asilia Kulipa Bei Inayofanana ilihali wapo Umbali Tofauti

Bei ya gesi ina makundi manne; ambapo, bei ya kisimani na tozo ya kuchakata na kusafirisha gesi hazibadiliki ila tu kwa makubaliano maalumu ya kimkataba au majadiliano na makampuni yanayozalisha gesi na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati (EWURA). Tozo ya usambazaji na masoko na gharama nyingine zinategemea na hali halisi ya soko.

Kwenye mapitio ya bei ya gesi nimegundua ya kwamba TPDC inatoza bei ya gesi kwa kiwango cha dola za Kimarekani 5.14/mmBTU kwa wateja wote bila kujali umbali kutoka kwenye chanzo cha gesi. Hii inamaanisha kwamba wateja waliopo mikoa ya Lindi na Mtwara wanalipia bei ya gesi asili inayolingana na wateja waliopo Dar es Salaam.

Ni mtazamo wangu kwamba kutoza bei ya gesi inayolingana kwa wateja wa gesi asilia waliopo Dar es Salaam na waliopo jirani na chanzo cha gesi katika mikoa ya Mtwara na Lindi sio njia sahihi ya kuhamasisha upatikanaji zaidi wa wateja.

Ninashauri TPDC kuandaa rasimu ya bei ya gesi itakayotofautisha bei za gesi zitakazokuwa zikilipwa na wateja mbalimbali kulingana na umbali kutoka kwenye chanzo cha gesi. Rasimu hiyo ipelekwe EWURA kwa uthibitisho ili kutoa fursa kwa wateja wengine waweze kuanza kutumia gesi asilia tofauti na TANESCO.

6.2.1.4 Kutokulipwa kwa Ankara za Mauzo Gesi Asilia kutoka TANESCO Kwenda TPDC kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni 61.35

Mnamo 31 Oktoba 2013, TPDC na TANESCO walisainiana mkataba; ambapo, TPDC alitakiwa kuuza gesi asilia kwa TANESCO. Pia, walikubaliana kwamba Serikali iweke dhamana benki kiasi kinachoweza kulipa mauzo ya gesi kwa miezi mitatu au zaidi kwa ajili ya TPDC huku dhamana hiyo ikitakiwa kuwapo hadi pale madeni yote ya TANESCO yanayohusiana na kuuziana gesi asilia yatakapolipwa.

Kinyume na makubaliano hayo, Serikali haijaweza kuweka dhamana hiyo. Hadi mwezi Desemba 2016, jumla ya deni la mauzo ya gesi asilia kiasi cha dola za kimarekani milioni 61.35, sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 133.4, kilikuwa kimelimbikizwa bila kulipwa na TANESCO.

Hali ya TANESCO kuchelewa kuilipa TPDC, inasababisha TPDC kuchelewa kuyalipa makampuni yanazouza gesi. Hivyo kuongeza hali ya sintofahamu kwenye ulipaji wa mkopo kutoka benki ya Exim ya China. Kuchelewa huku kwa malipo kunaweza kusababisha gharama zaidi za riba ambayo itatakiwa kulipwa na TPDC kwa wadai wake.

Ni mtazamo wangu kwamba, TPDC iandae mpango wa kufanya malipo kwa wauzaji wa gesi na mkopo kutoka Benki ya Exim ya China ili kuepuka kulipa riba kubwa hapo baadaye.

6.2.1.5 Kipengele cha mkataba wa mkopo kisichoridhisha

Tathmini ya mkataba wa makubaliano ya mkopo wa dola za Kimarekani bilioni 1.225 kati ya Serikali kama mkopaji mkuu na Benki ya EXIM ya China kama mkopeshaji kwa ajili ya ujenzi wa bomba la gesi na kituo cha uchakataji wa gesi imebaini kuwa Ibara ya 8 inaondoa kinga juu ya mali za Serikali, isipokuwa mali za kijeshi na kidiplomasia, iwapo kutakuwa na mgogoro wa kibiashara ambao utatakiwa kutatuliwa kimahakama isipokuwa kwa mali zote zilizo zuiliwa kuondolewa kisheria kabla ya makubaliano.

Ni maoni yangu kwamba, kifungu hiki kitaleta athari kubwa katika swala la fedha na uchumi wa nchi iwapo nchi itakabiliwa na mgogoro wa kibiashara utakaohitaji kutatuliwa kimahakama kutokana na utekelezaji wa mkataba huu.

Ninashauri Serikali kupitia upya vipengele vya mkataba na kufanya marekebisho ya mkataba huu. Pia, iandae sera itakayotoa muongozo wa namna dhamana za Serikali zinavyotakiwa kuwekwa kwa kuhakikisha uhakiki wa dhamana ambayo itatakiwa kuwa sawa na jumla ya mkopo na riba yake badala ya kuweka mali nyingi za nchi.

6.2.1.6 Tofauti ya Bei ya Gesi kwa Wauzaji wa Gesi kwa TANESCO

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa bei ya gesi inayotozwa kwa TANESCO na TPDC ni dola za Kimarekani 5.14/mmBTU wakati ile inayotozwa na PanAfrican Energy Tanzania Limited (PAET) kwa TANESCO ni dola za Kimarekani 3.5/mmBTU hivyo kuna tofauti ya kiasi cha dola za Kimarekani1.64/mmBTU kati ya bei ya TPDC na PAET kwa TANESCO.

Kutoza bei kubwa kuliko mshindani wako kunaweza kuathiri upatikanaji wa wateja. Hali hiyo inawezakusababisha kushuka kwa mapato, hivyo, kusababisha ucheleweshaji wa malipo ya mkopo.

Ninashauri TPDC kutathmini bei ya gesi na kupata hitimisho la jinsi bei ya gesi itakavyotozwa kulingana na soko na iwasilishwe kwa mamlaka husika kwa ajili ya kuidhinisha. Aidha, TPDC inatakiwa kufanya utafiti juu ya kile kinachotokea katika sekta ya gesi na kujitathmini juu ya uwezekano wa ulipaji wa mkopo kulingana na masharti ya mkataba ya sasa na kupata suluhisho na kuishauri bodi yake na Serikali.

6.2.1.7 Mapungufu ya Mfumo wa Usalama Katika Kituo cha Kinyerezi

Ukaguzi wa Uhakiki wa mradi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salam uliofanyika kuanzia tarehe 8 Februari, 2017 ulibaini kuwa hakuna eneo lilioachwa wazi (buffer zone) ili kutenganisha kituo cha kupokelea gesi cha Kinyerezi na makazi ya watu. Aidha, nilibaini pia kuwa hakuna mwangalizi ambaye kazi yake moja kwa moja ni kuangalia na kufuatilia matukio yanayotokea kwenye kamera za kielectroniki (CCTV), licha ya kuwepo waangalizi kadhaa ambao walikua wakifuatilia mwenendo wa kinachojiri kwenye bomba la gesi.
Zaidi ya hayo, sikuweza kumtambua mmiliki halali wa eneo la kituo cha kupokelea gesi asilia cha Kinyerezi kwa kuwa hakuna hati miliki iliyowasilishwa kwangu kwa ajili ya ukaguzi.

Mapungufu haya yanaweza kusababisha athari mbalimbali ya usalama katika kituo cha kupokelea gesi cha Kinyerezi. Mathalani, kuvamiwa kwa kituo. Nashauri TPDC iboreshe mfumo wa usalama kwa kuhakikisha unajengwa ukuta mrefu na eneo la wazi kati ya kituo na makazi ya watu. Pia, kuhakikisha kuwapo kwa mtu katika chumba cha udhibiti wa CCTV wakati wote; pamoja na kuwepo kwa walinzi katika eneo la kituo.

6.2.1.8 Mikataba ya Uuzaji wa Gesi yenye Kipengele cha Serikali Kulipia Gesi hata kama Haijatumia Gesi hiyo (Risks surrounding take or pay obligations)

Nilibaini kuwa mkataba wa mauziano wa gesi baina ya TPDC na makampuni ya M&P na Ndovu Resources Limited unataka baada ya tarehe ya kuanza biashara (commercial operations date), kila mwaka TPDC inunue kiwango cha gesi ambacho hakitakiwi kupungua asilimia 85 ya kiwango cha gesi kilichokubaliwa kwenye mkataba kwa mwaka huo.

Hata hivyo, hadi ukaguzi unafanyika tarehe halisi ya kuanza biashara ilikuwa haijaafikiwa kama inavyotakiwa na kifungu namba 6.4 cha mkataba wa mauziano ya gesi baina ya TPDC na M&P na kifungu namba 7.5 cha mkataba wa mauziano ya gesi baina ya TPDC na Ndovu Resources Limited.

Kulingana na matumizi ya sasa ya gesi, TANESCO ndilo mteja mkuu wa TPDC, ikitokea tarehe ya kuanza baishara imeafikiwa kwa hali iliyopo sasa Serikali itapata hasara.

Ni maoni yangu kuwa kabla ya kukubaliana tarehe halisi ya kuanza biashara, TPDC inahitaji kujitathimini kama inaweza kununua gesi kwa kiwango kilichokubaliwa kwenye mkataba bila kuathiriwa na gharama zinazoweza kuongezeka kutokana na masharti ya sasa ya mkataba.

Nashauri uongozi wa TPDC ufanye majadiliano na makampuni ya M&P na Ndovu Resource Limited ili kuhakikisha mabadiliko ya vifungu vya mikataba ya mauziano ya gesi vinabadirishwa ili kuondoa ulazima wa TPDC kuwalipa wauzaji wa gesi hata kwa gesi ambayo haikununuliwa na TPDC katika kipindi husika.

6.2.1.9 Mgogoro Usio na Ufumbuzi wa Bei ya Mabaki Yaliyotokana na Uzalishaji wa Gesi (Condensate)

Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC), kama muuzaji, liliingia mkataba na kampuni ya Kilimanjaro Oil Company Limited kama mnunuaji wa mabaki yaliyotokana na uzalishaji wa gesi (condensate) kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu hadi Januari 2017 kwa bei ya bila kodi ya ongezeko la thamani ya dola za kimarekani 310 kwa tani.

Hata hivyo, kabla mkataba huo haujafika mwisho, mnamo mwezi Februari mwaka 2016 mgogoro wa bei uliibuka baada ya kampuni ya Kilimanjaro Oil Company kuomba bei inayotozwa ipunguzwe kwa asilimia 35. Malalamiko hayo yaliwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama msuluhishi wa mgogoro kwa mujibu wa mkataba. Jambo hilo hadi leo hii halijapatiwa ufumbuzi kiasi cha kusababisha mlundikano wa mabaki hayo. Hivyo kuilazimu TPDC mnamo mwezi Juni 2016 kuingia mkataba na Kampuni ya Kimataifa ya Uhifadhi wa Petroli (TIPER) kwa gharama ya dola za Kimarekani 6.38 kwa kila mita ya ujazo kwa mwezi. Kwa sasa, tenki lenye ukubwa wa mita za ujazo 2,205 linalomilikiwa na TIPER limeshajaa; na TPDC ilikuwa inafikiria kupata tenki jingine ili kuepukana na mlundikano wa mabaki hayo. Kwa sasa TPDC inapata mabaki ya tani 600 kwa miezi mitatu.

Ni maoni yangu kuwa, gharama za uhifadhi kuanzia mwezi Juni hadi Desemba 2016 (USD 6.38 X 2205 X 6= USD 84,407) haikuwa sehemu ya makubaliano baina ya TPDC na kampuni ya Kilimanjaro Oil Company Limited; hivyo, kuongeza gharama za TPDC ambazo zinaweza zisilipike hata kama mteja mpya atapatikana.

Nashauri TPDC lifuatilie ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha muafaka unapatikana. Kwa upande mwingine, TPDC iongeze nguvu katika kuhakikisha mnunuzi au wanunuzi wapya

wanapatikana kwa wakati ili kuondokana na gharama za kuhifadhi mabaki hayo.

6.2.2 Mapitio ya Ulinganishi Kati ya PSA na MPSA na Utekelezaji na Makubaliano Katika Ibara za PSA.

A. Ulinganishi Kati ya Ibara za PSA na MPSA

6.2.2.1 Gharama Kubwa za Viwango Zitakazorejeshwa Kwenye PSA kuliko zilizopendekezwa kwenye MPSA

Marejesho yaliyopendekezwa katika ibara 9(b) ya mfano wa mkataba wa makubaliano ya uzalishaji wa gesi (MPSA) ya mwaka 1995 ni 60%; ibara 11(a) ya MPSA ya mwaka 2004 ni 70% na ibara 11(c) ya MPSA ya mwaka 2008 ni 50%. Asilimia za marejesho zilizokubaliwa kwenye mkataba wa makubaliano ya uzalishaji wa gesi (PSA) husika ni 75% kwa kampuni ya Pan African Energy Tanzania (Songosongo), 72.5% kwa Ophir (Kitalu No.4), 60% kwa Dodsal (Ruvu), na 60% kwa Heritage Rukwa (Bonde la Rukwa) na 60% kwa Heritage Rukwa (Bonde la Kyela).

Tathimini yangu ya mikataba mitano ya uzalishaji wa pamoja wa mafuta na gesi (PSA)imebaini kuwa asilimia za marejesho zilizokubaliwa kwenye PSA husika zinatofautiana na zilizopendekezwa kwenye MPSA kwa 2.5% kwa Ophir (Kitalu 4), 10% kwa Heritage Rukwa (Bonde la Rukwa na Kyela) na Dodsal (Ruvu), na 15% kwa Pan African Energy Tanzania (Songosongo).

Ni maoni yangu kuwa gharama zinazorejeshwa kwa wakandarasi zisipo jadiliwa vizuri zitapunguza faida ya gesi itakayopatikana kwa ajili kugawana baina ya wakandarasi na TPDC,na hivyo, kupunguza mapato ya Serikali.

Hivyo, naishauri Serikali kuongeza nguvu katika majadiliano ya mikataba na kuhakikisha mfano ya PSA inafuatwa kwa manufaa ya Serikali.

6.2.2.2 Kupungua Kwa Gawio la Faida kwa Serikali kadri Uzalishaji Unavyoongezeka

Ibara ya 9(g) ya mfano wa mkataba wa makubaliano ya uzalishaji wa gesi (MPSA) ya mwaka 1995 inaelezea kuwa mgawo wa mapato kwa Serikali utakuwa ukiongezeka kulingana na ongezeko la uzalishaji wa kila siku.

Hata hivyo, makubaliano ya mgawanyo wa uzalishaji (PSA) kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, TPDC na Pan-African Energy Tanzania Limited (PAET) yamekuwa kinyume ambapo gawio la Serikali hupungua wakati uzalishaji unaongezeka, kama ilivyoelezwa kwenye jedwali hapo chini:-

Jedwali Na. 12: Faida Kulingana na PSA Iliyokubaliwa baina ya Serikali na PAET

Wastani wa Mauzo kwa siku		**Ongezeko la mauzo kwa Gesi iliyoongezwa**	**Gawio la Faida ya mauzo ya gesi lililokubaliwa (%)**	
Mita za ujazo Millioni kwa siku (mmcfd)		**Mita za Ujazo Billion (BCF)**	**TPDC**	**PAET**
0 hadi 20		0 to 125	75	25
Zaidi ya 20 ila pungufu kuliko au sawa na 30	**OR**	Zaidi ya 125 ila pungufu kuliko au sawa na 250	70	30
Zaidi ya 30 ila pungufu kuliko au sawa na 40		Zaidi ya 250 ila pungufu kuliko au sawa na 375	65	35
Zaidi ya 40 ila pungufu kuliko au sawa na 50		Zaidi ya 375 ila pungufu kuliko au sawa na 500	60	40
Zaidi ya 50		Zaidi ya 500	45	55

Napendekeza kufanyika upya kwa makubaliano ya mgawanyo wa uzalishaji (PSA) ili kuiwezesha Serikali kunufaika zaidi pindi uzalishaji unapoongezeka.

6.2.2.3 PSA Sita Ambazo TPDC ina Ushiriki Mdogo wa Maslahi

Ibara ya 9(b) (i) ya MPSA 2008 inaitaka TPDC inapoona inafaa ichangie ushiriki usiopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya gharama zote zilizo kwenye makubaliano ukiachana na gharama zilizotumika kwenye utafutaji wa gesi.

Tathmini yangu ya mikataba 6 ya makubaliano ya uzalishaji wa gesi (PSA), imeonyesha kuwa, PSA tatu ambazo ni Swala Oil and Gas TZ Limited (Kilosa Kilombero), Petrobras(Kitalu 8) na Ndovu Resources Limited (Nyuni) zilikubaliana ushiriki wa maslahi kwa TPDC kuwa ni 15%, 20% na 20% kwa mfuatano huo. Mikataba miwili ambayo ni Heritage Rukwa inayofanya utafiti wa gesi Bonde la Rukwa na Heritage Rukwa (Bonde la Kyela) hazikuonyesha ushiriki wa maslahi wa TPDC. Wakati ushiriki wa maslahi wa TPDC kwa Motherland Industry Ltd walipatiwa kufanya utafiti Bonde la Malagarasi walikubaliana kuwa angalau iwe 20%.

Ni maoni yangu kuwa, ushiriki mdogo wa maslahi wa TPDC unapunguza mgawo wa faida kwa Serikali katika mradi na hupunguza uwazi wa utendaji kazi wa mradi.

Napendekeza Ushiriki wa Maslahi wa TPDC kwenye mikataba ya makubaliano ya uzalishaji wa gesi ili uongezwe kufikia asilimia ambazo zilioneshwa kwenye MPSA.

6.2.2.4 Malipo ya Mrabaha na kodi ya ziada kwa Serikali

i. Kiwango Kidogo cha Malipo ya Mrahaba Ukilinganisha na Kiwango Kilichopendekezwa Kwenye MPSA

Tathmini yangu ya mikataba mitatu ya ushirikiano wa uzalishaji wa gesi iliyosainiwa kwa kutumia mfano wa mkataba wa ushirikiano wa uzalishaji wa gesi (MPSA) ya mwaka 1995 na 2008 ambayo ni Beach Petroleum(T) Ltd inayofanya utafutaji wa gesi kwenye ziwa Tanganyika yenye kiwango cha mrabaha cha 5%, Petrobas Tanzania LTD

inayofanya utafutaji wa gesi katika kitalu namba 8 yenye kiwango cha mrahaba wa 5%, na Pan African Energy Tanzania Ltd inayofanya uchimbaji katika eneo la Songosongo ambayo haina kiwango cha mrabaha. Kiwango cha asilimia kilichokubaliwa kwenye mikataba ya makampuni ya Beach Petroleum (T) LTD na Petrobras Tanzania LTD zinatofautiana na kiwango cha 12.5% kilichopendekezwa kwenye mkataba wa mfanano wa ushirikiano wa uchimbaji gesi (MPSA) ya mwaka 2008.

Ni maoni yangu kuwa, kutoza kiwango kidogo cha mrabaha ni kuinyima Serikali mapato inayostahili. Hivyo, napendekeza Serikali kuimarisha timu zake zinazoshiriki katika majadiliano ya mikataba ili kulinda maslahi ya taifa.

ii. Kukosekana kwa Kifungu cha Kutozwa Kodi ya Ziada Katika Mikataba Sita ya Ushirikiano ya Uchimbaji Gesi

Tathmini yangu inaonesha kuwa mikataba wa ushirikiano wa uchimbaji gesi (PSA) ya makampuni sita ambayo ni Swala Oil and Gas Tz Limited (Eneo la Kilosa), Mother Land Industry Ltd (Bonde la Malagarasi), Heritage Rukwa (Bonde la Kyela na Bonde la Rukwa), Petrobras (kitalu namba 8), Ndovu Resources Ltd (Eneo la Nyuni) yote imesainiwa kulingana na mkataba wa mfanano wa ushirikiano wa uchimbaji gesi (MPSA) ya mwaka 2008. Na walahazijaweka kifungu kinachohitaji kutozwa kwa kodi ya ziada ambayo ni kwa mujibu wa ibara ya 15 ya MPSA ya mwaka 2008.

Pia,nilibaini kuwa kifungu cha 13.1(a) cha Ibara ya XIII ya mkataba wa ushirikiano wa uchimbaji gesi ya eneo la Songosongo kinaitaka PAET kulipa kodi ya ziada ya faida

(Additional Profit Tax) ambayo inatakiwa kulipwa kulingana na mkataba kila mwaka na itategemea faida halisi inayopatikana kutokana na mzunguko wa fedha kwenye mkataba husika.

Sambamba na hayo, nilibaini PAET haijawahi kuwasilisha ripoti ya kodi ya ziada ya faida (statements of additional profit tax report) licha ya kutakiwa kulipa kodi hiyo.

Pia, Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004 haikuwa na kipengele cha kodi la Ongezeko la Faida.

Ni maoni yangu kwamba, kukosekana kwa kifungu cha kutozwa kodi ya ziada kunasababisha Serikali kukosa kodi kutoka kwenye chanzo hiki cha mapato.

Napendekeza Serikali kupitia upya makubaliano ya mikataba na kufanya marekebisho ili iweke vifungu vinavyohusika na kutozwa kwa kodi ya ziada. Pia, Sheria ya Kodi ya Mapato inatakiwa ibadilishwe ili ijumuishe tozo la kodi ya ziada. TPDC ifuatilie kuhusu kodi ya Ongezeko la Faida kwa upande wa PAET ili kuhakikisha Serikali inapata mapato yake stahiki

6.2.2.5 Mikataba 18 Inayotoa Haki kwa Wawekezaji Kumiliki Mali Zinazohamishika Ambazo Gharama Yake Inafidiwa

Tathmini yangu imegundua kuwa jumla ya mikataba 18 ya ushirikiano wa uchimbaji gesi (PSA) imewapa haki wawekezaji kumiliki mali zinazohamishika licha ya kuwa gharama za kununua mali hizo zimehusishwa kwenye gharama ambazo zitafidiwa katika mkataba husika wa ushirikiano wa uchimbaji gesi. Mikataba hiyo ilisainiwa kwa kutumia mfano wa mkataba wa ushirikiano wa uchimbaji gesi (MPSA) ya mwaka 1995, 2004 na 2008.

Orodha ya mikataba hiyo ya ushirikiano wa uchimbaji gesi na maeneo yake husika kwenye mabano ni Maurel & Prom (Bigwa), Pan Africa Energy Tanzania Ltd (Songosongo), Petrodel (Kimbiji), Dodsal (Ruvu), Ndovu resources (Bonde la Ruvuma), Petrodel (Tanga), Ophir (Kitalu namba 4), Petrobras (Kitalu namba 6), Ophir (Kitalu namba 1), Statoil (Kitalu namba 2), Swala Oil and Gas TZ Limited (Kilosa Kilombero), Swala Oil and Gas TZ Limited (Pangani), Mother land Industry Ltd (Bonde la Malagarasi), Beach Petroleum Tz Ltd (Ziwa Tanganyika), Heritage Rukwa (Bonde la Kyela), Heritage Rukwa (Bonde la Rukwa), Petrobras (Kitalu namba 8), na Ndovu Resources Ltd (Eneo la Nyuni).

Kuwapa haki wawekezaji kumiliki mali hizo kulingana na mikataba ya ushirikiano wa uchimbaji gesi husika kunainyimahaki TPDC kumiliki mali hizo ikizingatiwa kuwa tayari zimefidiwa.

Napendekeza Serikali kuangalia uwezekano wa kuboresha makubaliano yaliyopo kwa lengo la kuhakikisha mali zinazohamishika ambazo gharama zake tayari zimefidiwa kumilikiwa na Serikali.

B. **Mapitio ya Mkataba wa Songosongo Kama Vifungu vya Mkataba Vilizingatiwa.**

6.2.2.6 Kutokuanzishwa Kwa Mfuko wa Urejeshaji wa Eneo la Uchimaji Katika Hali ya Awali.

Nimegundua kuwa ya mkataba wa mashirikiano ya uchimbaji gesi baina ya TPDC na PAET kuwapo kwa zaidi ya miaka 16 iliyopita,hadi leo taasisi hizo mbili bado hazijaanzisha mfuko maalumu kwa ajili ya kutelekeza na kurejesha eneo la uchimbaji wa gesi asilia la Songosongo katika hali ya awali huku ikiwa imebaki miaka 9 tu kabla ya mkataba huo kufika kikomo mnamo tarehe 10 Oktoba, 2025.

Ni maoni yangu kwamba, jukumu la kurejesha eneo katika hali ya awali baada ya muda wa mkataba wa ushirikiano wa uchimbaji gesi kumalizika litabakia kwa Serikali. Hivyo,napendekeza wahusika wa mkataba huu kuanzisha mfuko huo ili kuepusha Serikali kuubeba mzigo wa kurejesha eneo hilo peke yake.

6.2.2.7 Kodi na Mrabaha Kutokulipwa na PAET kwa Serikali.

i. Makadirio ya Kodi ya Mapato Kupunguzwa Moja kwa Moja Kutoka Kwenye Ankara za Mauzo ya Gesi

Mapitio yangu yamegundua kwamba, makadirio ya kodi ya mapato yanayolipwa na kampuni ya PAET kama ilivyo kwenye mkataba wa ushirikiano wa uchimbaji gesi wa Songosongo aya ya 12.(a) yanapunguzwa kwenye ankara za mauzo ya gesi kutoka TPDC.

Hii inapelekea kupungua kwa mapato ya Serikali kwa vile inapunguza mgawanyo wa mapato ambao unapelekwa TPDC.

Nashauri mkataba huu wa Songosongo uweze kujadiliwa upya ili kila upande uweze kulipa kodi yake stahili kwa Serikali.

ii. Makubaliano Yasiyoridhisha ya Malipo ya Mrabaha kwa Serikali

Mapitio ya kipengele XII cha mkataba wa uzalishaji wa pamoja wa gesi ya Songosongo yamegundua ya kwamba aya 12.2(c) inaelekeza kwamba TPDC ndilo litakalolipa mrabaha kwa Serikali kutokana na mgawo wake wa mapato unaotokana na faida kutoka kwenye eneo la uwekezaji.

Kutokana na kifungu tajwa hapo juu, nimegundua ya kwamba mrabaha umekuwa ukilipwa na TPDC kutoka kwenye mgawo wake wa mapato ya gesi, na mbia wake PAET halipi mrabaha ambapo ni kinyume na hali halisi ya uvunaji wa maliasili za nchi.

Vile vile, mkataba huo haujaeleza ni asilimia ngapi inatakiwa kulipwa kama mrabaha.Hata hivyo,niligundua ya kwamba kiwango cha mrabaha ambacho kinalipwa na TPDC ni asilimia 12.5 ya mapato inayopata toka kwenye mgao wa mapato ya mkataba.

Ni maoni yangu kwamba, mrabaha kulipwa kutoka kwenye gawiwo la TPDC kunaifanya kampuni ya PAET kutokulipa mrabaha. Hivyo kunasababisha kupotea kwa mapato ya Serikali. Hivyo, napendekeza mkataba wa Songosongo ujadiliwe upya na kipengele cha mrabaha kiweze kulipwa kutoka kwenye jumla ya uzalishaji wa gesi kabla ya kuondolewa kwa gharama za utafutaji gesi.

6.2.2.8 Mkataba wa Songosongo Kuruhusu PAET Kurudishiwa Gharama za Masoko na Utafiti wa Masoko.

Mkataba wa Songosongo aya ya 2.6 ibara ya II na III kifungu kidogo D (Taratibu za Kihasibu) umeorodhesha gharama ambazo zinastahili kurejeshwa bila kuomba idhini ya TPDC. Gharama za utafiti wa masoko na utafutaji masoko ambazo hazijazidi dola za kimarekani 250,000 ni mojawapo ya gharama ambazo zimeorodheshwa kustahili kurejeshwa.

Ni maoni yangu kwamba, gharama za masoko na utafiti wa masoko hazistahili kuingizwa kwenye gharama za utafutaji na uendelezaji wa gesi, hivyo kukubaliwa kurejeshwa kunapunguza mapato ya Serikali.

Hivyo, napendekeza kwamba, marejeo ya mkataba huu yahakikishe gharama hizo zimeondolewa kwenye orodha ya gharama zinazostahili kurejeshwa kwa mwekezaji.

6.2.2.9 Kushindwa kwa TPDC Kushiriki Kwenye Uwekezaji wa Shughuli za Maendeleo ya Uchimbaji wa Gesi

Katika kipindi cha ukaguzi, niligundua ya kwamba kinyume na kifungu cha 8(b) cha ibara ya VIII ya mkataba wa uzalishaji wa pamoja kati ya PAET na TPDC, TPDC haikuweza kushiriki kwenye uwekezaji wa shughuli za undelezaji wa uchimbaji wa gesi eneo la Songosongo tangu shughuli zilipoanza mwaka 2001.

Vile vile, niligundua ya kwamba TPDC na PAET wanarasimu ya mkataba wa ushirikiano wa pamoja ambayo tangu mwaka 2009 haijakamilika.

Ni matumaini yangu kwamba, kwa TPDC kutoshiriki kwenye shughuli za maendeleo kunaongeza athari ya TPDC kupoteza sehemu ya mapato kwa kutojua namna mapato ya ujumla na shughuli za uchimbaji wa gesi zinavyofanyika.

Napendekeza TPDC kuthathmini ulazima wa kushiriki kwenye shuguhuli za maendeleo kwa sasa, ikiwa hivyo TPDC na PAET wapiti upya na kusaini rasimu ya mkataba wa mashirikiano wenye tija kwa Serikali.

6.2.2.10 Kutosuluhishwa kwa Mgogoro wa Kimkataba Kuhusu Gharama Zinazopaswa Kurejeshwa Kiasi cha USD milioni 34.

Ukaguzi wangu umegundua ya kwamba TPDC na PAET bado wana mgogoro kuhusu usahihi wa gharama zinazopaswa kurejeshwa kiasi cha dola za kimarekani milioni 34 tangu tarehe 30 Novemba 2012.

Maoni yangu ni kwamba, kucheleweshwa kwa usuluhishwaji wa mgogoro huu unaweza kusababisha PAET kupeleka mashtaka mahakama ya usuluhishi wa migogoro. Kitendo hiki kitaigharimu Serikali hasa katika swala la kulipia gharama za kisheria na faini endapo itashindwa kesi.

Nashauri pande zote mbili kumaliza tofauti za mgogoro huu kwasababu unamadhara kwa kuathiri gharama zinazotakiwa

kurejeshwa hivyo kuchelewesha gawiwo lililokusidiwa kupatikana Kwa Serikali.

SURA YA SABA

UKAGUZI MAALUM NA KAGUZI ZA UCHUNGUZI WA KISAYANSI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

7.0 Utangulizi

Sura hii inaangalia mambo muhimu zaidi yaliyojitokeza katika kaguzi maalum na kaguzi za uchunguzi wa kisayansi katika Mashirika ya Umma. Kaguzi hizi maalum zimefanyika kwa mujibu wa Kifungu Na. 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 na Kanuni ndogo Na. 1 ya Kanuni ya 79 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009.

Katika mwaka huu wa ukaguzi, zilifanyika kaguzi maalum nne (4) na kaguzi wa Uchunguzi wa kisayansi mmoja (1). Kaguzi maalum nne zilifanyika katika Chuo cha Biashara (CBE), Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO) na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA). Ukaguzi wa kiuchunguzi ulifanyika kwenye Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (TGB). Yafuatayo ni mambo muhimu zaidi yaliyojitokeza kwenye kaguzi hizo:

7.1 Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)

Ukaguzi huu ulifanyika kufuatia maombi kutoka kwa Katibu Mkuu Uchukuzi kupitia barua yenye Kumb. Na. CCB.364/505/01 ya tarehe 23 Machi, 2016. Ukaguzi ulilenga kubaini waliohusika katika ukwepaji wa tozo za ushuru wa forodha na kubaini kiwango cha hasara iliyotokana na ukwepaji wa malipo husika.

Ukaguzi huu ulibaini upotevu wa malipo ya tozo za ushuru wa forodha Shilingi 15,021,886,716 ambayo hayakuingia katika akaunti ya TPA kutokana na ubadhirifu kwa njia zifuatazo:

i. Ankara za zaidi ya shilingi bilioni 1.13 na stakabadhi zake zilikubaliwa katika kutoa mzigo katika Bandari ya Dar es Salaam kupitia Bandari za nchi kavu (ICDs/IFs) ikionesha ushuru wa forodha umelipwa. Hata hivyo, hakuna rekodi ya malipo yaliyoakisiwa katika mfumo wa malipo wa TPA.

ii. Ankara zenye thamani ya Shilingi milioni 50.22 zilitambuliwa na TPA, hivyo kukubalika kutolea mzigo. Hata hivyo, ankara hizo hizo zilibainika kuwa zilifutwa katika mfumo wa malipo.

iii. Jumla ya ankara 1,310 za Shilingi bilioni 4.17 ambazo namba zake zilibainika kuwa kwenye mfumo wa malipo wa Bandari, zilitumika kutoa mizigo tofauti ya mawakala tofauti wa kutoa mizigo bandarini yenye thamani tofauti na hivyo yenye ushuru tofauti wa forodha.

iv. Ankara zenye zaidi ya Shilingi milioni 131.16 zimetumika kwa zaidi ya mzigo/nyaraka ya shehena (bill of lading) moja kwa wakala mmoja wa kutoa mizigo bandarini.

v. Hundi za shilingi milioni 195.54, ambazo miongoni mwao nyaraka za kuweka fedha (deposit slips) zilipokelewa kutoka benki ya CRDB, ambazo zilifikishwa benki ya CRDB na mawakala mbalimbali wa kutoa mizigo bandarini kwa ajili ya kulipa ushuru wa forodha zilionesha kuwa zimetumika kutoa mizigo inayohusiana na mawakala tofauti. Pia wengine nyaraka zao za kuweka fedha bado hazijapatikana kutoka CRDB mpaka wakati ripoti hii inaandikwa.

Wakala wa kutoa mizigo bandarini wanaofikia 82 hawakuweza kuleta taarifa zao katika ukaguzi huu, hivyo hawajawekwa kwenye uchambuzi.

Ukaguzi pia ulibaini mapungufu katika mfumo wa malipo kwa kuwa hakukuwa na muunganiko kati ya Bandari, Mamlaka ya Mapato na Benki ya CRDB katika taarifa za ulipaji. Hivyo, Kitengo cha mapato cha Bandari hakiwezi kujua kiasi cha ushuru wa forodha wa kutoza mpaka wakala wa kutoa mizigo bandarini alete nyaraka ya kuruhusu mzigo.

Nashauri Mamlaka ya Bandari kufuatilia na kurejeshewa fedha kutoka Benki ya CRDB shilingi milioni 195.54, ambapo hundi za benki hiyo zilipokelewa na Mamlaka. Hundi za shilingi milioni 616.37 na Dola za Marekani 21,789 ambazo zilipelekwa kwa ajili ya malipo katika benki ya CRDB hazikupatikana kipindi cha ukaguzi, zinatakiwa kukaguliwa vizuri na fedha husika kurejeshwa kutoka benki hiyo.

Mfumo wa malipo wa Mamlaka unatakiwa kuimarishwa ili usiruhusu kujirudia kwa hati za madai na stakabadhi. TPA ihakikishe kuna uwepo wa muunganiko wa taarifa kati ya Mfumo wa TANCIS na Mifumo ya Uendeshaji ya Bandari (Harbour View, Mfumo wa Mizigo na Mfumo wa kutolea bili) ili kuwezesha usahihi wa taarifa za meli (Call ID), manifesto na nyaraka za kuruhusu mizigo kwa ajili ya kufanya mlinganisho na ukaguzi.

7.2 Shirika la Viwanda Vidogovidogo (SIDO)

Bodi ya Wakurugenzi SIDO iliiomba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya Ukaguzi Maalum kwa mujibu wa Kifungu cha 29 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008. Mnamo Oktoba 21, 2015 nilianzisha Ukaguzi Maalum Juu ya Usimamizi wa Ardhi na Majengo yanayomilikiwa na Shirika la Viwanda Vidogovidogo (SIDO). Ukaguzi huu ulilenga kuhakiki

uhalali na usahihi wa thamani za Ardhi na Majengo, umiliki wa mali hizo na kutathmini misingi ya mchakato wa uuzaji wa mali hizo.

Ukaguzi ulibaini mabadiliko ya umiliki wa viwanja 25 vya SIDO ambayo hayakufuata taratibu za kisheria uliofanywa na Halmashauri za Wilaya za Kinondoni, Mtwara, Mbeya na Moshi. Mabadiliko hayo yalibatilishwa kupitia uthibitisho niliopokea kutoka Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Pia, iligundulika kuwa Menejimenti ya SIDO haikulinda ipasavyo ardhi waliyopewa na Serikali kwa kuwa hawakukamilisha taratibu za umiliki wa viwanja hivyo Wizara ya Ardhi. Pia, nyumba ya makazi katika Kitalu 41, Kinondoni ilikuwa inatumiwa na mfanyakazi wa zamani wa SIDO,ambapo, mtumishi huyo naye aliipangisha kwa mtu mwingine kinyume na taratibu.

Ukaguzi ulibaini pia uuzaji wa Viwanja vitano (5) SIDO vyenye Na.09 na 10 Kitalu "X" Mwakibete, Mbeya na Viwanja Na.673 - 675 Kitalu 46 Kijitonjama, Dar es Salaam kwa watu binafsi na Mfuko wa Pensheni wa PPF bila kufuata taratibu sahihi.

Shughuli za wapangaji wa Jengo la SIDO Small Business House (SSBH) haziko sambamba na malengo makuu ya SIDO. Ilibainika kuwa baadhi ya vyumba zilipangishwa kama vibanda ya chakula na vinywaji, ofisi za mawakili, taasisi zisizo za Kiserikali (NGO's) n.k. Kwa upande mwingine, kumekuwa na kesi mahakamani dhidi ya SIDO kuhusiana na wapangaji wa SSBH za mwaka 2007 na 2012 zilizofunguliwa na Scan-Tech Co. Ltd na Pluto Emanuel Minja na wengine 21 kwa mtiririko huo. Kesi hizi zimekuwa zikizuia SIDO kutumia jengo la SSBH kwa ufanisi.

Kwa upande mwingine, ukaguzi ulibaini makubaliano yasiyofaa ya viwanja vilivyokodishwa na Menejimenti ya SIDO kwa JAE (T) Ltd ambayo yalipelekea utaratibu wa 'Build Operate & Transfer

(BOT)' kufanyika kwa kipindi cha miaka 37 ambapo SIDO haikunufaika vya kutosha na matumizi ya Ardhi hiyo. Zaidi ya hayo, Mikataba kwa ajili ya kubadilishana sehemu ya ardhi ya SIDO na sheds sita (6) za viwanda haikuwa na ripoti za thamani ya ardhi hali inayoonyesha kwamba thamani halisi ya Ardhi hiyo haikufahamika kabla ya kubadilishana.

Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) iliibinafsisha Mbeya Ceramics Company (MBECECO), kampuni tanzu ya SIDO kwa Kyela Valley Foods Ltd mwezi Agosti 1995. Mkataba wa Mauzo ya Mali ulimtaka Kyela Valley Foods kuanza operesheni mara moja baada ya kununua. Kinyume chake, utekelezaji ulichelewa, Julai 2011 mapitio ya kikosi kazi cha Consolidated Holdings Corporation (CHC) juu ya makampuni mbalimbali yaliyobinafsishwa yalipendekeza kusitishwa kwa mkataba huo. Hata hivyo, mapendekezo hayo hayajatekelezwa tangu mwaka 2011.

Nilibaini kuwapo kwa Kesi Na. 4 ya 2012 ya Kyela Valley Foods Ltd wakidai Shilingi Bilioni 9.2 dhidi ya Mbeya City, SIDO na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kesi inatuhumu Mbeya City na SIDO kuruhusu wafanyabiashara waliosababisha moto ulioleta hasara katika eneo lililobinafsishwa kwake.

Mapendekezo;

i. Napendekeza Menejimenti ya SIDO kuchukua hatua muhimu ili kuokoa viwanja vyote vilivyobadilishwa bila kufuata utaratibu;

ii. Hatua mwafaka zichukuliwe dhidi ya wafanyakazi kutoka Halmashauri ya Manispaa za Kinondoni, Moshi, Mbeya, Mtwara na Wizara ya Ardhi ambao walihusika katika kubadili umiliki wa viwanja hivyo;

iii. SIDO iharakishe kufuatilia uhamisho wa umiliki wa viwanja ambavyo havina hati;

iv. Menejimenti iishirikishe Serikali ili kupata fedha kwa ajili ya maendelezo ya viwanja visivyoendelezwa kwa muda mrefu;

v. SIDO kujadili na JAE (T) Ltd ili kupata faida za makubaliano ya miaka 37 kipindi;

vi. Serikali kupitia Msajili wa Hazina inatakiwa kufikiria kusimamisha makubaliano ya kuuza mali kati ya PPSRC na Kyela Valley Foods Limted kutokana na ukiukwaji wa mkataba;

vii. Menejimenti ianzishe Kitengo cha 'Real Estate' ili kuwezesha usimamizi wa kitaalamu wa mali za Shirika; na

viii. Menejimenti ya SIDO inatikiwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili kuwaondoa wapangaji wa SSBH huku wakitatua migogoro iliyopo kwa amani.

7.3 Ukaguzi Maalum wa Ubia kati ya Shirika la Madini (STAMICO) na Tanzanite One Mining Limited (TML)

Ukaguzi Maalum wa Ubia wa Uendeshaji kati ya STAMICO na TML (hisa 50% kila mmoja) ulifanyika baada ya kupata maombi kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kupitia barua yenye Kumb. Na. CA 2/88 /01/J/222 ya tarehe 15 Februari 2016.

Ukaguzi huu ulijikita katika kutafuta kujua iwapo TML (Operator) alikuwa na udhibiti wa ndani katika kutekeleza uendeshaji wa ubia huo kutoka tarehe 20 Juni 2013 hadi Desemba, 2015.

Ukaguzi ulibaini masuala muhimu yafuatayo:

i. Mnamo tarehe 30 Januari 2015, Wizara ya Nishati na Madini ilitoa ridhaa ya mauzo ya hisa za asilimi 50 za TML (mbia wa

Serikali) zilizomilikiwa na M/s. Richland Resources Ltd kwenda kwa M/s. Sky Associates Ltd bila kufanya upembuzi yakinifu (due diligence) juu ya uwezo wa kifedha na kiufundi wa M/s. Sky Associates katika kufanya shughuli za uchimbaji wa madini ya Tanzanite. Uhamisho wa hisa za TML kati ya M/s. Sky Associates na M/s. Richland unahatarisha maslahi ya Serikali katika TML.

ii. Hapakuwa na akaunti ya pamoja ya mauzo wala akaunti ya 'Rehabilitation' iliyofunguliwa na TML, hivyo mapato yote ya mauzo ya Tanzanite yaliingia katika Amana Bank Akaunti Namba 005110122860001 na 005110122860002 zinazomilikiwa na TML. STAMICO haina udhibiti wa mapato ya mauzo ya Tanzanite na haijapata faida yoyote bado katika ubia huu.

iii. Januari hadi Septemba, 2015 Tanzanite yenye uzani wa Kilo 367.94 yenye thamani ya Dola za Marekani 3,374,683 ilichukuliwa kutoka mgodini kwenda Arusha kwa ajili ya kuchagua, kukata na kusafisha (polishing) kinyume na Ibara ya 15(1)(b) ya Mkataba. Kutengeneza Tanzanite nje ya mgodi huenda kusionyeshe thamani halisi ya madini hayo na hivyo kodi ya ongezeko la thamani na mrahaba isiwe katika viwango sahihi.

iv. Hadi tarehe 31 Machi 2016 TML ilikuwa haijalipa malipo ya kisheria kiasi cha Shilingi 4,396,083,315.09 yanayopaswa kulipwa kwa TRA, NHIF, NSSF, Simanjiro DC na TAMICO hii ina maana kwamba TML haifuati Sheria na Kanuni mbalimbali.

v. Uchimbaji madini haramu usiodhibitiwa unaoendelea chini ya ardhi ya Kitalu "C" ya TML yani "mitobozano" ni changamoto kubwa katika uzalishaji wa Tanzanite. Hii ni kwa kuwa unaleta wasiwasi mkubwa wa usalama katika shughuli za kila

siku za uchimbaji wa madini. Mahandaki hayo chini ya ardhi hutumiwa kwa ajili ya ulanguzi wa Tanzanite kutoka Kitalu "C" na wachimbaji haramu, hivyo kusababisha hasara katika Mapato ya Serikali.

Mapendekezo:

i. Wizara ya Nishati na Madini inapaswa kufanya upembuzi yakinifu na kutathmini uwezo wa M/s. Sky Associates Ltd katika kufanya shughuli za uchimbaji wa madini ya Tanzanite;

ii. Menejimenti ya STAMICO ikishirikiana na TML (mbia mwenza) ihakikishe ufunguzi wa Benki Akaunti ya pamoja na wote kuhakikisha kwamba mapato yote ya mauzo Tanzanite yanaingia kwenye akaunti hiyo;

iii. STAMICO iimarishe usimamizi katika uchakataji wa Tanzanite kwa kuhakikisha unafanyika mgodini kwa kutumia mitambo ya TML katika uwepo wa STAMICO na Taasisi zingine za Serikali kama inavyotakiwa;

iv. Menejimenti ya TML inapaswa kuhakikisha malipo yote ya kisheria yanalipwa kwa wakati kulingana na mahitaji ya Sheria husika; na

v. Kamishna wa Madini mara moja afanye ukaguzi maalum chini ya ardhi katika vitalu vyote vya Tanzanite. Pia akague kwenye shughuli za wachimbaji wadogo katika eneo la migodi ili kubaini kiwango cha uchimbaji kinyume na sheria na kuchukua hatua stahiki ipasavyo.

7.4 Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)

Ukaguzi Maalum wa Chuo cha Elimu ya Biashara uliombwa na Katibu Mkuu (Biashara na Uwekezaji) wa Wizara ta Viwanda, Biashara na Uwekezaji, mnamo tarehe 19 Mei, 2016, kupitia barua yenye kumbukumbu na. CKA23/48/01/1 baada ya Wafanyakazi wa Chuo hicho kutoa malalamiko ya matumizi mabaya ya fedha yanayofanywa na utawala wa Chuo hicho katika Kampasi zake za Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya na Mwanza. Ukaguzi wangu ulibaini yafuatayo:

7.4.1 Matumizi Mabaya ya Ada za Wanafunzi

Kifungu Namba 4(4) cha Muongozo wa Fedha wa Chuo kinataka ada za wanafunzi kulipwa moja kwa moja katika akaunti maalum ya Chuo, kisha stakabadhi ya malipo kupelekwa chuoni. Ukaguzi wangu katika Kampasi ya Dodoma ulibaini kuwa, shilingi milioni 265.53 kutoka kwa wanafunzi hazikuonekana katika kumbukumbu za Chuo. Ada hizo zilizopokelewa hazikulipwa kupitia akaunti ya Chuo, bali zilipokelewa moja kwa moja na Ofisi ya uhasibu kinyume na matakwa ya muongozo wa fedha.

Wafanyakazi sita (6) waliohusika katika upotevu huo walifukuzwa kazi huku wanafunzi wakiamriwa kulipa upya ada hizo. Mpaka wakati wa ukaguzi huu, kiasi cha shilingi 108,965,400 kilikuwa tayari kimeshalipwa na wanafunzi hao.

Ukaguzi katika Kampasi ya Mwanza ulibaini ubadhirifu wa Shilingi 17,671,600 uliofanywa na Mhasibu aliyekuwa akipokea ada za wanafunzi na kuwaaminisha kuwa angezipeleka benki. Hata hivyo, hakuzipeleka benki na wakati mwingine akipeleka kiasi pungufu.

Tumebaini kwamba Mhasibu huyo alitumia mbinu ya kughushi risiti, ambapo, risiti halali iliyotolewa kwa mwanafunzi inaonesha kiasi sahihi alicholipa wakati nakala za risiti hizo zinazobaki kwenye kitabu zinaonesha kiasi pungufu. Kiasi hicho pungufu

kinachoonekana katika nakala za risiti (carbon copy) ni sawa na kiasi kinachoonekana katika slip ya benki na taarifa za benki (bank statement).

Kufuatia ubadhirifu huo, Menejimenti ilichukua hatua ya kutoa taarifa Polisi. Mhasibu huyo aliacha kazi. Mpaka wakati wa ukaguzi huu, kiasi cha Shillingi 15,008,000 kilikuwa kimesharejeshwa Chuoni.

7.5 Ukaguzi wa Uchunguzi Juu ya Tuhuma za Matumizi Mabaya ya Ofisi Katika Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania

Kwa mujibu wa Kifungu cha 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 na baada ya kupokea tuhuma juu ya matumizi mabaya ya ofisi, mnamo Oktoba 26, 2016 nilifanya Ukaguzi wa kiuchunguzi katika Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania na kubaini yafuatayo:

7.5.1 Kodi ya Ushindi wa Michezo Isiyokusanywa Shilingi 427,906,771

Ukaguzi umebaini kiasi cha Shilingi 427,906,771 ambayo ni kodi ya ushindi wa michezo ya bahati nasibu haijakusanywa kutoka kwa M/s. Entertainment Africa Ltd kwa miezi ya Julai na Agosti mwaka 2015.

Tarehe 30 Juni 2015 kodi ya ushindi wa michezo ilianzishwa kufuatia marekebisho ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ya 2003. Bodi ya Michezo kupitia barua yenye Kumb. Na. GBT/SB/131/VOL.i/42 ilitoa utaratibu wa namna ambayo ukusanyaji wa kodi hiyo utafanyika.

Kampuni ya Entertainment Africa Ltd ilibaini matatizo katika ukusanyaji wa kodi hiyo, kwamba hakuweza kuratibu mashine zake za michezo ya kubahatisha ndani ya miezi miwili. Malipo ya

Shilingi 200,000,000 yalilipwa kufidia kodi ya Shilingi 300,899,241 na Shilingi 327,007,530 kwa ajili ya mwezi wa Julai na Agosti 2015. Kwa muktadha huo, kodi ya Shilingi 427,906,771 bado haijalipwa.

7.5.2 Kodi ya Adhabu Isiyokusanywa Shilingi 80,237,357

Kufuatia kuwasilisha malipo madogo ya kodi, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha kwa barua yenye Kumb.Na. GBT/CAS/TEL/VOL.IV/14 ya Desemba 3, 2013 iliitoza M/s. Le Grande Casino adhabu ya Shilingi 80,237,357 (ambayo ni asilimia 50% ya kiasi kikuu) kwa mujibu wa Kifungu cha 35 (2) cha sheria ya Michezo ya Kubahatisha No.4 ya mwaka 2003.

M/s. Le Grande Casino aliomba msamaha kwa ajili ya adhabu hiyo kwa msingi kuwa kosa la kuwasilishwa kodi pungufu halihusiani na matakwa ya Kifungu cha 35 (2). Bodi ilikataa maombi hayo, kwani hawawezi kuondoa adhabu hiyo kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Ninapendekeza kuwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ishirikishe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Kamishna Mkuu wa TRA kuhakikisha kodi ambazo hazijakusanywa kutoka kwa Entertainment Africa Ltd na Le Grande Casino zinakusanywa.

7.6 Ukaguzi Maalum wa Ubia kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na ETC Holding Limited (ETC)

Ukaguzi Maalum wa ubia wa Uendeshaji kati ya NDC na ETC Cargo Ltd (wenye umiliki wa mtaji wa asilimia 25% kwa 75%) ulifanyika baada ya kupata maombi kutoka Katibu Mkuu Wizara ya Biashara Viwanda na Uwekezaji kupitia Barua yenye Kumb. Na. CAB.211/263/01/29 ya tarehe 21 Juni 2016.

Ubia huo ulianza Januari 14, 2009 ukiwa na lengo kuu la kuendeleza Bandari Kavu na Kiwanda cha Usindikaji wa Bidhaa za

Kilimo kwenye viwanja No.1-66 Kitalu 'R' na 101 Kitalu 'Q' vilivyopo Mbagala Rangi Tatu, Dar es Salaam.

Sambamba na Kifungu 29 (2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 nilianzisha Ukaguzi Septemba 19, 2016 wenye lengo kuu la kutaka kujua iwapo ubia huo unatekelezwa kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa au la. Yafuatayo yalibainika:

7.6.1 Uundaji na Kusaini Mkataba wa Ubia huo bila Mapitio na Ridhaa ya Mwanasheria Mkuu

Mkataba kati ya NDC na ETC Holding Limited ulisainiwa tarehe 14 Januari 2009 bila kupitiwa na kuridhiwa. Kaimu Msajili wa Hazina kupitia barua Na. TYC/N/40/6/17 ya tarehe 11Aprili 2011 alisema kwamba NDC walipaswa kuwasilisha rasimu ya Mkataba huo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kusainiwa kwa kuwa Mkataba huo unahusisha kiasi zaidi ya Shilingi milioni 50.

7.6.2 Mkopo wa Dola za Marekani 9,647,605 kutoka ETC Holding Limited uliotolewa kwa ETC Cargo Limited bila kibali cha Bodi ya Wakurugenzi

Tarehe 1 Januari 2012, ETC Holding Ltd iliingia mkataba na ETC Cargo Ltd wa mkopo wa USD 9,647,605 kufadhili mahitaji ya mtaji. Mkopo huo ulitolewa kwa riba ya asilimia 8.50 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu (3).

Mkutano wa 13 wa Bodi ya ETC Cargo Ltd uliofanyika tarehe 20 Juni 2013, ikiwa ni miaka 4 na nusu tangu kuanzishwa kwa mkataba, uliidhinisha kutolewa kwa mkopo huo. Hata hivyo, idhini ya Bodi ya Wakurugenzi haikutolewa kabla ya kuingia mkataba. Aidha, jumla ya mkopo wa Dola za Marekani milioni 10.35 ulitolewa kwenda kwa M/s. ETC Cargo Ltd tarehe 31 Mei 2013 badala ya Dola za Marekani milioni 9.65 kama ilivyokuwa kwenye makubaliano, hivyo, kufanya Dola za Marekani 707,164 kulipwa juu ya kiasi cha makubaliano.

7.6.3 Uhamisho wa Viwanja vya NDC Na 1-66 Kitalu "R" Mbagala Rangi Tatu kwenda kwa ETC Cargo Ltd (Company) bila Kufuata Taratibu

Uhamisho wa umiliki wa Kiwanja Na. 1-66 Kitalu "R" kwenda kwa M/s ETC Cargo Ltd haukupata idhini ya Bodi ya Wakurugenzi wa NDC wala ridhaa ya Msajili wa Hazina. Pia, Kiwanja Na. 101 Kitalu "Q" kilikodishwa kwa miaka 98 kwa ETC Cargo Ltd na Menejimenti ya NDC bila idhini ya Bodi ya Wakurugenzi.

Kulingana na yaliyobainika ninapendekeza yafuatayo :

i. Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Menejimenti na Bodi ya NDC, na kwa kushauriana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wanapaswa kuhakikisha urejeshwaji wa mali za NDC ambazo zilihamishwa bila kufuata utaratibu.

ii. Menejimenti na Bodi ya NDC inapaswa kuchukua hatua mwafaka kwa watumishi wote wa NDC wanaohusishwa katika masuala mbalimbali yaliyoanishwa katika ripoti hii.

SURA YA NANE

MASUALA MENGINEYO NA MATOKEO YA JUMLA YA UKAGUZI

8.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea masuala mengineyo ya ukaguzi na matokeo ya ukaguzi ambayo kwa ujumla wake yameelezwa katika aya ya 8.1 na 8.2 kwa mtiririko huo hapa chini.

8.1 Masuala ya Ukaguzi mengineyo

Katika mwaka wa ukaguzi, nilifanya ukaguzi wa taasisi 150 na kubaini masuala muhimu ambayo yameripotiwa katika sura ya nne ya ripoti hii na masuala mengine na matokeo ya jumla ya ukaguzi ambayo yameelezwa katika aya ya 8.2 na Kiambatisho cha II. Pamoja na hayo, kulikuwa na kaguzi 32 zinazoendelea wakati wa wa kuandaa ripoti hii.

Hata hivyo, sikuweza kufanya ukaguzi kwa taasisi 18 kama ilivyoorodheshwa katika kiambatisho IV kutokana na ukosefu wa fedha kutekeleza kazi ya ukaguzi kwa Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo hayakuweza kumudu kulipa gharama za ukaguzi.

8.2 Matokeo ya Jumla ya Ukaguzi

Sehemu hii inahusisha masuala ambayo yamejitokeza kwenye mashirika mbalimbali. Masuala hayo yameainishwa hapa chini:

8.2.1 Kutokuwepo kwa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma

Kwa mwaka huu wa ukaguzi, kulikuwa na Bodi za mashirika 18 ambazo zimemaliza muda wake; na hakuna Bodi mpya za kusimamia mashirika hayo zilizochaguliwa hadi tunakamilisha ukaguzi wetu mwezi Machi 2017. Baadhi ya taasisi zimekuwa zikiendelea na utendaji wa kazi bila ya Bodi kwa zaidi ya mwaka mmoja. Taasisi ambazo hazina Bodi zimeonyeshwa kwenye kiambatisho III. Kutokuwapo kwa Bodi ya Wakurugenzi na

Wadhamini kunazorotesha shughuli za kiutendaji za mashirika hayo. Taasisi ambazo zina Bodi lakini hazikuweza kukaa kujadili na kupitisha taarifa za mahesabu zimeonyeshwa kwenye kiambatisho VI.

Tunashauri serikali iteue Bodi za Wakurugenzi na wadhamini kwa wakati pindi zinapomaliza muda wake.. Pia Bodi zipitie na kupitisha taarifa za mahesabu kwa muda muafaka ili kuwezesha mchakato wa ukaguzi kuendelea na kukamilika kwa wakati.

8.2.2 Uwezekano wa Kuwepo kwa Deni Linalotokana na Wafanyakazi Hewa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Katika mwaka 2015/16, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianzisha kikosi kazi kwa ajili ya kufanya zoezi maalum la kuwatambua wafanyakazi hewa katika taasisi mbalimbali za Serikali. Wafanyakazi hewa waliotambuliwa walikuwa katika mfumo wa malipo ya mshahara wa taasisi hizi. Hivyo, kuna uwezekano kuwa michango yao ilipelekwa kwenye mifuko ya pensheni.

Kaguzi za mifuko ya pensheni zimebaini kuwa mifuko bado haijapokea majina na taarifa za wafanyakazi hewa kutoka Hazina; na hakuna uhakiki binafsi uliofanywa na menejimenti za mifuko ili kutambua deni linalotokana na michango ya wafanyakazi hewa.

Kuna uwezekano wa kuwapo kwa deni linalotokana michango ya wafanyakazi hewa katika Mifuko. Ukubwa wa deni kwa kila mfuko unategemea idadi ya watumishi hewa wa umma wenye uanachama katika mfuko husika.

Menejimenti za Mifuko yaPensheni zinashauriwa kuwasiliana na Hazina ili kupata orodha ya wanachama waliotambuliwa kuwa wafanyakazi hewa. Zaidi ya hapo, mifuko inahitajika kufanya uhakiki binafsi kwa kuchambua wanachama waliopo ili kutambua

makisio ya deni linalodhaniwa. Pia inapaswa kuepuka kutambua mzigo mkubwa wa deni kwa wakati mmoja, kwani inaweza kuwa na athari kwenye utendaji wa mifuko.

8.2.3 Madeni ya Serikali Yaliyozidi Muda wa Kulipwa Shilingi trilioni 1.6

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakopa kutoka taasisi za mbali mbali za umma. Pia inadhamini mashirika mengine kukopa katika taasisi za umma kwa kuwa ina wajibu kisheria kufanya hivyo. Kwa mantiki hiyo, Serikali inachukua jukumu la madeni hayo yanayotakiwa kulipwa kulingana na matakwa ya kisheria na kimikataba kama walivyokubaliana.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16 imebainika ya kwamba, serikali inadaiwa shilingi trilioni 1.6 yaliyozidi muda wake wa kuliwa kutoka katika taasisi tofauti kumi na tisa (19). Madeni haya yanatokana na mikopo ya moja kwa moja, dhamana, na michango ambayo haikuwasilishwa kulingana na matakwa ya kisheria.

Pamoja na hayo, kuna mkopo wa shilingi bilioni 44.29 uliotolewa kwa Chuo Kikuu cha Dodoma na NHIF kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya. Aidha hakuna makubaliano wala udhamini wa serikali uliotolewa.

Jedwali Na. 13: Madeni ya Serikali yaliyozidi muda wa kulipwa

Na.	Taasisi inayokopesha	Asili ya mkopo	Muhusika/mkopwaji	Kiasi 'Shilingi bilioni
1	LAPF	Kutokuwasilishwa kwa michango	Wizara ya Fedha na Mipango	44.47
2	LAPF	mkopo wa upanuzi na uendelezaji	PPL BUNGE	4.55
3	LAPF	mkopo wa upanuzi na uendelezaji	Chuo Kikuu cha Dodoma	42.70
4	LAPF	mkopo wa upanuzi	HOMBOLO	69.85

Na.	Taasisi inayokopesha	Asili ya mkopo	Muhusika/mkopwaji	Kiasi 'Shilingi bilioni
		na uendelezaji		
5	LAPF	mkopo wa upanuzi na uendelezaji	Chuo cha Nelson Mandela	7.43
6	LAPF	kufidia mabadiliko kutoka mfumo wa uchangiaji kwenda mfumo wa mafao	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	74.43
7	WCF	Kutokuwasilishwa kwa michango	Wizara ya Fedha na Mipango	26.60
8	PPF	Mkopo wa ujenzi	Chuo Kikuu cha Dodoma	121.95
9	PPF	Mkopo wa ujenzi	Chuo cha Nelson Mandela	12.57
10	PPF	Mkopo wa ujenzi	Mradi wa NIDA	5.03
11	NHIF	Upatikanaji wa vifaa	Wizara ya Mambo ya Ndani	42.60
12	NHIF	Miradi ya CHF	Wizara ya afya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto	1.20
13	PSPF	mkopo wa upanuzi na uendelezaji	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu	259.67
14	PSPF	mkopo wa upanuzi na uendelezaji	Wizara ya Mambo ya Ndani	32.72
15	PSPF	mkopo wa upanuzi na uendelezaji	Ofisi ya Rais	27.97
16	PSPF	mkopo wa upanuzi na uendelezaji	Chuo Kikuu cha Dodoma	289.55
17	PSPF	mkopo wa upanuzi na uendelezaji	PCCB	14.02
18	NSSF	Dhamana ya Serikali	Mikopo ya makampuni	428.47
19	NSSF	Mkopo wa miradi ya Serikali	Taasisi mbalimbali	90.58
	Jumla Kuu			**1,596.35**

Kutokulipwa kwa madeni hayo kwa taasisi husika kunaathiri nguvu za kifedha za taasisi zinazotarajia kupokea fedha hizo; Kwa upande mwingine, kunaathiri shughuli zao za kiutendaji.

Serikali inashauriwa kufanya juhudi za makusudi kuokoa hali hiyo kwa kulipa madeni hayo; kwani baadhi ya taasisi zimedhoofika

kifedha kiasi kwamba haziwezi kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu na kwa ufanisi unaotakiwa.

8.2.4 Ucheleweshaji na Kutopelekwa kwa Makato ya Kisheria Shilingi bilioni 26.26

Tathmini ya makato ya kisheria ilibaini kwamba baadhi ya mashirika hayakupeleka makato yake kwa muda uliowekwa. Makato hayo ya kisheria ambayo hayakupelekwa yanajumuisha michango ya kodi ya VAT, PAYE, michango ya pensheni pamoja na kodi ya ujuzi na maendeleo lenye thamani ya shilingi bilioni 26.26.

Madeni hayo yameendelea kuongezeka kwa miaka kadhaa. Hali hii naweza kupelekea kulipa faini, riba, na adhabu ambazo zitaathiri hali ya kifedha ya mifuko; hivyo kupelekea kushindwa kufikia malengo yaliyopangwa.

Kutokulipa kwa kodi kunaweza kuaathiri kiasi cha mapato ambayo Serikali ingepata. Pia, kutolipa michango ya pensheni kwa wakati kunaathiri uwezo wa kulipa mafao kwa wafanyakazi wakati wa kustaafu.

Mafao ya wafanyakazi na kodi ambayo hayajapelekwa kwa wakati imeelezewa kwenye jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 14: Ucheleweshaji na kutopelekwa kwa makato ya kodi

Entity	Kodi (VAT & PAYE) 'Shilingi bilioni	Mifuko ya Pensheni 'Shilingi bilioni	SDL 'Shilingi bilioni	Jumla 'Shilingi bilioni
Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Songea	0.07	-	-	0.07
Chuo Huria cha Tanzania	3.64	0.44	-	4.08
Shirika la Posta Tanzania	10.58	-	3.77	14.35
DAWASCO	2.95	1.17	2.72	6.84

Entity	Kodi (VAT & PAYE) 'Shilingi bilioni	Mifuko ya Pensheni 'Shilingi bilioni	SDL 'Shilingi bilioni	Jumla 'Shilingi bilioni
Ushirika wa Soko la Kariakoo (KMC)	0.37	-	0.27	0.64
Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Lindi	0.06	0.09	-	0.15
Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Tanga	-	-	0.12	0.12
Jumla	**17.68**	**1.70**	**6.88**	**26.26**

Menejimenti za taasisi hizo zinashauriwa kufanya jitihada za ziada ili kuhakikisha makato yote ya kisheria yanapelekwa kwenye taasisi husika kwa wakati. Hali hii itasaidia kuepuka faini, riba na adhab7 u zisizokuwa za lazima.

8.2.5 Malipo Yaliyofanyika Bila Risiti za Kieletroniki (EFD)

Serikali ilianzisha utaratibu wa matumizi ya vifaa vya kielektroniki (EFD) ili kurahisisha utoaji wa risiti za mauzo kupitia Kanuni za Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) za mwaka 2010 na Kanuni za Kodi (Vifaa vya Kielekroniki) za mwaka 2012. Sheria hiyo inafanya utoaji wa risiti za kielektroniki kuwa lazima pindi wauzaji wanapouza bidhaa zao.

Kinyume na matakwa ya Sheria tajwa hapo juu, taasisi mbali mbali za umma zilifanya malipo ya jumla kiasi cha Sh 5.61 billioni bila kupatiwa risiti za kielektroniki kama uthibitisho wa malipo ya bidhaa zilizonunuliwa.

Jedwali Na. 15: Taasisi zilizofanya malipo bila kupatiwa risiti za kielektroniki:

Na	Jina la Taasisi	Kiasi kwenye Shilingi (Bilioni)
1	Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)	0.87
2	Chuo Kikuu cha Mzumbe (MU)	1.30

3	Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mbeya (MUWASSA)	3.44
	Jumla	**5.61**

Utoaji wa risiti za kielektroniki unarahisisha ukusanyaji wa kodi. Hii ni kwa sababu, vifaa hivyo hurahisisha upatikanaji sahihi wa taarifa za mauzo kadri risiti zinavyotolewa; hivyo kupunguza mwanya wa ukwepaji kodi. Kufanya malipo bila kupokea risiti za kielektroniki kama uthibitisho wa malipo kunaongeza mwanya wa ukwepaji kodi kwa wauzaji wa bidhaa; hivyo, kupunguza juhudi za Serikali katika ukusanyaji wa kodi.

Uongozi wa taasisi tajwa za umma unakumbushwa kudai risiti za kielektroniki kwenye manunuzi yote yanayofanywa na taasisi hizo ili kukidhi matakwa ya sheria.

8.2.6 Madeni ya Muda Mrefu ya Shilingi 61.28 bilioni

Ukaguzi ulibaini kuwa mashirika na taasisi mbalimbali zina wadaiwa ambao hawajalipa kwa muda mrefu. Madeni hayo yamepita ukomo wa malipo kama ilivyoelekezwa kwenye sera za kusimamia ukusanyaji wa maduhuri za kila shirika.

Kwa upande wa vyuo, tuligundua kuwa wanafunzi waliohitimu wameshachukua vyeti vyao bila kulipia madeni yao ya ada; Hivyo, kuwa ngumu kwa vyuo husika kuweza kukusanya madeni hayo. Vyuo ambavyo hali hii imeonekana ni pamoja na Chuo Kikuu Dar es Salaam (UDSM), Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE).

Malimbikizo hayo ya madeni ya muda mrefu yamesababishwa na ukosefu wa ufanisi katika usimamizi wa madeni. Zaidi ya hayo, kuna dalili za udanganyifu/rushwa kwa vile wahitimu hupokea vyeti vyao wakati hawajalipa na kumaliza madeni yao.

Mchanganuo wa madeni hayo ni kama ifuatavyo:-

Jedwali Na. 16: Madeni ya Muda Mrefu

Na.	Shirika/Taasisi	Asilimia ya deni zima	Kiasi Shilingi 'Bilioni'
1	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza	42%	2.16
2	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Moshi	86%	2.20
3	Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)	61%	1.18
4	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (DUCE)	51%	0.85
5	Chuo Kikuu cha Ardhi	99%	4.50
6	Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)	70%	5.68
7	Mamlaka ya Udhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA)	51%	14.60
8	Ubungo Plaza	87%	4.25
9	Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM)	69%	4.48
10	Chuo Kikuu Dar es Salaam (UDSM)	29%	6.79
11	Shirika la Utangazaji la Tanzania (TBC)	46%	2.57
12	Shirika la Posta Tanzania (TPC)	64%	10.75
13	Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP)	72%	1.26
	Jumla		**61.28**

Madeni yaliyoorodheshwa hapo juu ni muhimu na yanaweza kuathiri shughuli za mashirika na taasisi husika kwa sababu fedha nyingi zipo katika mikono ya wadaiwa badala kulipwa ili ziweze kutimiza majukumu yaliyolengwa.

Menejimenti za Mashirika na taasisi husika zinashauriwa kupitia upya taratibu na njia za usimamizi wa madeni kwa maboresho zaidi ili kuweza kukusanya madeni kwa wakati.

HITIMISHO

Napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa menejimenti za Mashirika ya Umma niliyoyakagua kwa ushirikiano walioutoa katika kufanikisha ukaguzi huu na hivyo kuwezesha kuwasilisha ripoti hii kwa Mheshimiwa Rais, Dk. John Pombe Joseph Magufuli.

Ni matumaini yangu kuwa, kupitia ripoti hii, Serikali itachukua hatua za haraka na muhimu kuhusiana na masuala yaliyojitokeza.

Hili litawezekana iwapo Serikali itaweka mikakati kama sera mpya, taratibu na mfumo wa sheria ili kuboresha utendaji wa Mashirika ya Umma kama ilivyoshauriwa katika ripoti hii.

Kuhusiana na mapendekezo yangu yaliyopita na yanayojirudia mara kwa mara, naisisitiza Serikali kuongeza juhudi katika utekelezaji wa mapendekezo hayo ili kuleta ufanisi katika Mashirika husika.

VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. I: Mchanganuo wa Hati Zilizotolewa katika mwaka 2015/2016

Na.	Shirika la Umma	Hati
1	Bodi ya Usajili ya Wasanifu na Wakadiriaji Majengo (AQSRB)	Hati Inayoridhisha
2	Chuo Kikuu cha Ardhi	Hati Inayoridhisha
3	Ukumbi wa Kimataifa wa Arusha	Hati Inayoridhisha
4	Chuo cha Ufundi Arusha (ATC)	Hati Inayoridhisha
5	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha	Hati Inayoridhisha
6	Taasisi ya Ukimwi ya Benjamini Mkapa	Hati Inayoridhisha
7	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba	Hati Inayoridhisha
8	Taasisi ya Saratani (Ocean Road)	Hati Inayoridhisha
9	Mamlaka ya Udhibiti wa Soko la Mtaji (CMSA)	Hati Inayoridhisha
10	Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Kijijini (CARMATEC)	Hati Inayoridhisha
11	Mamlaka ya Maji Safi Chalinze	Hati Inayoridhisha
12	Chuo cha Wanyama Pori - Mweka	Hati Inayoridhisha
13	Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)	Hati Inayoridhisha
14	Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB)	Hati Inayoridhisha
15	Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam (DIT)	Hati Inayoridhisha
16	Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE)	Hati Inayoridhisha
17	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)	Hati Inayoridhisha
18	Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASCO)	Hati Inayoridhisha
19	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA)	Hati Inayoridhisha
20	Bodi ya Bima ya Amana (DIB)	Hati Inayoridhisha
21	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma	Hati Inayoridhisha
22	Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA)	Hati Inayoridhisha
23	Baraza la Walaji la Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA CCC)	Hati Inayoridhisha
24	Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB)	Hati Inayoridhisha
25	Tume ya Ushindani (FCC)	Hati Inayoridhisha
26	Bodi ya Bahati Nasibu Tanzania	Hati Inayoridhisha
27	Mfuko wa Taifa wa Mafao ya Watumishi wa Serikali (GEPF)	Hati Inayoridhisha
28	Chuo cha Usimamizi wa Fedha	Hati Inayoridhisha
29	Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini	Hati Inayoridhisha
30	Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW)	Hati Inayoridhisha
31	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Iringa	Hati Inayoridhisha
32	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama	Hati Inayoridhisha

Na.	Shirika la Umma	Hati
33	Shirika la Masoko la Kariakoo	Hati Inayoridhisha
34	Kituo cha Elimu Kibaha	Hati Inayoridhisha
35	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kigoma	Hati Isiyoridhisha
36	Kampuni ya uendelezaji wa uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO)	Hati Inayoridhisha
37	Mfuko wa Pensheni wa LAPF	Hati Inayoridhisha
38	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Lindi	Hati Inayoridhisha
39	Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU)	Hati Inayoridhisha
40	Mamlaka ya Maji ya Masasi Nachingwea	Hati Inayoridhisha
41	Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya	Hati Inayoridhisha
42	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya	Hati Inayoridhisha
43	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa	Hati Inayoridhisha
44	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro	Hati Inayoridhisha
45	Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi	Hati Inayoridhisha
46	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Moshi	Hati Inayoridhisha
47	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara	Hati Inayoridhisha
48	Hospitali ya Taifa Muhimbili	Hati Inayoridhisha
49	Chuo cha Afya na Teknolojia Muhimbili	Hati Inayoridhisha
50	Mamlaka na Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma	Hati Inayoridhisha
51	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza	Hati Inayoridhisha
52	Chuo cha Mzumbe	Hati Inayoridhisha
53	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Namtumbo	Hati Inayoridhisha
54	Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA)	Hati Inayoridhisha
55	Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)	Hati Inayoridhisha
56	Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE)	Hati Inayoridhisha
57	Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC)	Hati Inayoridhisha
58	Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)	Hati Inayoridhisha
59	Chuo cha Usafirishaji (NIT)	Hati Inayoridhisha
60	Baraza la Sanaa la Taifa	Hati Inayoridhisha
61	Hifadhi ya Taifa Ngorongoro	Hati Inayoridhisha
62	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Njombe	Hati Inayoridhisha
63	Mfuko wa Pensheni NSSF	Hati Inayoridhisha
64	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT)	Hati Inayoridhisha
65	Mfuko wa Pensheni PPF	Hati Inayoridhisha
66	Bodi ya Wataalam wa Manunuzi na Ugavi	Hati Inayoridhisha
67	Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA)	Hati Inayoridhisha
68	Mfuko wa Pension wa Utumishi wa Umma (PSPF)	Hati Inayoridhisha
69	Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Same	Hati Inayoridhisha
70	Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga	Hati Inayoridhisha
71	Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Singida	Hati Inayoridhisha
72	Mfuko wa mikopo kwa wajasiriamali wadogo (SELF)	Hati Inayoridhisha
73	Udhibiti ya Mifuko Kijamii Tanzania (SSRA)	Hati Inayoridhisha
74	Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Songea	Hati Inayoridhisha

Na.	Shirika la Umma	Hati
75	Bodi ya Sukari Tanzania	Hati Inayoridhisha
76	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga	Hati Inayoridhisha
77	Baraza la walaji la Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi kavu na Majini	Hati Inayoridhisha
78	Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi kavu na Majini (SUMATRA)	Hati Inayoridhisha
79	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tabora	Hati Inayoridhisha
80	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga	Hati Inayoridhisha
81	Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania	Hati Inayoridhisha
82	Tume ya Nguvu za Nyuklia Tanzania (TAEC)	Hati Inayoridhisha
83	Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)	Hati Inayoridhisha
84	Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania	Hati Inayoridhisha
85	Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)	Hati Inayoridhisha
86	Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA)	Hati Inayoridhisha
87	Bodi ya Maziwa Tanzania	Hati Inayoridhisha
88	Mamlaka ya Elimu Tanzania	Hati Inayoridhisha
89	Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA)	Hati Inayoridhisha
90	Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)	Hati Inayoridhisha
91	Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)	Hati Inayoridhisha
92	Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE)	Hati Inayoridhisha
93	Benki ya Biashara - TIB	Hati Inayoridhisha
94	Benki ya Rasilimali -TIB	Hati Inayoridhisha
95	Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TSLB)	Hati Inayoridhisha
96	Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA)	Hati Inayoridhisha
97	Mamlaka ya Bandari Tanzania	Hati Isiyoridhisha
98	Benki ya Posta Tanzania	Hati Inayoridhisha
99	Bodi ya Tumbaku Tanzania	Hati Inayoridhisha
100	Bodi ya Utalii Tanzania	Hati Inayoridhisha
101	Bodi ya Usajili wa Maghala	Hati Inayoridhisha
102	Benki ya Wanawake Tanzania	Hati Isiyoridhisha
103	Bodi ya Chai Tanzania	Hati Inayoridhisha
104	Benki ya Maendeleo ya TIB	Hati Inayoridhisha
105	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa (TPRI)	Hati Inayoridhisha
106	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tukuyu	Hati Inayoridhisha
107	Benki ya Twiga Bancorp	Hati Inayoridhisha
108	Kampuni ya Ubungo Plaza	Hati Inayoridhisha
109	Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)	Hati Inayoridhisha
110	Chuo Kikuu Dodoma	Hati Isiyoridhisha
111	Kampuni ya Nyumba za Watumishi	Hati Inayoridhisha
112	Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)	Hati Inayoridhisha

Kiambatisho Na. II: Masuala Mengineyo ya Ukaguzi

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
1	MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA DODOMA (DUWASA)	**Ubadhilifu uliobainika wa shilingi milioni 590.85**	
		Menejimenti ya DUWASA iliripoti ubadhilifu wa shilingi milioni 590.85 ambao ulifanywa na wafanyakazi wa mamlaka hii kama ilivyoonyesha kwenye ripoti ya hesabu katika kipengele Namba 23. Ilibainika kwamba kiasi cha shilingi milioni 408.85 zilikusanywa kutoka katika wateja wa maji lakini hazikuwekwa kwenye akaunti ya benki ya mamlaka. Pia, taarifa za wateja zenye thamani ya shilingi milioni 185.85 zilibadilishwa na baadhi ya wafanyakazi wa mamlaka wasiokuwa waaminifu. Hii inasababishwa na kutokuwa na mifumo ya ndani madhubuti ya usimamizi wa makusanyo na fedha. Hali hii inaashiria uwezekano wa kuwapo kwa ubadhilifu mwingine unaoendelea ambao haujabainika.	Menejimenti inashauriwa kuhakikisha kiasi cha fedha kilichopotea kinarudishwa kwenye mamlaka. Pia kuhakikisha mifumo ya usimamizi ya ndani inaimarika ili kupunguza uwezekano wa ubadhilifu.
2	MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA MWANZA (MWAUWASA)	**Mikataba iliyosainiwa bila ya dhamana ya utendaji shilingi milioni 529.05**	
		Kanuni za manunuzi zinamhitaji mzabuni aliyeshinda kuwakilisha kwenye taasisi husika dhamana ya utendaji (performance security) iwe kama dhamana yake ya kufanya na kumaliza kazi aliyopewa. Ilibainika kwamba kiasi cha zabuni zenye thamani ya	Menejimenti inashauriwa kuhakikisha dhamana za utendaji zinapatikana kutoka kwa wazabuni kabla ya kupewa mkataba wa kufanya kazi ili kupunguza usumbufu wowote utakaoweza katika kutekeleza majukumu ya mkataba wa kazi.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		shilingi milioni 529.05 zilitolewa kwa wazabuni bila ya mamlaka kupokea dhamana ya utendaji kutoka kwa wazabuni hao. Hali hii inaweza kulipa MWAUWASA hasara endapo mzabuni atashindwa kufanya kazi yake kama inavyotakiwa.	
		Bidhaa zilizonunuliwa bila ya mkataba shilingi bilioni 1.19	
		Kanuni ya 50 ya sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 inaitaka taasisi yoyote kuwa na mkataba (framework agreement) kabla ya kununa bidhaa ili kuhakikisha mchakato wa manunuzi unafanyika kwa ufanisi na kwa gharama nafuu. Imebainika kwamba bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 1.19 zilinunuliwa katika mwaka 2015/2016 bila kuwa na mkataba. Manunuzi yote haya yalifanyika kutoka kwa wazabuni wawili tuu. Hali hii ya kutokuwa na mkataba baina ya wazabuni na Mamlaka inaweza kuathiri maslahi ya mamlaka.	Menejimenti inashauriwa kuhakikisha kuwa sheria ya manunuzi inazingatiwa kikamilifu ili kupunguza uwezekano wa hasara au matatizo yananyoweza kusababishwa na kutofuata sheria hii ya manunuzi.
3	MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA (NHIF)	**Kutokuwa na mikataba na watoa huduma ya Afya**	
		Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya ya Mwaka 1999 inauhitaji Mfuko kuwa na mikataba halali na watoa huduma katika kipindi chote. Pia, muongozo wa madai Inaihitaji menejimenti kushughulikia madai ya watoa huduma ambao Mfuko	Menejimenti inashauriwa kuwa na mikataba na watoa huduma wote ili kuondokana na hatari zinazohusiana na kutofuata amri na sheria mbalimbali za Mfuko.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		umeingia nao mkataba. Katika mwaka 2014/2015 ilibainika kwamba vituo 6 vya kutoa huduma vilikuwa havijasajiliwa ikiwa ni hospitali ya Tumaini, Regency, Kairuki, MOI, Muhimbili na Taasisi ya Kansa ya Ocean Road. Kutokuwa na mikataba na watoa huduma kunaweza kusababisha hasara kwa mfuko, hasa pale inapotokea mafarakano au kutokubaliana.	
		Kuwa na usimamizi duni wa fedha	
		NHIF haina sera rasmi amabayo imeweka kikomo cha juu ambacho anaweza kupatiwa mfanyakazi kwa ajili ya mafunzo ya kikundi, na mikutano. Matokeo yake ni kwamba, mfanyakazi anaweza akapewa kiasi chochote kwenye akaunti yake ya benki ili kukidhi shughuli mbalimbali. Katika kipindi cha mwaka unaoishia 2014/2015 kiasi cha shilingi milioni 85.58 kilitumwa kwa wafanyakazi watatu kwa niaba ya wafanyakazi wengine kwa ajili ya kugharamia usafiri, mafunzo, mkutano, malazi, na posho mbalimbali. Utaratibu wa kuwapa hela nyingi wafanyakazi wa mfuko ambazo menejimenti haina udhibiti wa moja kwa moja inaongeza hali ya hatari ya wizi na ubadhilifu.	Menejimenti inashauriwa kuanzisha sera za kusimamia fedha na kuweka utaratibu utakaopunguza uwezekano wa kutuma hela kwenye akaunti za wafanyakazi ili kupunguza uwezekano wa wizi na ubadhilifu.
4	**MAMLAKA YA**	**Makusanyo kupitia MAXCOM ambayo hayakuwasilihwa**	

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
	MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MBEYA	**Shilingi milioni 400.52**	
		Mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira Mbeya iliingia mkataba na MAXCOM AFRICA LIMITED kukusanya pesa kutoka kwa wateja kupitia M-Pesa. Jumla ya Shilingi milioni 400.52 zilikusanywa kupitia utaratibu huu kwa mwaka wa fedha 2015/16. Kufuatia utaratibu huu, nilibaini kuwa Shilingi milioni 127.73 sawa na asilimia 32 ya jumla ya makusanyo kupitia MAXCOM iliwasilishwa kwa mamlaka lakini hazikuwekwa kwenye akaunti ya benki na uongozi. Pia, Shilingi milioni 272.79 sawa na asilimia 68 ya jumla ya makusanyo kupitia MAXCOM hazikuwasilishwa kwa mamlaka. Kwa kutoweka makusanyo hayo kwenye akaunti za benki kwa wakati, menejimenti inaweka mianya ya udanganyifu kwakuwa fedha inawepesi wa kuibiwa. Pia kutowasilisha makusanyo ya mapato kwa mamlaka kunaathiri utendaji kazi wa mamlaka.	Menejimenti inashauriwa kufanya ufatiliaji wa karibu kwa MAXCOM AFRICA LIMITED ikiwa ni pamoja na kurekebisha mkataba wa awali ili kutekeleza kwa haraka uwasilishaji wa fedha zilizokusanywa. Pia, fedha zinazokusaywa ziwekwe kwenye akaunti ya benki kwa kadiri ya zinavyokusanywa kama sera ya mamlaka inavyotaka.
5	**TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)**	**Kuwepo kwa maendeleo hafifu katika mradi wa Uporoto**	
		Mnamo mwaka 2013 TCU iliingia katika kutoa huduma za ushauri wa usanifu wa majengo pamoja na usimamizi kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za kudumu za TCU katika eneo la Uporoto. Gharama ya Shilingi milioni	Menejimenti inashauriwa kufanya maamuzi kuhusu muendelezo wa mradi huu.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		126 zilitumika kuendeleza jengo hilo la Uporoto na kuripotiwa katika taarifa za fedha kama kazi inayoendelea, Aitha nilibaini ya kwamba hakukuwa na maendeleo yoyote katika mradi huu kwa miaka 3 iliyopita tangu kuanzishwa kwa mradi.	
6	**CHUO KIKUU CHA ARDHI**	**Kushindwa kutekeleza mradi kwa wakati**	
		ARU ina jumla ya miradi mitano. Kati ya hiyo, miradi miwili ni mikubwa yenye thamani ya shilingi milioni 642.70 na miradi mitatu ni midogo yenye thamani yashilingi milioni 698.40 na kufanya jumla ya Shilingi bilioni 1.34. Hadi kufikia sasa, miradi yote imekigharimu chuo jumla ya shilingi milioni 906. Nilibaini kuwapo kwa ucheleweshwaji wa kukamilisha miradi hiyo kwa zaidi ya miaka mitatu kinyume na matakwa Kanuni ya 114(b) ya manunuzi 2013 inayoitaka taasisi inayofanya manunuzi kuwajibika kwa ufatiliaji na usimamizi bora wa miradi na kuhakikisha ukamilishwaji wa shughuli za miradi kwa wakati. Kuchelewa kukamilika kwa mradi kutasababisha kushindwa kufikia malengo na pia kusababisha kuongezeka kwa gharama kutokana na mfumuko wa bei, hivyo kulazimisha ongezeko la fedha za ziada ili kukamilisha miradi hiyo.	Menejimenti ya ARU inashauriwa kuhakikisha kwamba miradi inakamilishwa bila kusababisha ucheleweshaji zaidi utakaopelekea ongezeko la gharama za kukamilisha miradi.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		Deni la muda mrefu la shilingi milioni 631.7	
		Chuo kimekuwa na deni la muda mrefu la shilingi milioni 631.7. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi milioni 313.6 zinawasilisha wakala wa serikali ambao ni HESLB (Shilingi milioni 178.6), Wizara ya ardhi na maendeleo ya makazi (Shilingi milioni 62.7) NHIF (shilingi milioni 201.3) na kiasi cha shilingi milioni 116.8 kinawakilisha wazabuni waasiojulikana walioweka fedha kwenye akaunti ya benki ya chuo. Ucheleweshaji wa kuilipa serikali/wasambazaji/ watoa huduma kwa wakati inaweza kuathiri uwezo wa kukopesheka wa chuo kikuu. Pia, deni la muda mrefu linatia shaka ya uhalali na usahihi wake.	Chuo kifanye uchunguzi wa madeni yote ya muda mrefu. Kisha, itathmini kama madeni hayo ni ya kweli na ya halali na kutafuta namna ya kuweza kulipa madeni hayo bila kuchelewa zaidi.
7	**BOHARI KUU YA MADAWA**	**Ongezeko la ada la mwaka lisilokuwa na uhalisia**	
		Hospitali ya Taifa ya Muhimbili iliingia mkataba wa huduma na kituo cha ufumbuzi wa afya cha M/s. NAPIER (India) kwa ajili ya msaada wa kiufundi wa JEEVA kwa kiasi cha shilingi milioni 172.9 kwa mwaka. Mkataba ulitoa nafasi ya ongezeko la asilimia 12 kwa mwaka ikiwa ni ongezeko la athari ya kushuka kwa thamani ya fedha (Shilingi milioni 196.7). Hata hivyo, kiwango cha asilimia 12 kwa	Usimamizi kupitia na kujadili na kusaini mkataba mpya na NAPIER Healthcare (India) ltd kwa lengo la kupunguza kiasi cha athari ya kushuka thamani ya fedha ili kiendane na kiasi cha mfumko wa bei unaotangazwa na benki ya India.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		mwaka ni ongezeko kubwa sana kulinganisha na inavyoainishwa na benki ya India ambayo ndio huchapisha viwango vya mfumuko wa bei kila mwaka kwa miaka 5 iliyopita na ndio mtoa huduma anapofanyia shughuli zake za msingi. Tovuti ya akiba ya Benki ya India imeainisha kiwango cha mfumuko wa bei nchini India kuwa wastani wa asilimia 7.48 kwa mwaka kuanzia mwaka 2012 hadi 2016. Ongezeko la asilimia 12 kwa mwaka iliyoombwa na M/S NAPIER ni takribani mara mbili ya kiwango kinachoonekana. Kadhalika, bili hii iko katika sarafu ya dola ambayo ni fedha imara kuliko RUPII ya Kihindi, pia kasi ya mfumuko wa bei ya kila mwaka ya Marekani kwa miaka mingi imebakia chini ya asilimia 2.5. Udhaifu katika kusimamia mikataba na majadiliano inaleta athari ya kutoza gharama za juu na kuleta hasara kwa taasisi.	
8	**BODI YA TAIFA YA UHASIBU NA UKAGUZI (NBAA)**	**Kushindwa kulipa deni la NSSF Shilingi bilioni 8.93 kwa mwaka 2015/2016**	
		Tarehe 1 Novemba 2010, Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA) iliingia mkataba na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kupewa mkopo wa Shilingi bilioni 15 wenye asilimia 100 ya	Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA) inashauriwa kufikia muafaka na NSSF kuhusu ongezeko la deni hilo na kulifanya jengo la APC liwe la kibiashara ili

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		dhamana ya Serikali kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Taaluma ya Uhasibu (APC). Niligundua kuwa Bodi imeshindwa kusimamia mkopo huo kwa kuwa mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2016 ilikuwa inadaiwa Shilingi bilioni 8.93.	kuweza kuzalisha fedha za kulipa mkopo huo.
9	**HIFADHI ZA BAHARI NA MAENEO TENGEFU (MPRU)**	**Kuwapo kwa kambi ya wavuvi katika Hifadhi ya Eneo Tengefu Nyororo**	
		Kisiwa cha Nyororo kilitangazwa kuwa Hifadhi ya eneo tengefu kupitia Tangazo la Serikali namba 52 lililochapishwa tarehe 2 Machi 2007. Kifungu Na. 4 cha Sheria ya Uvuvi (Marudio 2002) kinasema, hakuna mtu atakayeruhusiwa kuingia au kukaa kwenye hifadhi ya bahari bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa Mkurugenzi wa Uvuvi". Hata hivyo, kulikuwa na wavuvi 200 katika kisiwa hicho licha ya Menejimenti kutoa barua yenye kumbukumbu na. BC.152/230/02/12 ya tarehe 4 Julai 2016 inayowataka wavuvi hao kuondoka mara moja. Kuwapo kwa kambi za wavuvi unaongeza hatari ya uvuvi wakutumia baruti ambazo hudhuru miamba ya matumbawe na maeneo ya uzalishaji.	Hifadhi ikishirikiana na Wizara husika inatakiwa kuhakikisha wavuvi hao wanaondoka mara moja ili kuendelea kutunza mazingira ya hifadhi.
10	**KAMPUNI YA NYUMBA ZA WATUMISHI**	**Ukosefu wa Bima kwa Ujenzi wa Miradi ya Shilingi billioni 1.95**	
		Majengo ya Kampuni ya	Mfuko wa WHC-REIT

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
	(WHC)	Shilingi billioni 1.95 hayajakatiwa bima katika gharama kamili ya ujenzi kama inavyotakiwa na Kifungu Na. 51(8) cha Sheria ya Masoko ya Hisa na Mitaji pamoja na Kanuni zake za 2011. Majengo yaliyoendelezwa na Mfuko wa WHC-REIT kupitia wahandisi wa ndani yapo katika hatari mbalimbali ya kutorejeshwa kwa thamani ya jingo pindi ikitokea janga la moto au majanga asilia.	unatakiwa kufanya uchambuzi wa gharama na faida kwa kuweka bima ya majengo katika gharama nzima ili kuepuka hasara.
13	**BODI YA TUMBAKU TANZANIA (TTB)**	**Kupungua kwa Soko la Tumbaku na Sekta kwa Ujumla Tanzania**	
		Soko la Tumbaku limekuwa likipungua na wanunuzi wameanza kutoka kwenye soko. Mnamo Agusti 2016, kampuni ya Alliance One Tobacco Tanzania ilitoa taarifa rasmi kwamba itatoka kwenye soko mara moja baada ya kipindi cha mwaka 2018. Pia, baadhi ya wanunuzi wamejitoa wenyewe kwenye soko la Namtumbo na Songea. Hali hii inaonesha ushiriki hafifu na kuathirika kwa soko la tumbaku Tanzania. Hii itaathiri uchumi hasa ikizingatiwa tumbaku ni moja ya zao muhimu linalochangia uchumi wa taifa.	Menejimenti ya Bodi inashauriwa kutathmini hali hii na kufanyia kazi. Mikakati ya soko inatakiwa kubadilishwa ili kushinda ushindani wa kimataifa.
		Udhaifu katika Ukusanyaji Mapato na Udhibiti wa Rekodi	
		Imegundulika kuwa, Bodi inatumia mfumo wa fedha taslimu (cash basis) katika kuripoti taarifa za mapato	Menejimenti inashauriwa kuhifadhi kumbukumbu za miamala ya mapato ya mfumo usiokuwa wa

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		badala ya mfumo usiokuwa wa fedha taslimu (accrual basis). Mapato ya ada ya Shilingi milion 212.40 (sawa na Dola za Marekani milioni 0.91) ziliandikiwa Ankara katika kipindi cha mwezi Aprili na Juni 2016 lakini hazikuwekwa kwenye vitabu vya hesabu. Taarifa ya mapato isiyokamilika inaweza kusababisha ubadhirifu wa fedha, upotevu wa taarifa za wadeni na hivyo hasara kwa Serikali kwa kutokukusanya madeni husika.	fedha taslimu hata kama ankara haijapelekwa kwa mteja.
14	**NHC AND PPF COMPANY LIMITED**	**Uwepo wa Wapangaji Wasiokuwa na Mikataba**	
		Mapitio ya Mkataba wa ukodishaji yalionesha kuwa wapangaji 20 walikuwa hawana mikataba. Mikataba miwili ilikuwa imekwisha muda wake tangu 2014 na haikuhuishwa kufikia mwaka Juni 2016. Pia, niligundua baadhi ya mikataba ilikuwa haina ushuru wa stempu. Kushindwa kuingia mikataba inaathiri ufuatiliaji sahihi wa mapato na kunyima kampuni haki yake kwakuwa itakuwa ngumu kushinda mbele ya mahakama.	Menejimenti inashauriwa kuhakikisha mikataba inakuwepo kwa kila mpangaji ili kuepuka kuvuja kwa mapato na kuhakikisha haki za kampuni zinalindwa.
15	**SHIRIKA LA UTANGAZAJI TANZANIA (TBC)**	**Ukosefu wa Vifaa Muhimu vya Utangazaji**	
		Niligundua kuwa TBC haina vifaa muhimu vya shughuli ya matangazo. Upungufu wa kila vifaa ni kati ya asilimia 31 hadi 467. Hali hii inazuia	Menejimenti ya TBC inatakiwa kushirikiana na Serikali kuona ni jinsi gani upungufu huu wa vifaa unaweza

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		uwezo wa TBC kufanya shughuli zake kwa ufanisi na hivyo kuathiri ufanisi wa uendeshaji.	kutatuliwa.
16	**MAMLAKA YA UDHIBITI WA USAFIRI WA NCHI KAVU NA MAJINI (SUMATRA)**	**Usimamizi Duni wa Masurufu ya Mamlaka**	
		Kanuni Na. 282 Na. 425 ya Kanuni za Fedha za Mamlaka inahitaji masurufu kurejeshwa ndani ya siku saba baada ya kumalizika kwa safari au kazi husika. Hata hivyo, niligundua kuwa kuna jumla ya Shilingi milioni 554 ambazo bado hazijarejeshwa na wahusika hadi kufikia 30 Juni 2016. Hali hii inaashiria udhibiti duni wa masurufu ambao unaweza sababisha makisio ya chini ya matumizi na matumzi mabaya ya fedha na Mamlaka.	Menejimenti ya SUMATRA inashauriwa kufuata kanuni na udhibiti wa ndani uliopo.

Kiambatisho III: Mashirika yasiyokuwa na Bodi ya Wakurugenzi au Bodi ya Wadhamini

Na.	Shirika la Umma
1	Bodi ya Katani(TSB)
2	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko(CPB)
3	Chama cha haki miliki Tanzania(COSOTA)
4	Mamlaka ya maendeleo ya Bonde la Rufiji (RUBADA)
5	Bodi ya Pamba (TCB)
6	Shirika la Chakula na Kituo cha Lishe Tanzania (TFNC)
7	Wakala wa wakulima wadogo wadogo wa chai Tanzania (TSHTDA)
8	Shirika la Ukaguzi na usimamizi wa vyama vya Ushirika (COASCO)
9	Kituo cha uwekezaji Tanzania (TIC)
10	Shirika la kuendeleza miradi na miundombinu UTT (UTT-PID)
11	Chuo cha kumbukumbu ya mwalimu Nyerere (MNMA)
12	Taasisi ya Taifa ya Uchunguzi wa magonjwa ya Binadamu (NIMR)
13	Chuo cha Taifa cha Sukari (NSI)
14	Shirika la kusimamia Mali na huduma kwa wawekezaji (UTT - AMIS)

Na.	Shirika la Umma
15	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama
16	Kampuni ya mbolea Tanzania (TFC)
17	Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)
18	Kampuni ya kusimamia Ralisilimali za Shirika la Reli Tanzania (RAHCO)

Kiambatisho IV: Kaguzi ambazo hazikufanyika kwa sababu ya kutokuwa na Fedha.

Na.	Jina la Shirika la Umma
1	Mamlaka ya Maji Safi Mpanda
2	Mamlaka ya Maji Safi Korogwe
3	Mamlaka ya Maji Safi Kyela
4	Mamlaka ya Maji Safi Karatu
5	Shirika la Uhandisi na Ubunifu wa Viwanda Tanzania (TEMDO)
6	Kampuni ya Marine Services
7	Mamlaka ya Maji Safi Ngara
8	Mamlaka ya Maji Safi Muleba
9	Chuo cha kilimo na teknolojia Julius K. Nyerere
10	Mamlaka ya Maji Safi Bariadi

Kiambatisho V(a): Mapendekezo yaliyopita kwenye masuala muhimu ya ukaguzi

Na.	Aya	Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali	Maoni ya Mkaguzi
		Mwaka wa Fedha 2008/2009		
1	**3.2.2**	**Mkopo wa Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Umma Shilingi Bilioni 53 kwa Bodi ya Mikopo** Mkopo wa PSPF Shilingi bilioni 53 kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu bado haujarejeshwa kwa zaidi ya miaka 9 sasa. Mpaka kufikia tarehe 30 mwezi Juni, 2015 Serikali	Tayari Serikali imemuagiza Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali kuhakiki madeni yote ya Serikali kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hivyo deni la PSPF litalipwa pale uhakiki utapokamilika na kushauriwa kufanya hivyo.	Naendelea kusisitiza kwamba, Serikali ihakikishe inalipa deni lililobaki ili kuepuka gharama Zaidi za riba na adhabu ya kuchelewesh

Na.	Aya	Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali	Maoni ya Mkaguzi
		imeshalipa Shilingi bilioni 21.9 kwa PSPF; hivyo, kubakiwa na deni la Shilingi bilioni 40 inayojumuisha adhabu ya kuchelewesha marejesho. *Serikali inapaswa ichukue hatua kuhakikisha kwamba inalipa ya deni lote la mkopo huu (ikiwa ni kiasi cha mkopo na riba) uliokopwa kutoka Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Umma inalipwa, ili kuepuka gharama zaidi za riba na adhabu itokanayo na kuchelewa kulipa mkopo husika.*	(i) Mwaka 2006 na 2007 Serikali iliidhamini Bodi ya Mikopo kulipa deni lake la Shilingi bilioni 53 kwa PSPF. (ii) Kwa ajili ya kuharakisha malipo ya deni la Serikali kwa PSPF, mwezi Februari, 2016 Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali chini ya maelekezo ya Wizara ya Fedha na Mipango alifanya uhakiki wa deni la mkopo uliopewa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) (iii) Ripoti ya uhakiki imeonesha kuwa mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2015, Serikali ilikuwa imeshalipa Shilingi 21,948,080,195.48 kwa PSPF. Hivyo deni lililobaki ni Shilingi 40,330,467,749.72 lisilojumuisha adhabu ya kuchelewesha	a marejesho.

Na.	Aya	Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali	Maoni ya Mkaguzi
			marejesho.	
Mwaka wa Fedha 2010/2011				
2	3.3.1	**Majengo ya Shirika la Maendeleo ya Taifa Kwenye Kitalu Na.2338 yaliyopo Mbezi Beach, Barabara ya Bagamoyo Hayana Mkataba wa Pango** Nilibaini kuwa Shirika la Maendeleo la Taifa halina mkataba wa pango na mpangaji wa sasa wa jengo hilo, Messrs Vignan Education Foundation (IMTU) baada ya mkataba na Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC) kwisha mwezi Agosti, 2011. Vignan Education Foundation limekataa kukubali masharti ya mkataba ulioandaliwa na Shirika la Maendeleo ya Taifa ambao pamoja na mambo mengine una kodi ya mwezi ya Shilingi milioni 60, ambayo ilikadiriwa na mthamini. *Kwa hali hiyo, bado naendelea kusisitiza mapendekezo yaliyotolewa kwa Shirika la Maendeleo ya Taifa yatekelezwe na suala hili kupatiwa ufumbuzi.*	Suala hili limeshafikishwa mahakamani, Serikali kupitia NDC itaendelea kufuatilia taratibu za mahakama.	Naendelea kusisitiza mapendekezo yangu yaliyopita.
3	3.3.2	**Usimamizi wa Rasilimali za UDOM** Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Pensheni kwa	Taarifa za kuhamisha vifaa na thamani za Hospitali zipo Makao Makuu ya Wizara kwa ajili ya umaliziaji.	Naendelea kusisitiza mapendekezo yangu yaliyopita.

Na.	Aya	Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali	Maoni ya Mkaguzi
		Wafanyakazi wa Umma (PSPF), Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (LAPF), Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Pensheni wa PPF yalitumia jumla ya Shilingi bilioni 415.4 kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), chini ya makubaliano ya buni, jenga, endesha, na kisha hamisha miliki baada ya miaka kumi (10). Majengo haya hayapo kwenye vitabu vya Chuo Kikuu cha Dodoma wala katika vitabu vya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii husika. *Hivyo basi, naendelea kusisitiza majengo hayo kuingizwa kwenye vitabu vya UDOM kama nilivyopendekeza awali.*	Uhamishaji wa majengo bado haujafanyika. Hata hivyo, ujenzi wa awamu ya kwanza umeshakamilika tangu mwezi Oktoba, 2015 na inategemewa kukabidhiwa na Mkandarasi mwezi Oktoba 2016 baada ya kipindi cha uangalizi wa mradi kuisha.	
Mwaka wa Fedha 2012/2013				
4	3.5.2	**Umiliki wa Benki ya Azania** Benki ya Azania (hapo mwanzo ikiitwa 1st Adili Bancorp Limited) ni benki binafsi iliyoanzishwa mnamo mwaka 1995. Wanahisa wake ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (36%), Mfuko wa Pensheni wa PPF (30%), Mfuko wa Pensheni wa Watumishi Umma (12%), Mfuko wa Pensheni wa LAPF (14%), Benki ya Maendeleo ya	Serikali imekubali mapendekezo ya CAG na kwa kuwa Benki inamilikiwa na Mifuko ya Hifazi ya Jamii itawasiliana na wadau wake ili kupata njia nzuri ya kushughulikia jambo hili.	Naendelea kusisitiza mapendekezo yangu yaliyopita.

Na.	Aya	Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali	Maoni ya Mkaguzi
		Afrika Mashariki (2.3%), wafanyakazi wa Benki ya Azania na wanahisa wengine (1.4%). Mifuko ya Pensheni kwa pamoja inamiliki asilimia 92 ya hisa zote katika Benki hiyo. Hii inamaanisha kuwa Mifuko hii ina uwezo wa kuisimamia Benki hii kwa kutoa miongozo na maamuzi muhimu yanayohusu shughuli za uendeshaji. Kwa upande mwingine, Mifuko yote ya Pensheni inamilikiwa na Serikali kupitia Msajili wa Hazina. Kwa kuzingatia uhusiano huu, ni wazi kuwa Benki ya Azania inamilikiwa na Serikali kupitia Mifuko ya Pensheni. Benki ya Azania inatakiwa iwe chini ya Msajili wa Hazina, Hivyo, kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 9(a) iii na iv cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kinaitaka Benki hii kuwasilisha hesabu kwenye Ofisi yangu kwa ajili ya kukaguliwa.		
6	3.5.4	**Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo Vijijini (PRIDE Tanzania Limited)** Taasisi ya PRIDE Tanzania ilianzishwa mnamo tarehe	Pride Tanzania ilisajiliwa kama Kampuni yenye umiliki kwa dhamana na sio umiliki kwa	Nasisitiza kuwa, bado haijawekwa wazi ni kwa jinsi gani

Na.	Aya	Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali	Maoni ya Mkaguzi
		5 Mei, 1993 chini ya Sheria ya Makampuni (CAP 212) kwa dhamana. Madhumuni ya kuanzishwa kwa chombo hiki ni kutoa mikopo midogo midogo kwa wajasiriamali. Taarifa ya Msajili wa Hazina iliyoonesha kuwa uwekezaji wa Serikali katika kampuni hii. Kufikia tarehe 30 Juni, 2008, ilionyesha kuwa hisa zote za PRIDE zinamilikiwa na Serikali. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa ya Msajili wa Hazina inayoishia tarehe 30 Juni, 2012, Shirika hili liliondolewa katika orodha ya Mashirika ya Umma. Uhalali na sababu za kuondolewa kwa Shirika hili katika orodha ya Msajili wa Hazina haukuweza kubainika. Kwa mujibu wa kifungu cha 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, kila Shirika la Umma linatakiwa kupeleka hesabu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukaguliwa katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha. Hata hivyo, hesabu za PRIDE Tanzania hazijawahi kuwasilishwa kwenye Ofisi yangu kama inavyotakiwa na sheria.	hisa, hivyo Serikali haikuwa na hisa. Hata hivyo, Serikali ipo kwenye mchakato wa kuibadilisha PRIDE Tanzania kutoka Kampuni yenye umiliki wa dhamana na kuwa Kampuni yenye umiliki wa hisa chini ya Msajili wa Hazina ambaye atakuwa na umiliki wa Kampuni kwa asilimia 100.	umiliki wa serikali katika shirika ulivyo hamishwa kwenda kwa wamiliki binafsi. Hivyo basi, ninaendelea kusisitiza kuwa Msajili wa Hazina anapaswa kufuatilia kwa karibu juu umiliki wa kisheria wa hisa/dhamana za PRIDE Tanzania zilizokuwa zinamilikiwa na Serikali na baadaye kuamishiwa kwa wamiliki binafsi.

Na.	Aya	Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali	Maoni ya Mkaguzi
		Pamoja na majibu ya serikali kuwa kampuni imeacha kupata fedha kutoka Serikali ya Kifalme ya Norway na Tanzania mwaka 2005, haijawekwa wazi jinsi hisa za kampuni hii zilivyohamishwa kwenda kwa wamiliki binafsi. *Hivyo basi ninaendelea kusisitiza kuwa Msajili wa Hazina anapaswa kufuatilia kwa karibu juu umiliki wa kisheria wa hisa za PRIDE Tanzania zilizokuwa zinamilikiwa na Serikali na baadaye kuamishiwa kwa wamiliki binafsi*		
Mwaka wa Fedha 2014/2015				
8	4.4.1	**Ongezeko la hasara katika thamani (Actuarial) na kutokulipwa kwa deni la Serikali** Ripoti ya Tathmini (Actuarial) ya Mfuko ya mwaka 2014 inaonesha kwamba, Mfuko una hasara ya thamani ya Shilingi trilioni 11.15 (2014: Shilingi trilioni 6.49 kwa mujibu wa tathmini iliyofanyika mwaka 2010). Msingi wa hasara hii ni matokeo ya Serikali kuchelewa kulipa madeni ya mafao ya wanachama waliokuwepo kabla ya kuwanzishwa kwa Mfuko tarehe 01 Julai 1999. Pia, Mfuko una madai ya	Serikali inatambua deni lililotokana na kuchelewa kulipa madeni ya mafao ya wanachama waliokuwepo kabla ya kuanzishwa kwa Mfuko tarehe 1 Julai, 1999. Kwa sasa mipango ya kulipa deni hilo kupitia hati fungani inaendelea. Zaidi, Serikali inalipa deni kwa marejesho ya Shilingi bilioni 76.1 kila mwaka ili kutimiza lengo la Mfuko la kulipa mafao wastaafu. Pia, Serikali	Naendelea kusisitiza mapendekezo yangu yaliyopita.

Na.	Aya	Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali	Maoni ya Mkaguzi
		mikopo kutoka taasisi za Serikali yenye thamani ya Shilingi bilioni 499.7 kufikia tarehe 30 Juni 2015 (2014: Shilingi bilioni 382.9). *Serikali inashauriwa kuusadia Mfuko kulipa deni lililobaki hususani kwa Hati Fungani kama inavyopendekezwa. Hii itasaidia uwezo wa Mfuko kufikia majukumu yake yakiwemo mafao kwa wanachama wastaafu. Pia, taasisi zinazohusiana na Serikali zinashauriwa kuweka kipaumbele malipo ya madeni kutoka kwenye Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) ili kuokoa Mfuko katika hatari ya kufilisika.*	inatambua madeni yake yote kwa Mifuko ya Pensheni iliyowekeza kwa pamoja kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo, PSPF ikiwemo. Taratibu wa kulipa deni lililobaki kwa kutumia hati fungani zinaendelea. Malipo yatafanyika pindi zoezi la uhakiki likikamilika.	
12	4.15.1	**Utekelezaji wa Mkataba wa Ubia katika Mradi wa Mji wa Kisasa wa Arumeru kati ya NSSF na Azimio Housing Estate Ltd (AHEL)** Kama ilivyoonekana katika mwaka wa fedha uliopita na katika mwaka huu wa fedha, shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii ilianzisha mradi mwingine wa kujenga mji wa kisasa katika Wilaya ya Arumeru mkoa wa Arusha kupitia kampuni iliyoanzishwa kwa ubia na kampuni ya Azimio kwa jina la Hifadhi Builders Ltd	Serikali imekubali mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na itahakikisha kabla ya kuingia makubaliano na Mwekezaji kwenye mradi wowote. NSSF ina pesa za kutosha kwa ajili ya kutekeleza makubaliano hayo.	Kuingia katika mradi bila kujihakikishia uwepo wa fedha kungeweza kusababisha gharama zisizo za lazima pamoja na matumizi mabaya ya rasilimali kwa upande wa shirika. Hivyo,

Na.	Aya	Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali	Maoni ya Mkaguzi
		Kifungu cha 5 cha mkataba huo kinaonesha kuwa pande zote zimekubaliana kutoa kiasi cha mtaji unaofikia Dola za Marekani bilioni 3.34 (Shilingi Trilioni 7.2) na ushauri wa kiufundi kwa ajili ya uanzishaji wa mji huo wa kisasa; ambapo, asilimia 20 (sawa na Dola za Marekani milioni 668.12) imefanywa kuwa thamani ya ardhi. Azimio amekubali kutoa ardhi ya ekari 500 kwa ajili ya uendelezaji wa mradi huo. Katika ukaguzi, imeonekana kuwa shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii limepokea upembuzi yakinifu wa mradi pendekezwa kutoka Azimio Housing Estate Ltd kupitia barua yake ya tarehe 16 Mei 2013 yenye kumbukumbu Na. AZIMIO/NSSF/ARUMERU/13/5; ambapo, Bodi ya Wadhamini iliidhinisha kuingiza katika ubia ardhi iliyotolewa na kampuni ya Azania katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Mwanza na Arusha kwa ajili ya uwekezaji unaofanana na huu. Ada ya ushauri kwa ajili ya kubuni mradi huo ni Dola za Marekani milioni 218.09 (Shilingi bilioni 468.9) na ilipangwa Shilingi bilioni 2.4 itumike katika awamu		naendelea kusisitiza mapendekezo yangu yaliyopita.

Na.	Aya	Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali	Maoni ya Mkaguzi
		ya upangaji wa mradi. Hata hivyo, kiasi hicho kiliongezwa hadi kufikia Shilingi bilioni 102 bila ya idhini ya Bodi. Kiasi halisi cha ada ya ushauri mpaka kufikia mwisho wa mwaka kilikuwa Dola za Marekani milioni 20.1 (Shilingi bilioni 43.9) kutoka katika Dola za Marekani bilioni 102 za ongezeko. Tarehe 20 Januari 2016, shirika na kampuni ya Azania walisaini makubaliano ya kusitisha utekelezaji wa mradi huu kwa makubaliano ya pamoja. Uongozi wa shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii umetoa sababu ya kutokulipwa marejesho ya mikopo yake kutoka kwa Serikali kama sababu ya kusitisha mradi huo. Kama ilivyoainishwa katika makubaliano ya usitishaji, kiasi cha Shilingi bilioni 43.9 kilicholipwa na shirika kama sehemu ya ada ya ushauri ibadilishwe kuwa mkopo ambao utarejeshwa na kampuni ya Azimio kupitia sehemu ya Mauzo ya nyumba katika mradi wa Dege ndani ya miaka mitatu kwa riba ya asilimia 3 kwa mwaka. *Kuingia katika mradi bila kujihakikishia kuhusu kuwapo kwa fedha kungeweza kusababisha gharama zisizo za lazima*		

Na.	Aya	Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali	Maoni ya Mkaguzi
		pamoja na matumizi mabaya ya rasilimali kwa upande wa shirika. Uongozi unatakiwa kuhakikisha kuwapo kwa fedha za kutosha kuendesha mradi uliopangwa kabla ya kuingia katika mkataba. Pia, linapaswa na kuhakikisha kiasi cha Dola za Marekani milioni 20.1 (Shilingi bilioni 43.9) kinarejeshwa katika muda stahiki kwa kuzingatia mabadiliko ya thamani ya fedha kulingana na muda. Pia, kiasi cha riba kinatakiwa kuakisi kiasi cha riba kinatakiwa kuakisi kiasi kinachotozwa na soko.		
13	4.15.2	**Malipo yaliyofanywa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii kwa zaidi ya kiasi kilichokubaliwa cha Dola Za Marekani milioni 9.01** Katika mwaka wa ukaguzi 2014/2015 imegundulika kuwa mpaka sasa shirika limewekeza kiasi cha Shilingi bilioni 205.14 (makadirio ya Dola za Marekani milioni 123). Kampuni ya Azania imechangia kiasi cha ziada cha Dola za Marekani milioni 5.5 kwenye mradi husika. Makubaliano kati ya pande husika ni kuwa shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii litawekeza mpaka	Hakuna majibu	Utaratibu dhaifu wa ufuatiliaji wa uchangiaji wa kila mbia ungeweza kusababisha mbia mmoja kuchangia zaidi ya mbia mwingine, wakati mbia aliyechangia kidogo akiendelea kupata mgao wa mauzo ya nyumba kwa mgawanyo ulio katika makubaliano.

Na.	Aya	Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali	Maoni ya Mkaguzi
		pale thamani ya uwekezaji wao uwe sawa na thamani ya ardhi iliyotolewa na kampuni ya Azania, ndipo pande zote zianze kuchangia katika uwiano ulio sawa. Hii ina maana kuwa shirika la Hifadhi ya Jamii limechangia Dola za marekani milioni 9.01 zaidi ya kiasi kilichotakiwa kuchangia ili kuwa sambamba na vigezo vya makubaliano ya ubia. Uongozi unashauriwa kuhakikisha uwepo wa ufuatiliaji wa uchangiaji wa kila mbia kwenye mradi. Pia, viwango vya uchangiaji kwa mujibu wa makubaliano vizingatiwe.		Hivyo, naendelea kusisitiza mapendekezo yangu yaliyopita.
14	4.15.3	**Kutolewa kwa Mkopo zaidi ya asilimia 50 ya Thamani ya Mali za SACCOS** Katika kupitia uwekezaji ulio katika mfumo wa mikopo, imegundulika kuwa shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii limetoa kiasi cha mikopo kwa SACCOS tisa kinachozidi asilimia 50 ya thamani ya mali za SACCOSS husika kinyume na Sera ya kukopesha ya shirika. Upembuzi wa awali wa maombi ya mkopo ulionyesha kuwa SACCOS zimeomba kiasi ambacho hazikustahili. Hata hivyo, ushauri huo ulipuuzwa na	Hakuna majibu	Naendelea kusisitiza mapendekezo yangu yaliyopita.

Na.	Aya	Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali	Maoni ya Mkaguzi
		uongozi na maombi ya mkopo kuidhinishwa. Kukosekana Kwa ufanisi katika taratibu za kupitisha mikopo kunaliweka shirika katika hatari ya kutorejeshewa mikopo husika. *Uongozi unashauriwa kufuata taratibu na sera zilizoidhinishwa na Bodi ya Wadhamini katika utoaji wa mikopo kwa SACCOS.*		

Kiambatisho Na. V (b): Mapendekezo Yaliyopita kwenye Mapitio ya Mikakati na Uendeshaji wa Kiufanisi Katika Mashirika ya Umma ambayo hayakupatiwa majibu na Serikali

Na.	Aya	Hoja na Mapendekezo ya Ukaguzi
		Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)
1	5.1.1	**Tathmini ya Machakato wa Ubinasfishaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)** Serikali inashauriwa kufanya upembuzi yakinifu kati ya faida na hasara zinazoweza kupatikana kutokana na shughuli zozote za kibiashara zinanazohusisha ubinafsishaji pamoja na ushirikiano na sekta binafsi kabla ya kuingia mkataba wowote na sekta binafsi ili kuhakikisha maslahi ya umma yanalindwa.
2	5.1.2	**Kutokuwapo kwa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi vya Kibiashara** Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) inatakiwa kutengeneza mfumo, sera na mkakati wa usimamizi wa athari zinazoweza kujitokeza. Pia inapaswa

Na.	Aya	Hoja na Mapendekezo ya Ukaguzi
		kuanzisha na kuendeleza regista ya vihatarishi ikiwa ni pamoja na mapitio ya kila mwaka ili kuimarisha muundo wa uongozi unaoshughulikia vihatarishi. Pia, uongozi wa Shirika unashauriwa kuandaa mpango wa utelelezaji ambao utaboresha utendaji kazi wa Shirika na kuwa wa kisasa zaidi.
3	5.1.3	**Ukodishaji wa Ndege Usiokuwa na Faida** Kampuni iandae Mpango kabambe wa biashara baada ta kufanya uchambuzi wa kina wa ukodishaji wa ndege kabla ya kufanya maamuzi ya kuchukua mkopo kwenye Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) ili kukodi ndege zinazohitajika.
4	5.1.4	**Kukosekana kwa Mkakati Mahususi wa Kufufua Shirika** Kampuni ya Ndege Tanzania itengeneze mkakati utakaoliwezesha kurudi katika hali nzuri ya kifedha kwa kufanya tathmini ya kina kubaini sababu na matatizo yaliyopelekea kuwa na matatizo ya hali ya kifedha iliyopo, pamoja na kuboresha mifumo na namna ya kuendesha biashara hiyo ili kuwa na Shirika jipya lenye ufanisi na kujiendesha kwa faida.
5	5.1.5	**Kushindwa kupata vyeti muhimu vya usafiri wa anga** Kampuni ya Ndege Tanzania iweke utaratibu wa kuwajengea uwezo watumishi au kuwajiri watumishi wapya wenye sifa stahiki pamoja na kuwa na mpango wa kurithishana ujuzi kwa nafasi muhimu za uongozi wa Shirika ili kuwa na watumishi wasomi, wazoefu, waliohamasika na wenye uwezo wa kukabiliana na ushindani katika soko linalokuwa kwa kasi la usafiri wa anga. (i) Kampuni ya ndege Tanzania (ATCL) inatakiwa kupata vyeti vyote kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Kimataifa (IATA) pamoja na ukaguzi wa usalama wa usafiri wa anga. Kulingana na taratibu na kanuni za uendeshaji wa makampuni yote ya ndege kufuata taratibu za usalama za

Na.	Aya	Hoja na Mapendekezo ya Ukaguzi
		usafiri wa anga.
6	5.1.6	**Kuporomoka kwa Hali ya Kifedha ya Shirika** Ninapendekeza kuwa kuna ulazima Serikali iangalie changamoto zinazolikabili Shirika na kutafuta njia nzuri za kufanyia mageuzi Shirika la Ndege la Taifa na kuweka mfumo ambao utaliwezesha shirika kutoa huduma za kiushindani na pia kujiendesha kwa faida.
Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA)		
7	5.7.1	**Ukosefu wa Mpango Mkuu (Master Plan) wa Anga wa Nchi** Menejimenti inashauriwa kuandaa Mpango Mkuu wa Anga nchini ili kuboresha utekelezaji wa majukumu yake.
8	5.7.2	**Mapitio ya Mipango na Utendaji wa Menejimenti katika Mradi** (i) Menejimenti inashauriwa kufanya mapitio ya faida ya mradi wa ADSB na kuzingatia athari za kufilisika kwa muuzaji wa mfumo huo na gharama kamili zinazohitajika kuleta rada zenye uwezo kwa kutumia mfumo wa ADSB (ii) Uongozi unashauriwa kutengeneza mipango ya teknolojia ambayo itawajibika kwa uchunguzi na kipimo cha faida ya teknolojia kabla ya teknolojia mpya haijaweza kutumia na Mamlaka ya Usafiri wa Anga.
Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania (TCRA)		
9	5.7.3	**Uandaaji na Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Mwaka** (i) Menejimenti ya Mamlaka inapaswa kuwandaa mpango wa utekelezaji na kuendelea na ufuatiliaji wake katika mwaka mzima wa uendeshaji wa shuguli za mamlaka ili kupata mafanikio na kufikia lengo la mkakati huo. (ii) Mamlaka ya Mawasiliano inatakiwa kuhakikisha kuwa uandaaji wa mpango wa utekelezaji unaimarika ikiwa ni pamoja na kujumuisha

Na.	Aya	Hoja na Mapendekezo ya Ukaguzi
		viashiria na malengo katika kila shughuli inayotekelezwa.
10	5.7.4	**Kushindwa Kufanya Upembuzi Yakinifu Kabla ya Utekelezaji wa Mradi wa TTMS** Menejimenti inapaswa kuandaa mpango wa utekelezaji utakaoziwezesha mamlaka kufanya upanuzi wa matumizi ya moduli ya TTMS kwa ngazi ya juu kwa kuwashirikisha wadau wengine kama makampuni ya simu, Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania.
11	5.7.5	**Kuanzisha Mpango wa Ufuatilia Mauzo ya Muda wa Mawasiliano (ARMS)** Menejimenti inapaswa kubaini masuala ya muundo wa usimamizi na utawala bora katika kuimarisha mradi na kufanya tathmini ya vihatarishi vya mradi mzima ili kuongeza udhibiti wa kukusanya kodi ya mapato;
12	5.7.6	**Haja ya Matumizi Bora ya Moduli za TTMS** Ni muhimu kuhakikisha kuwa mawasiliano kati ya wadau muhimu yanaimarishwa ili kuhakikisha kwamba mahitaji yote maalamu yanabainika na kufanyiwa kazi toka mwanzo wa mradi ili kuepuka kuwa na mradi usiokidhi mahitaji yao.
13	5.7.7	**Ukosefu wa Mawasiliano Miongoni mwa Wadau Muhimu wa Mradi** (i) Taasisi za umma zinapaswa kushirikiana na wadau husika ili kuhakikisha kwamba miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa ubia wa sekta ya umma na sekta binafsi inalenga katika kupata thamani ya fedha. (ii) Ni muhimu sana upembuzi yakinifu na wa kina ufanyike kabla ya uamuzi wa utekelezaji wa mradi wowote mkubwa ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa mafanikio, faida inapatikana na kufikia malengo yaliyokusudiwa.
		Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)

Na.	Aya	Hoja na Mapendekezo ya Ukaguzi
24	5.7.10	**Kutofikia malengo ya viashiria muhimu vya ufanisi** Kuanzisha chombo cha kusimamia miradi ili kuhakikisha na upembuzi yakinifu unafanyika kikamilifu kabla ya utekelezaji wa miradi.
25	5.7.11	**Mapungufu Katika Uendeshaji na Udhibiti wa Karakana ya Meli ya Gati ndogo ya Nchi Kavu Dar Es Salaam** (i) Kuhakikisha kunakuwa na muunganisho na ushirikishaji wa wadau wote wa Bandari kama vile Wizara ya Fedha, Msajili wa Hazina, Wizara ya Uchukuzi na vyombo vingine vya utekelezaji kwenye kipindi cha mipango ya miradipamoja na kipindi cha utekelezaji wa miradi husika. (ii) Mamlaka ya Bandari kuupa kipaumbele ukarabati wa bandari ya Dar es Salaam ili kuiweka kwenye ushindani kwenye ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.
27	5.7.13	**Kusuasua kwa utekelezaji wa miradi iliyoainishwa kwenye Mpango Mkuu wa Bandari wa 2028** Kuhakikisha ujenzi wa gati 13 & 14 unakamilika mapema iwezekanavyo kwani kwa kutokamilika kunaathiri utekelezaji wa malengo ambayo Mamlaka imejiwekea Malengo mengi yanategemea kukamilika kwa gati namba 13 & 14.
28	5.7.14	**Mapungufu Kwenye Mkataba Baina ya TICTS na Mamlaka ya Bandari** (i) Mamlaka ya Bandari ikusanye maelezo kutoka kwenye mfumo wa kompyuta wa TANCIS ambayo yataionesha makontena yaliyopokelewa na TICTS na kuyalinganisha na idadi halisi yaliyopokelewa na TICTS. (ii) Serikali ipitie upya mkataba wa upangishaji wa TICTS ili kuona ni jinsi gani matakwa ya jamii yametekelezwa kwa kupitia mkataba huu. Pia, matakwa ya kisheria ya kuongezea muda mkataba huu kabla ya kuisha kwa muda kwa mkataba wa kwanza. Kutathmini na kuona kama kulikuwa na

Na.	Aya	Hoja na Mapendekezo ya Ukaguzi
		manufaa na pia kuwangalia kama kuna uwezekano wa kuuvunja mkataba huu. (iii) Menejimenti ya Mamlaka ya Bandari ifuatilie kwa karibu masuala ya TICTS na kuhakikisha inafuata vigezo na masharti ya mkataba wa upangishaji.
29	5.7.15	**Matengenezo ya Eneo la Kuhifadhia Mizigo la Kisarawe** Serikali ipitie upya maamuzi ya kuusimamisha mradi wa kujenga sehemu ya kuhifadhi mizigo ya Kisarawe ili kuhakikisha Mamlaka ya Bandari inatekeleza majukumu yake kwa upana ili kuongeza ufanisi.
Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)		
34	5.5.4	**Kukosekana kwa Utaratibu wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Gharama za Ubia** (i) Menejimenti inashauriwa kutengeneza sera ambayo itatoa mwongozo katika zoezi zima la ufuatiliaji na tathmini ya miradi kama inavyotakiwa na Kanuni na. 46 (2) ya Kanuni za Manunuzi za Mwaka 2013. (ii) Shirika la Maendeleo la Taifa lazima liimarishe mchakato mzima wa ufatiliaji na uthaminishaji kwa kuongeza kifungu ambacho bila kujali idadi ya hisa ambazo Shirika linamiliki katika mikataba ya ubia, mara kwa mara lazima kupitia na kupitisha ripoti za mapato na matumizi ya kampuni ya ubia ili kuhakikisha hakuna ongezeko la gharama na kupunguza mapato kwa ajili ya malipo ya mrahaba, kodi na mgawanyo wa gawio.
35	5.5.5	**Mapungufu katika Ununuzi wa Hisa za General Tyre (EA)** Serikali inashauriwa kutoa fedha zinazohitajika ili kuwezesha Shirika la Maendeleo la Taifa kupata umiliki wa uendeshaji wa Kiwanda cha Tairi cha General Tyre (EA).
36	5.5.6	**Mlolongo wa Maamuzi ya Serikali Unaochelewesha Uanzishwaji wa Miradi**

Na.	Aya	Hoja na Mapendekezo ya Ukaguzi
		(i) Serikali inashuriwa kuongeza kasi katika mchakato wa Kiwanda cha Tairi cha General Tyre (EA) ili kuwa kwenye nafasi nzuri ya kuvutia wawekezaji. (ii) Stadi za upembuzi yakinifu na upatikanaji wa rasilimali pamoja na tathmini ya mali ni muhimu zifanyike ili kubaini masoko, mwekezaji na mahitaji ya rasilimali za kufufua kiwanda. (iii) Serikali inashauriwa kufuatilia kwa haraka mchakato wa kumilikisha mashamba makubwa ya mpira kwa Shirika la Maendeleo la Taifa ili kuiwezesha kuvutia wawekezaji. (iv) Serikali inashauriwa kuratibu shughuli zote za wizara ili kuepusha ucheleshwaji usio wa lazima, Kama ilivyo sasa mwekezaji kulipia gharama zote za mradi, hatua madhubuti zichukuliwe kabla mwekezaji hajajitoa katika mradi kama inavyoweza kuwa ngumu katika suala la muda na kutenga kiasi cha pesa cha kumpata mwekezaji mwingine mwenye nia ya kuwekeza. (v) Serikali inashauriwa kufanya maamuzi kwa wakati muafaka ili kuepukana na ongezeko la gharama za miradi zisizo za lazima na hivyo kuchelewa kupata manufaa yaliyotarajiwa katika miradi. (vi) Kama Shirika la Maendeleo la Taifaa bado inaona mradi una manufaa, inabidi kushirikiana na wanahisa wengine kwa kuwangalia vyanzo vya nje vya fedha kabla ongezeko la gharama halijakwamisha mradi.
38	**5.5.8**	**Mapungufu katika Utekelezaji wa Mradi wa Mchuchuma na Liganga.** (i) Menejimenti inashauriwa kufanya tathmini ya uwezekano wa kuhakikisha kuwa serikali haipo katika hatari kwa kuingia makubaliano na washirika wa sekta binafsi. Iwapo hakuna njia mbadala ya kudhamini mkopo zaidi ya hati za uchimbaji za mradi kama ilivyopendekezwa katika mkataba, basi asilimia za umiliki zinapaswa

Na.	Aya	Hoja na Mapendekezo ya Ukaguzi
		kubadilika. (ii) Menejimenti inashauriwa kutafuta fedha na kuwalipa mara moja fidia raia wote waliohamishwa ili kuepuka madai yoyote hapo baadaye. (iii) Shirika la Maendeleo la Taifa iwasiliane na menejimenti ya Shirika la Umeme Tanzania ili kuweza kuwanzisha mjadala ambao utasaidia pande zote mbili za ubia kufikia muafaka mzuri wa mkataba wa manunuzi ya umeme.
		Shirika la Ugavi wa Umeme (TANESCO)
39	**5.6.1**	**Mapitio ya faida ya kampuni na ufanisi katika uendeshaji.** Menejimenti inatakiwa kuendelea kuchukuwa hatua stahiki za mda mfupi na mrefu katika kuhakikisha kwamba uwezo wa kifedha wa Shirika unaboreshwa kwa kutambua vikwazo vinavyorudisha nyuma ufanisi wake.

Kiambatisho Na. VI: Ripoti Zinazosubiri Kuidhinishwa na Bodi Husika

Na.	Shirika la Umma
1	Kituo cha Uwekezaji Tanzania
2	Mfuko wa Uwekezaji Tanzania wa Kusimamia Miradi na Maendeleo ya Ujenzi
3	Mfuko wa Uwekezaji Tanzania wa kusimamia Mali na Uwekezaji
4	Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa vyama vya Ushirika (COASCO)
5	Kampuni ya Uwekezaji ya NHC-PPF
6	Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogovidogo
7	Mamlaka ya Maji Makambako
8	Mfuko wa Uwekezaji wa Nyumba wa Watumishi
9	Chuo cha Kilimo cha Sokoine
10	Chuo cha Ufundi Stadi Tanzania (VETA)
11	Chuo cha Elimu Watu Wazima
12	Chuo cha Uhasibu Arusha
13	Taasisi ya Taifa ya Sukari
14	Taasisi ywa Utafiti wa Viwanda na Maendeleo
15	Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu
16	Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere
17	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam
18	Kampuni ya Ranchi za Taifa

Na.	Shirika la Umma
19	Kampuni ya Mbolea Tanzania
20	Kampuni ya Magazeti Tanzania
21	Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli Tanzania
22	Mamlaka ya Maji Kahama
23	Kampuni ya Mawasiliano Tanzania
24	Baraza la Taifa la Biashara
25	Bodi ya Pareto Tanzania
26	Bodi ya Korosho Tanzania
27	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko
28	Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)
29	Baraza la Ujenzi la Taifa
30	Bodi ya Pamba Tanzania
31	Kituo cha Chakula na Lishe Tanzania
32	Bodi ya Katani Tanzania
33	Mamlaka ya Rufaa ya Manunuzi ya Umma (PPAA)
34	Mamlaka ya maendeleo ya Bonde la Rufiji -RUBADA
35	Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA)
36	Bodi ya Kahawa Tanzania
37	Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania
38	Baraza la Sanaa la Taifa